# KCSE 2023 REPLICA

# KISWAHILI

## (KCSE PREDICTIONS 1-10)

*Series of Exclusive Set of Expected Questions Predicted in the Final KCSE 2023 Examinations Scheduled for November 2023.*

*A REPLICA OF QUESTIONS TO EXPECT IN FINAL KCSE 2023 EXAMS.*

---

## CONFIDENTIAL!

---

***For Marking Schemes***

***Mr Isaboke 0746 222 000 / 0742 999 000***

## SUCCESS TO ALL CANDIDATES

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 1

# KISWAHILI

Paper 1

**Time: 1¾ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education*

**MAAGIZO**

***1.*** *Andika insha* ***mbili****. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima.***

***2.*** *Kisha chagua insha moja nyingine kutoka kwa hizo tatu zilizobakia.*

***3.*** *Kila insha isipungue* ***maneno 400***

***4.*** *Kila insha ina* ***alama 20***

***5.*** *Kila insha* ***lazima*** *iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| | 1 | 2 | 3 | 4 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| SWALI | | | | | |

# MASWALI

**1. LAZIMA**

Andika hotuba utakayotoa katika mkutano wa vijana uliondaliwa na katibu wa baraza wa mawaziri wa uratibu wa ndani bwana **Profesa Kithure Kindiki** katika kaunti yako ukilalamika madhara ya pombe haramu huku ukipendekeza njia za kukabiliana nayo.

**2.** Fafanua jinsi ambavyo Elimu huchangia kupata umoja wa kitaifa.

**3.** Andika insha inayoambatana na methali;-

**Mui huwa mwema;-**

**4.** Andika insha itakayo malizika kwa maneno;

**"….Nilipogutuka nilikuwa nimezungukwa na aila yangu huku hali ya wasiwasi ikiwa imetanda."**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 1

# KISWAHILI

Paper 2

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

## *Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

***(a)****Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

*(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

*(c) Jibu maswali yote.*

***(d)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

***(e)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

## 1. UFAHAMU (ALAMA 15)

***Soma masimulizi yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Tuliongozana sote watatu hadi ofisi ya *Hatubagui Publishers*. Njiani Pam aliyenichukulia zawadi, alinichangamkia na kunizungumzia kama kurumbiza. Tim alijitia tabasamu bandia, lakini kainama kama kondoo. Haikosi alibeba mazito moyoni.

Meneja wa uchapishaji wa kampuni hiyo ya uchapishaji alikuwa mwanamme mmoja wa makamo, mwembamba, aliyevalia miwani. Alikuwa hana ubaguzi hasa. Alitupokea kwa mawili-matatu hata kabla ya kutujua sisi nani. Hakuwa na vikwazo vya kumwona. Nilipojitambulisha kwake alionyesha msisimko mkubwa.

"Umemlanda babako kweli kweli, hukumbakisha," alimaka. "Hamjambo?"

"Mgonjwa, ndio maana amenituma kwako," nikajibu. "Ataka ajue diwani yake itachapishwa lini? Mbona nyie wachapishaji mnakawia sana na miswada ya watu? Kama muswada ni mbaya hauchapishiki rejeshea mwenyewe haraka."

"Lo! Hajapokea kifurushi chetu bado?" aliniuliza meneja.

"Kipi?"

"Diwani ya Mzee Sululu tuliichapisha miezi sita iliyopita. Tulimtumia nakala zake sita kwa njia ya posta."

"Kweli?"

"Basi hajazipata bado?"

"Nimetoka nyumbani siku chache zilizopita na alikuwa bado hajapata chochote."

"Basi wafanyikazi wa posta wamenyakua kifurushi hicho. Wengi wao ni kama paka waliowekwa kulinda kitoweo. Kawaida yao kudondoa mali za watu, na kuzichelewesha barua kufika."

Meneja wa uchapishaji alinyanyuka kitini. Akafungua kabati alimotoa nakala sita za diwani ya babangu akazitia kwenye katoni ndogo na kunipa.

"Mpelekee Mzee nakala hizi," akaniambia.

"Ahsante bwana," nikamshukuru. "Amesubiri miaka zaidi ya kumi na kitu tangu kuwasilisha muswada wake. Hapana shaka kwamba atafurahi sana. Alikuwa anahofia kupatwa na kifo pasi kukiona kitabu chake kwenye chapa."

"Na hii hapa nakala yako Bwana mdogo," alinipa nakala moja ya kitabu hicho.

Kilikuwa na jalada ya binti mrembo na anwani Kero za Mkiwa. Nilishukuru, tukamuaga na kwenda zetu.

Hayawi hayawi huwa. Ndoto ya baba imetimia hatimaye. Furaha yangu kwa kukiona kitabu cha babangu mahabubu kimechapishwa ilihafifisha mengine yaliyonitendekea kutwa hiyo, mabaya na mazuri. Nilitafahari. Niliterema. Nilijitanua kifua. Hatubagui publishers sio kampuni uchwara ya uchapishaji. Ni miongoni mwa mashirika ya uchapishaji vitabu yenye kuheshimika sana nchini. Baba alikuwa kafaulu kutenda kilichowashinda hata baadhi ya wanachuo, licha ya kisomo chake haba. Ari na bidii yake havikwenda bure yao. Subira yake ilikuwa imevuta heri.

Nilikumbuka alivyojiendeleza mwenyewe kimasomo baada ya ya kuhitimu elimu ya ngumbaru. Nikafikia hitimisho kuwa nia ni nguzo muhimu katika maisha ya binadamu; humkokota mtu ikamfikisha kusikotarajiwa katu.

***(Kufa Kuzikana - Ken Walibora(2003) uk 51-53)***

## MASWALI

**a)** Linganua hasia za marafiki za msimulizi walipokuwa njiani**.** **(Alama 2)**

**b)** Meneja wa Hatubagui Publishers ni mtu mbaraza. Toa ushahidi kifunguni. **(Alama 3)**

**c)** Kifungu hiki kinaonyesha hali kadha za kutamausha. Thibitisha. **(Alama 3)**

**d)** Kwa kumrejelea Mzee Sululu, tetea kauli "…nia ni nguzo muhimu…humkokota mtu ikamfikisha**…"** **(Alama 2)**

**e)** Tambua mbinu zozote tatu za lugha zilizotumika kifunguni. **(Alama 3)**

**f)** Fafanua maana ya vifungu hivi kama vilivyotumika kwenye masimulizi. **(Alama 2)**

**i.** Haikosi alibeba mazito moyoni

**ii.** Ni paka waliowekwa kulinda kitoweo

## 2. UFUPISHO (ALAMA 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Je, mtazamo hasi ni nini? Huwa na athari gani kwa binadamu? Mtazamo hasi ni kukata tamaa, kutamauka kuhusu hali, mtu au jambo fulani. Ni hisia ya kutotaka kushiriki wala kuhusishwa na jambo au hali fulani. Mtazamo huu ndio huwafanya wanafunzi kuchukia au hata kudunisha baadhi ya masomo na walimu wanaoyafundisha. Licha ya wengi kuwa na mtazamo huu, kwa kweli huwa hawatambui. Asilimia kubwa ya wanaotambua hutatizika kujikwamua kutoka katika hali hii.

Inakadiriwa kwamba mtu wa wastani huwa na takribani mawazo elfu sitini ya kibinafsi kwa kila saa 24. Asilimia 95 ya fikra hizi huwa sawa na siku iliyotangulia na asilimia 80 ya fikra hizi zilizorudiwa huwa hasi. Isioshe, fikra hizi nyingi hutokea bila mtu mwenyewe kutambua na huwa ni mazoea. Hii ina maana kwamba watu wengi hawana ufahamu wa atahri za fikra hizi maishani mwao.

Mitazamo hasi ina vyanzo na pia suluhu. Mwanzo kabisa ni imani potovu. Hiki ndicho chanzo cha mitazamo hasi. Kushikilia imani potovu kuhusu maisha pamoja na matukio fulani maishani hujenga mtazamo hasi. Unayaona maisha kwa macho ya imani zako na iwapo imani hizo ni potovu basi hutayathamini maisha yako. Ili kukabiliana na hali hii, sharti kwanza ubadili imani yako. Uamini kwamba mabadiliko yanaweza kutokea na uchukue hatua ya kuanzisha mabadiliko hayo

maishani mwako. Unahitaji kuepuka fikra hasi zinazoambatana na maisha yako ya awali na kulithamini kila tukio maishani kama tukio huru; lisilo na uhusino na yaliyowahi kukutamausha.

Kujikwamua kutoka katika imani duni unahitaji kuibuka na idadi kubwa ya imani chanya kuliko zilizo hasi kuhusu hali mahususi. Baada ya hilo, zikabili imani zako potovu moja baada ya nyingine huku ukijiuliza endapo imani hizo ni kweli na endapo zina mashiko. Tumia dakika tano hivi kila siku kushadidia fikra chanya inayokinzana na ile inayokudidimiza. Ukifanya hivi kwa takribani siku thelathini imani yako itaanza kuchukua mkondo unaofaa. Familia yako na rafiki unaoandamana nao huathiri pakubwa hisia zako. Wakiwa na mtazamo hasi huweza kukushawishi ukaanza kuhisi wanavyohisi na kuyaona mambo kwa mtazamo wao. Kukabiliana na hali wapaswa kudhibiti hisia zako.

Tawala namna unavyohisi na kukabiliana na hali mbalimbali bila kuathiriwa na wandani hawa. Epuka wandani wa aina hii kadri inavyowezekana, ikiwezekana, jitenge nao ili ujifunze kuwa na uhuru wa kufanya maamuzi yako binafsi bila kuathiriwa nao. Unapaswa kupunguza ushirika hata na jamaa zako wanaokuingiza katika hali ya kutamauka. Punguza muda wa kukaa nao hasa wanapogeukia mkondo huu wa kukukatiza tamaa.

Mazingira hasi ni kizingiti kingine. Pengine huoni ukuruba baina ya maisha yako na mazingira unamokulia au unamokaa. Ukweli ni kwamba, huenda umedumu katika mazingira hayo na kuyaozoea hata ukafikiri huwezi kuyabadilisha. Kadri unavyohisi huna uwezo wa kuyabadilisha ndivyo unajizamisha zaidi katika mtazamo hasi. Ili kukabiliana na hali hii, unahitaji kuelewa kwamba fikra zako au za watangulizi wako ndizo zilikuingiza katika mazingira haya. Kwa hivyo, unapaswa kubadili mkondo wa fikra zako na kuanza kujaribu mazoezi ambayo umekuwa ukiyaona kama usiyoyaweza. Hatua kwa hatua utagundua panapo jitihada na uelekezi unaofaa kwamba mazoezi hayo yamekuwa mepesi na hivyo kukubakishia kuyabadilisha mazingira yako.

Unapojikuta ukilalamika jinsi ulivyokerwa na hali fulani, hii ndiyo sababu ya kuwa na mtazamo hasi kuhusu hali hizo. Inaweza kukuwia vigumu kulikubali hili lakini kadiri utakavyolikubali mapema ndivyo utayaboresha maisha yako mapema. Kulalamika tu kutakudunisha katika hali zisizokuridhisha. Kwa hivyo ili uyabadilishe maisha yako, sharti ukome kulalamika tu kuanza kujikwamua toka kwenye hali hizo. Katika kufanikisha jambo lolote jema sharti viwepo vizingiti njiani. Mtendaji wa jambo lolote jema liwalo ana jukumu la kuibuka na mikakati mwafaka ya kuvikabili vizingiti hivi ili afanikishe ndoto yake. Hii huwa chanya. Kwa jinsi hii utayabadilisha maisha yako yawe ya kuridhisha zaidi na kuwa kielelezo kwa wengi waliotamaushwa na mitazamo hasi.

## MASWALI

**a)** Fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa maneno 60. (utiririko 1**)** **(alama 5)**

**b)** Eleza namna ya kukabiliana na mitazamo hasi kwa maneno 80. (utiririko 1) **(alama 8)**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**(a)** Andika sauti zenye sifa zifuatazo: **(alama 1)**

**(i)** irabu ya juu, viringe

**(ii)** king'ong'o cha kaakaa gumu

**(b) (i)** Eleza maana ya sauti mwambatano. **(alama 1)**

**(ii)** Andika sauti mwambatano zinayotamkwa katika midomo. **(alama 1)**

**(c)** Andika neno lenye mofimu zifuatazo: kikanushi cha nafsi ya kwanza umoja, kikanushi cha wakati uliopita, yambwa, mzizi, kauli tendea, kauli tenda.

**(d)** Onyesha aina za nomino katika sentensi ifuatayo: **(alama 2)**

Uadilifu wa wanafunzi hao uliwapendeza wakurugenzi wa Shule ya Tumaini.

**(e)** Tumia kielezi cha idadi kamili badala ya kile kilichopigwa mstari. **(alama 1)**

Wazalendo huimba <u>mara kwa mara</u>.

**(f)** Andika katika wingi **(alama 2)**

Mwanafunzi huyu alinunua uzi ambao nitautumia kushona.

**(g)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama 3)**

Ijapokuwa Sikitu aliwahonga Wanatomoko, alishindwa katika uchaguzi uliofanyika juzi.

**(h)** Eleza matumizi ya viambishi vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo. **(alama 3)**

Huyu <u>ndi</u>ye mkimbia<u>ji</u> aliye<u>ku</u>sifu uwanja<u>ni</u>.

**(i)** Tumia kitenzi 'la' kama nomino katika sentensi. **(alama 1)**

**(j)** Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mstari. **(alama 3)**

Unga uliomwagika sakafuni umefagiliwa na Jerotich.

**(k) Tofautisha** maana: **(alama 2)**

**(i)** Ningepiga kura ningekuchagua.

**(ii)** Ningalipiga kura ningalikuchagua.

**(l)** Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya **futa** na **vuta**. **(alama 2)**

**(m)** Tunga sentensi mbili kubainisha maana mbili za neno: **koo** **(alama 2)**

**(n)** Andika katika msemo wa taarifa

"Nitaenda mahakamani kesho kukushtaki kwa kuniibia ng'ombe wangu," Yama alimwambia Birirei. **(alama 3)**

**(o)** Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya vitenzi katika jinsi iliyo mabanoni. **(alama 2)**

**(i)** toa (kutendesha)

**(ii)** cha (kutendeka)

**(p)** Huku ukitoa mifano mwafaka, eleza miundo ya majina katika ngeli ya Li-Ya. **(alama 2)**

**(q)** Kanusha **(alama 1)**

Kucheza kwake kulimkasirisha Kapaloti.

**(r)** Sahihisha sentensi ifuatayo **(alama 1)**

Furaha zao zilibainika walipokiona kiziwi akituzwa.

**(s)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo **(alama 2)**

Miguu yake ilimuuma alipokuwa akibeba mlango huo.

**(t)** Unganisha sentensi zifuatazo ili kuunda sentensi changamano **(alama 1)**

(i) Mwangeka alifiwa na mkewe.

(ii) Mwangeka alimuuoa Apondi.

**(u)** Andika sentensi ifuatayo kama ulivyoshauriwa. **(alama 1)**

Mwanafunzi ambaye hana kitabu hataweza kusoma.

Anza kwa: Kusoma…

**(v) Bainisha** silabi zinazowekwa shadda katika maneno yafuatayo **(alama 1)**

**(i)** angalia

**(ii)** mwananchi

**(w)** Bainisha kiima na yambwa katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Huyu mzee alimnunulia Karori zawadi nyingi.

## 4. ISIMU-JAMII (ALAMA 10)

**(a)** Fafanua jinsi kanuni zifuatazo zinavyoathiri matumizi ya lugha katika jamii. **(alama 4)**

**(i)** Hali

**(ii)** Uhusiano

**(iii)** Lugha azijuazo mtu

**(iv)** Jinsia

**(b)** Ukiwa shuleni ulipata nafasi ya kumsikiliza mtaalamu wa masuala ya vijana kuhusu maadili ya jamii.Ni mambo gani ambayo ungezingatia ili kuupata ujumbe wake barabara? **(alama 6)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 1

# KISWAHILI

Paper 3

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

## *Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

***a)*** *Andika jina lako, shule, nambari ya mtihani kisha utie sahihi katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
***b)*** *Jibu maswali manne pekee*
***c)*** *Swali la kwanza ni la lazima*
***d)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Ushairi*
***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | JUMLA | |

## 1. SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

***Soma utungo ufuatao kasha ujibu maswali yanayofuata.***

Nilipokukopoa,
Cheko la mwivu wangu lilipaa sana
Ukewenza ukamshawishi kuchukua buruji kueneza habari.
“Njooni mwone jana la ajabu.”
“Hajawahi kuonekana kama huyu
Tangu kuumbwa kwa ulimwengu.”
Ndivyo walisema walokubeza
Kijiji kizima kilimiminika mwangu nyumbani
Kuyatuma maozi kukutazama weye
Uso na thamani walikwona,
Wakaupa unyonge moyo wangu toto,
Wakanituma kuola viungo vyako
Wakanitanabahisha upungufu ulokulemaza!
Chozi chungu likapukitika
Likalovya change kidari
Likalovya chaoko kipaji
Tabasamu ukatoa kunihakikishia
“Mimi si mjalana!
Katu sivyo wasemavyo walimwengu!”
Neno lako hili likanipa tulivu
Nikaamua alakulihali kupambana na yangu jumuiya
Ilpsema kwa moja kauli utokomezwe, chakani utupwe.
Tazameni mahasidi mloteka
Teko la dharau mlonimwaiya
Mkanitia ukiwa usomithilika!
Oleni! Tungeni macho!
Mwana mlioambaa ukoma
<lomwinga ja nyuni wala mtama, tazameni
Mekuwa malaika, anowaauni
Kiguru mlomtajia hakimzuwii kufuma mishale!
Maadui wamwonapo hutetema kama jani
Mefagia vijiji vinane kwa pigo moja la kiganja chake
Mepigana vita visohisabika
Na Wetu mahasimu waliotupoka na mifugo.

Jamii yetu sasa metawala kote

Umekuwa nahodha mwenye kubwa saburi
Akili yako nyepesi sumaku kweli kweli
Hupakata yote ya neema na shwari
Mwili wako japo lemavu,
Mesheheni nguvu za majagina mia moja!
Naposhika zana, maadui elfu huanguka!
Umeifaa jamii hii, ilotaka kuangamiza
Majagina wote, wakusujudia
Walokufurusha wamebaki hizika
Watukuka ewe shibli
Mfano wa Shaka Zulu
Alowayeyusha kama barafu.

Limwengu mzima wakujua, mwana
Alozawa kishika mkuki
Ulosema na miungu, alfajiri lipoukumbatia ulimwengu
Wla mwana jihadhari usaliti wao waja
Wasije kutosa lindini kwa nduli kukukabidhi.

**MASWALI**

**a)** Ainisha utungo huu kimuundo na kimaudhui. **(ala. 2)**
**b)** Eleza sifa tatu za mighani ambazo zinajitokeza katika utungo huu**.** **(ala.6)**
**c)** Jadili fani katika wimbo huu. **(ala.5)**
**d)** Jadili sifa za jamii iliyoizaa kazi hii. **(ala. 2)**
**e)** Ni nani anayimba wimbo huu (nafsineni)? **(ala.1)**
**f)** Eleza **tofauti 4** kati ya mighani na visasili **(ala.4)**

## SEHEMU YA B: CHOZI LA HERI

***Jibu swali la 2 au 3.***

**2.** Fafanua jinsi riwaya ya chozi la Heri ililenga kuiadilisha **jamii.** **(ala. 20)**

**3.** Usalama ni mojawapo ya mahitaji ya kibinadamu, kwa hakika, tunaweza kusema kuwa usalama ni mojawapo ya mahitaji ya kimsingi. Bila usalama binadamu hawezi hata kushiriki shughuli……”

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili **(ala.4)**
**b)** Eleza umuhimu wa mzungumzaji katika kujenga plot**i** **(ala.8)**
**c)** Mzungumzaji anazungumzia swala la usalama. Jadili matokeo ya ukosefu wa usalama ukirejelea matukio katika riwaya ya Chozi la Heri. **(ala.8)**

## SEHEMU C: TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA

**Jibu swali la 4 au 5**

**4.** ***Teknolojia na maendeleo ni baadhi ya mabadaliko ya lazima katika jamii ya Afrika.*** Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya ***Bembea ya Maisha.*** **(alama20)**

**5.** Elimu ni mafundisho muhimu yanayotolewa katika jamii. Jadili kwa kurejelea tamthilia ya ***Bembea ya maisha.*** **(alama20)**

## SEHEMU YA D: HADITHI FUPI, MAPAMBAZUKO YA MACHWEO

**Jibu swali la 6 au 7**

**6.** ***...iwapo penzi hili litatia doa, basi nirudishie mfuko huu kama ishara ya kulitupa penzi langu kama jongoo na mti wake..."***

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

**b)** Fafanua mbinu mbili ambazo zimetumika katika dondoo hili. **(alama 4)**

**c)** Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. **(alama 6)**

**d)** Eleza umuhimu wa msemewa wa hadithi hii katika kujenga ploti. **(alama 6)**

**7.** Kwa kurejelea hadithi zifuatazo, jadili maudhui ya **nafasi ya vijana** katika jamii. **(alama 20)**

**i.** Toba ya kalia
**ii.** Ahadi ni deni iii.
**iii.** Nilitamani
**iv.** Pupa

## SEHEMU YA E: USHAIRI

**8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yaliyofuata.**

**1.** Jambo lolote ni nia, kuweka yako azima,
Hasa ukikusudia, kulepuka la lawama,
Mola takusaidia, kila la ovu kuzama,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**2.** Hakika si masikhara, wa kale waliyosema,
Ni maneno ya busara, tena ni wasia mwema,
Kuwa hasira hasara, ghadhabu zisizokoma,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**3.** Mja katu haitaki, hasira kuziandama,
Punguza zako hamaki, moyo uwe na huruma,

Kwani zikizidi chuki, hapo huja uhasama,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**4.** Na uhasama ujapo, uadui kukwegema,
Hapo ndipo upatapo, kukufikia zahama,
Mwisho ndipo ujutapo, ikabaki kulalama,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**5.** La usawa sinyamai, kukweleza ni lazima
Chuki nyingi hazifai, hebu tuliza mtima,
Waweza tupa uhai, au nyingi darahima,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**6.** Upunguze wako mori, mwana na mtu mzima,
Upoze moyo wa hari, hasira zipate hama,
Subira huvuta heri, ikaleta na neema,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**7.** Kifaya nilipofika, hapa ndiyo kaditama,
Sahibu wasia shika, hasira si kitu chema,
Mtegemee Rabuka, atakulinda Karima,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**MASWALI**

**a)** Toa anwani mwafaka kwa shairi hili. **(Al. 1)**
**b)** Ainisha shairi hili kwa kuzingatia:- **(Al. 4)**
**i)** Mishororo
**ii)** Vipande
**c)** Fafanua umbo la shairi hili. **(Al. 4)**
**d)** Dhihirisha matumizi ya idhini ya mshairi katika shairi hili. **(Al. 3)**
**e)** Andika ubeti wa sita kwa lugha tutumbi. **(Al. 3)**
**f)** Eleza toni ya shairi hili. **(Al. 2)**
**g)** Ni nani nafsineni katika shairi hili? Eleza **(Al. 1)**
**h)** Fafanua msamiati ufuatao kama ulivyotumika shairini. **(Al. 2)**
**i)** Mtima
**ii)** Darahima

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 2

# KISWAHILI

Paper 1

**Time: 1¾ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

**a)** *Andika jina lako na nambari ya usajili kwenye nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
**b)** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
**c)** *Andika insha* ***mbili****. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima.***
**d)** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
**e)** *Kila insha isipungue maneno* ***400****.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. | 20 | |
| 2. | 20 | |
| 3. | 20 | |
| 4. | 20 | |
| JUMLA | 40 | |

## MASWALI

**1.** Suala la Afya ya akili ni suala nyeti na telezi na ambalo halijapewa umakini ufaao na wanajamii kutokana na unyanyapaa unaohusishwa nalo. Ukiwa Mhariri Mkuu wa Gazeti la Mzalendo, andika tahariri kuangazia vyanzo vya changamoto hii na kupendekeza suluhu mwafaka.

**2.** "Vijana ndio nguzo kuu katika kuimarisha mshikamano wa kitaifa". Thibitisha.

**3.** Tunga kisa kitakachodhihirisha matumizi ya methali ifuatayo:

*Jifya moja haliinjiki chungu*

**4.** Tunga kisa kitakachokamilika kwa maneno yafuatayo:

*Kweli nimetambua kuwa, familia ni nguzo muhimu katika ujenzi wa jamii*.

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 2

# KISWAHILI

Paper 2

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

*a) Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

*b) Jibu maswali yote.*

*c) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*

*d) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

**1: UFAHAMU: (Alama 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

"Asante baba, asante mama," akasema Bahati jioni moja baada ya chajio, "Sijui ilitokeaje kukawa na watu wanaothamini binadamu wenye mahitaji maalumu katika jamii hii. Sitawauliza mlichofanya kunikinga na hukumu ya ukoo ya kuniangamiza; hayo mtakuja kunihadithia siku moja. Ila nataka mjue kwamba kuishi na ulemavu wa aina yoyote ile kuna dhiki kuu. Niliyokabiliana nayo baada ya uamuzi wenu wa kunipeleka shuleni hayawezi kutoshea hata chapisho la kurasa elfu.Si kudhihakiwa na miale ya jua; ngozi yangu inashindwa kuuhimili ukali wake, si kutengwa na marika, si kulazimika kusoma hati za kawaida hadi pale serikali ilipoanzisha sera ya kuhakikisha kwamba matini zote za kiusomi zimeandikwa pia kwa hati ambazo zinaweza kusomwa na wenye changamoto kama yangu, si kubaguliwa kazini...."Bahati alitua, akawatazama wazazi wake kama anayetaka kuona taathira ya maneno yake kisha akaendalea.

"Msinione kama aliyekosa hisani, ila' nataka niwaambie kwamba hata uamuzi wenu wa kunitafutia mlinzi kuandamana nami hadi shuleni ulinitia kwenye ngome zaidi.Nilijihisi kama niliyedhulumiwa zaidi katika kule kulindwa! Najua mlikuwa mnachelea kwamba ningekuwa windo rahisi kwa walanguzi wa binadamu ambao wanaamini kwamba viungo vyetu sisi ni dawa ya kutibia ndwele mbalimbali.Hata hivyo, katika kipindi chote hicho nilitamani kwamba mngenifunza mbinu za kujilinda mimi binafsi. Amini usiamini hata nilitamani kwamba ningetekwa nyara, nijadiliane na watesi wangu kuliko kupokwa nafasi ya kubuni mikakati ya kujihakikishia usalama".

"Mwanangu Bahati," alisema mume wangu, "binadamu hawi jagina kwa kuzifuata tamaduni za jamii yake bila kuzichunguza. :haidhuru kwamba ilichukua muda kuyangamua haya'. La muhimu ni kwamba umeweza kuishi kama ndugu zako".

Nilimtazama mume wangu kwa macho yaliyokuwa yamepofushwa na dimbwi la machozi. Moyo uliituma akili yangu kurudi nyuma kule -e-e-e- kwenye miereka ya baada ya kuzaliwa kwa Bahati. Asubuhi hiyo ya kipupwe nilishika ujia ulioelekea kwenye msitu uliokuwa karibu na boma la Mzee Kedi, baba mkwe wangu; mgongoni nimeifungia mbeleko ambayo ilikisitiri kitoto changu. Nilitazama nyuma, nikaiona nyumba ambayo mimi na mume wangu tulikuwa tumechanga bia kuijenga.

"Haya yote nayaacha," nilijiambia, "nayaacha na mengine mengi. Nawaacha mabinti wangu wawili, namwacha mume wangu, naiacha kazi yangu, nayaacha maisha yangu wala sijuti kwa kuyaacha haya yote. Sina cha kujutia kwani imebidi kuondoka. Jamii yangu imenitema; mimi na mwanangu.Haina nafasi ya mwanangu, kwa hivyo nami nimeamua kwamba haina nafasi yangu kwa vile imesema huu ni mzigo wangu. Ikiwa ukoo umeamua kuwa hatima ya mwanangu huyu ni kuwa kitoweo cha fisi, basi na tuwe sote karamu ya fisi" nilitamatisha kauli yangu kisha nikayarudisha nyuma tena mawazo yangu.

Nilikumbuka sauti ya muuguzi hospitalini siku ambayo nilijikopoa, "Pongezi Tamasha, Mungu amekutunukia kipusa". Nilikifunua kitoto changu kilichokuwa kimefunikwa gubigubi,

nikakitazama viguu, vikono, uso...kisha, 'Mungu wangu!' ikanitoka. "Dadangu, unastahili kumshukuru Mungu," akasema muuguzi, "wapo wanawake, mimi mwenyewe nikiwemo, ambao hawajawahi kuambulia ujauzito, sikwambii hata kupoteza mimba.Huyu wako ni kiumbe kamili, kasoro yake i kwenye ngozi tu, na hii ni hali ambayo unaweza kukabiliana nayo. Hapa unionapo nimelazimika kumpa mume wangu talaka, mwenyewe alienda kortini akaiomba. Anadai kwamba hatusikilizani. Ila najua kiini cha haya yote ni kutoshika kizazi".

Nilimtazama huyo muuguzi kana kwamba hajasema lolote. Nilimwona kama anayeuona mzigo wangu kuwa kanda la usufi. Huenda huyu muuguzi hakujua kwamba katika jamii yangu watoto wa aina hii ni kama pacha, huaminiwa kuwa nuksi kwa ukoo mzima, kwa hivyo hutupwa. Muuguzi huyu hakujua pia kwamba tayari nilikuwa na watoto wawili wa kike na huo tayari ulikuwa mzigo mkubwa kwangu kwani ilibidi kumhakikishia mavyaa kila mara kwamba hawa pia walikuwa watoto.

Moyo ulinipa kukumbuka jitimai iliyojiandika usoni mwa mume wangu asubuhi hiyo alipokuja hospitalini. Alikitazama kitoto chetu kana kwamba anaona mzuka. Alinyamaza kwa muda, akashusha pumzi, kisha akanishika kwenye bega na kuondoka kwenye wodi. Machozi yalivunja kingo zake huko yanakohifadhiwa, nikalia kama mfiwa, Mume wangu alirudi tena baada ya siku mbili; anakuja kunipeleka nyumbani.

"Mke wangu, naomba msamaha kwa kutokuja kuwatazama kwa siku mbili. Ilibidi nishauriane na ukoo kuhusu tanzia hii. Inavyoonekana ni kwamba msimamo wa baba na wazee wengine ni ule ule. Wanasema ukoo wa Baulanga haujawahi kupata mtoto wa aina hii, kwamba kumhifadhi mwana huyu kutakuwa kuupaka masizi ukoo. Wahenga hawatakubali tendo hili. Sijui nitakutetea vipi.Nimo kwenye njia panda," mume wangu alikamilisha uzungumzi wake na kuelekea kwenye afisi ya mhasibu kukamilisha viviga vya kutuondoa hospitalini.

"Huna haja ya kuniitetea. Sijafanya kosa lolote. Nililofanya ni kujaliwa kiumbe ambaye anaonekana kuwa punguani kwa misingi ya jamii yako. Nitakilinda kitoto hiki hata kifoni," nilimwambia mume wangu mawazoni.

## MASWALI

**(a)** "Kufanikiwa kwa watu wenye mahitaji maalumu kunategemea jamii." Thibitisha kwa kutoa hoja sita kutoka aya tatu za kwanza. **(alama 6)**

**(b)** Kwa kurejelea aya ya nne hadi ya saba, onyesha jinsi unyanyasaji wa kijinsia unavyoendelezwa katika jamii hii. **(alama 3)**

**(c)** "Msimulizi anahimiza. uwajibikaji." Thibitisha kwa kutoa hoja nne kutoka aya tatu za ' mwisho. **(alama 4)**

**(ii)** Eleza maana ya, 'kuupaka masizi' kulingana na taarifa. **(alama 1)**

**2 UFUPISHO (Alama 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Wakenya walipoipata katiba mpya waliidhinisha mfumo wa ugatuzi. Katika mfumo huu, mamlaka ya serikali kuu katika uongozi, usimamizi na utumiaji wa rasilimali za nchi hupunguzwa. Kiasi Fulani cha mamlaka hutwaliwa na maeneo ya ugatuzi. Suala hili halikuzingatiwa katika katiba ya awali ambapo mamlaka yote yalikuwa mikononi mwa serikali kuu. Kutokana na upana na wingi wa maeneo, iliiwia vigumu serikali kuu kuhakikisha kwamba kulikuwa na usawa wa kimaendeleo katika sehemu nchini.

Kwa mujibu wa katiba mpya, serikali kuu haina budi kuyasaidia maeneo yote ya ugatuzi ili yaweze kujinyanyua kiuchumi na kuboresha hali za maisha za wakazi wake. Vilevile ni jukumu la kila eneo la ugatuzi kuweka mikakati madhubuti ili kuchunguza na kubainisha rasirimali zote katika maeneo husika. Hili litasaidia kufumba rasilimali ambazo zinaweza kuchangia katika ustawishaji wa maeneo haya. Maeneo haya pia yanatakiwa kutafuta mbinu zitakazofanikisha uzalishaji na utumiaji wa rasilimali hizi kwa njia endelevu. Mojawapo ya mbinu hizi ni uongezaji thamani katika rasilimali yoyote inayozalisha kwenye eneo mahususi.

Maeneo mengi ya ugatuzi nchini humu yanategemea kilimo cha ufugaji kama mhimili wa uchumi. Licha ya kuwa nguzo, kilimo hiki hakijawahi kupigiwa darubini vizuri kwa lengo la kukiimarisha ili kiwanufaishe wenyeji kikamilifu. Aghalabu wafugaji wengi huandama mbinu za jadi za ufugaji ambazo haziwahakikishii ongezeko la mapato.Isitoshe, wafugaji hawa wanakabiliwa na tatizo katika soko la mifugo ambapo wengi hupunjwa na matapeli. Pamoja na haya, baadhi ya wakazi huuza mifugo nje ya nchi wakiwa wazimawazima bila kuwazia matokeo ya kitendo hiki. Si ajabu kuwaona ng'ombe, ngamia, mbuzi na kondoo wakipakiwa kwenye malori na kusafirishwa nje ya nchi. Ukweli ni kwamba jambo hili ni hatari sana, si kwa uchumi wa maeneo husika tu, bali pia kwa Kenya kwa jumla. Hii ni kwa kuwa walionunua mifugo wazimawazima wanaweza kuhiari kutowachinja na badala yake kuwatumia kama mbegu kwani baada ya muda huenda wanaonunua mifugo wakijitosheleza na kukosa kununua mifugo wengine. Hali ikiwa hivyo, maeneo yaliyotegemea soko hili huenda yakalipoteza taratibu, na bila shaka kupoteza natija inayotokana na soko lenyewe.

Ili kudhibitisha hali hii, itakuwa bora ikiwa viwanda vya kuchinjia mifugo na kupakia nyama vitajengwa katika maeneo haya ya ugatuzi. Hili litawawezesha wakazi kuuza nyama badala ya kuuza mifugo wazimawazima. Fauka ya hayo maeneo haya yatajikinga dhidi ya kupoteza bidhaa zinazotokana na mifugo. Hizi ni kama vile ngozi, kwato na pembe ambazo bila shaka zina natija kuu. Ngozi kwa mfano, ni bidhaa muhimu sana katikasekta ya utengenezaji wa mavazi na mifuko. Viwanda vinavyotumia ngozi kama malighafi vikijengwa katika maeneo haya, wakazi wake watanufaika si haba. Madhalani, viwanda vya kutengenezea viatu, mishipi, mifuko na nguo vikianzishwa,wawekezaji watalazimika kuanzisha viwanda vingine tegemezi. Kathalika, ni dhahiri kwamba bidhaa zinazotokana na ngozi huhitaji kutiwa nakshi. Kuanzishwa kwa viwanda hivi basi kutazua haja ya kuanzishwa kwa viwanda vingine vya kutengeneza rangi, pamoja na maduka ya kuuza bidhaa zenyewe. Isitoshe, gundi ya kugandisha bidhaa hizi itahitajika, hivyo kusababisha

haja ya kuanzishwa kwa kiwanda cha gundi. Matokeo ya shughuli hizi zote ni kuzalishwa kwa nafasi anuwaiza kazi kwa wakazi. Hili litakuwa na matokeo zaidi chanya, hususan kwa vijana. Badala ya kushiriki ulevi na burudani zinazowahatarisha, wataweza kujitafutia riziki katika viwanda hivi.

Juu ya hayo, mfumo wa ugatuzi utayaweza maeneo husika kuongeza thamani, utoaji wa huduma za kijamii na kuitawala kulingana na mahitaji ya maeneo haya. Ni muhimu hata hivyo kuzingatia kwamba kila eneo la ugatuzi lina upekee wake, navyo vipaumbele hutofautianakulingana na maeneo. Kuna yale ambayo yatasisitiza usalama, mengine ujezi na uimirishaji wa miundomusingi kama vile barabara, vituo vya afya na hata taasisi za elimu. La muhimu ni wakazi wa maeneo husika kubainisha ni lipi litatekelezwa kwanza.

Kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Kufanikiwa kwa mfumo wa ugatuzi kutategemea juhudi za kila mkazi wa eneo husika. Ni muhimu kila mkazi kujiona kuwa mmiliki wa eneo zima la ugatuzi na kuwajibika katika kuliendeleza kwa hali na mali.uwajibikaji huu unajumuisha uteuzi wa viongozi wenye muono mzuri na ambao utawawezesha kuyafikia malengo yao ya kimaendeleo. Hakika, mustakabali na uwepo wa eneo la ugatuzi utakuwa zao la maamuzi ya wanaeneo. Vilevile ufanisi wa maeneo ya ugatuzi utakuwa msingi wa ufanisi wa taifa kwa jumla.

**a)** Fupisha ujumbe wa aya tatu za mwanzo kwa maneno 85-90 (alama 8, 1 mtiririko)

**Matayarisho:**

**Nakala safi:**

**b)** Kwa kutumia maneno 75-80, bainisha masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya tatu za mwisho. (alama7, 1 mtiririko)

**Matayarisho:**

**Nakala safi:**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

**(a)** Andika neno lenye sauti zifuatazo: **(alama 1)**

Kipasuo hafifu cha midomo, irabu ya mbele wastani, kikwamizo sighuna cha ufizi, irabu ya kati chini. _____

**(b)** Tunga sentensi moja moja yenye aina zifuatazo za vishazi**:** **(alama 2)**

(i) Cha nia

(ii) Kitegemezi cha wakati

**(c)** Andika maana ya maneno yaliyopigiwa mstari**.** **(alama 2)**

Wali<u>sita</u> kufanya kazi hiyo baada ya saa <u>sita</u> usiku.

**(d)** Tia shadda: **(alama 2)**

i. pekee

ii. alinyongwa

**(e)**Huku ukitoa mfano, onyesha miundo mitatu ya maneno katika ngeli ya U-I **(alama 3)**

**f)** Tunga sentensi yenye vijisehemu vifuatavyo vya sarufi**:** **(alama 2)**

Kiambishi kiwakilishi cha kiima

Kiambishi kiwakilishi cha wakati

Yambwa

Mzizi - dhiki

Kauli ya kutendesha

Kiishio

**(g)** Tumia neno dhahiri kama**:** **(alama 3)**

**i.** Kitenzi_____

**ii.** Kivumishi_____

**iii.** Kielezi_____

**(h)** Huku ukitoa mifano, eleza miundo mitatu ya silabi za Kiswahili. **(alama 3)**

**(i)** Tofautisha mzizi na shina kwa mifano**.** **(alama 2)**

**(j)** Nyambua ziba katika kauli ya kutenduka kisha utungie sentensi. **(alama 2)**

**(k)** Bainisha hali zinazorejelewa katika sentensi hizi**.** **(alama 3)**

(i) Mwangeka hufika kituoni mapema._____

(ii) Mgonjwa angetibiwa angepona._____

(ii) Umekuwa nanasi, kutagia mibani? _____

**(l)** Andika katika udogo wingi**.** **(alama 2)**

Ugwe ulipitishwa juu ya ukuta uliomea uyoga na kufungiwa kwenye makuti.

**(m)** Onyesha kiarifu katika sentensi hii. **(alama 1)**

Kilimia kimechomoka angani.

**(n).** Changanua kwa kielelezo cha mstari**.** **(alama 3)**

Ndege aliruka angani ghafla.

**(o)** Ainisha Virai vinne katika sentensi ifuatayo**.** **(alama 2)**

Kicha cha funguo kilikuwa kimepotea jana nikicheza kandanda.

**(p)** Tunga sentensi kuonyesha matumizi mawili ya nukta mkato**.** **(alama 2)**

**(q)** Andika methali yenye maana sawa na jivu usilolilala usilipigie Jibwa**.** **(alama 1)**

**(r)** Andika upya sentensi ifuatayo ukianza kwa shamirisho kitondo. **(alama 2)**

Kaizari amewakatia ng'ombe majani kwa muundu.

**(s)** Damka ni kwa rauka, wakati ni kwa_____oa ni kwa taliki uza ni kwa_____

**4. (ISIMUJAMII)** **(alama 10)**

**a)** Katika jamii huwa wakati mwingine kuna matumizi ya lugha isiyo ya kistaarabu. Taja mifano mitano ya lugha sampuli hiyo **(alama 5)**

**b)** Taja mambo matano yanayoathiri jinsi tunavyoweza kutumia lugha katika jamii. **(alama 5)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 2

# KISWAHILI

Paper 3

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

***a)*** *Andika jina lako, shule, nambari ya mtihani kisha utie sahihi katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
***b)*** *Jibu maswali manne pekee*
***c)*** *Swali la kwanza ni la lazima*
***d)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Ushairi*
***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | JUMLA | |

## SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

**Swali Ia Iazima**

**1. (a)** Tofautisha kati ya mighani na maghani. **(alama 2)**

(b) Taja na ueleze ama tatu ya maghani ya kawaida. **(alama 6)**

(c) Eleza sifa za maghani. **(alama 4)**

(d). Kwa kurejelea mifano mwafaka eleza majukumu manane ya nyimbo katika jamii, **(alama 8)**

## SEHEMU B: USHAIRI

***Jibu swali la 2 au la 3***

**2.** ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***.

Ewe hisia!
Umeniamshia ndoto niloisahau zamani
nyimbo ya kale
na mdundo usonivutia
ila hayawani na mwangu rohoni.

Tulia sasa tulia
Hebu tulia ewe hisia ulo mtimani
Nataka katu kusisimka
kwa sauti yako laini
Kwani njia zetu ni
daima hazioani

Umesubutu vipi kuniita
kutoka mwako ngomeni
ulimosahauliwa tangu zamani
Basi yawache maombolezi yako yaso maoni,
yawateke hao mashujaa wa kale
wafu walo kaburini.

Hebu tulia, usiniingilie
Usinihangaishe!
Kukuandama katu haimkini
Kwani hata sasa…kwa kukuwaza tu dakika hini
naona majuto ya mbali moyoni
kama kwamba nimegawa wangu wakati
na wazimu, majinuni.
Basi nenda zako hisia…shuu…hebu tokomea.

## MASWALI

(a) Huu ni utungo wa aina gani? **(alama 2)**

(b) Huku ukitoa mifano, fafanua sifa zinazoufanya utungo huu kuwa **shairi** **(alama 5)**

(c) Mistari mishata ni nini? Toa mifano kwenye shairi hili. **(alama 4)**

(d) Fafanua tamathali za kifasihi katika shairi hili. **(alama 3)**

(e) Eleza mbinu **tatu** alizotumia mtunzi kutosheleza kaida za kishairi. **(alama 6)**

**3.** ***Soma shairi lifwatalo kisha uyajibu maswali yanayoliandama:***

Naandika yangu haya, kwa uwezo wa Wadudi,
Kanipa njema afiya, kumsifu sina budi,
Nifundishie insiya, hino methali ya jadi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo

Ago mchama huuya, mbele mambo yakizidi,
Hurudi pakawa kaya, kupapenda hana budi,
Kwingi angawayawaya, ago shuruti arudi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Kule kwetu Mwarakaya, kijiji chetu cha jadi,
Yalidhihirika haya, bwana mmmoja mkaidi,
Aloalikwa ulaya, kadhani ‘mepata sudi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo,

Alidhani hatauya, ‘endapo nchi ***baidi***,
Na kusema bila haya, kwa inda na ukaidi,
Kwamba akenda ulaya, harudi kwenya samadi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Aliranda akitaya, kwa mbwembwe na zake tadi,
Nguo moto kazitiya, nyumbaye akainadi,
Kasema vyote ‘ishiya; kurudi sina ahadi
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Matusi aliyamwaya, mengi yasiyo idadi,
Mkewe kamwita yaya, na kudharau abidi,
Kanena ***‘mekata waya’***, ng’ambo nenda kufaidi,
Mchama ago hayeli, huenda akauya papo,

Ng’ambo alielekeya, kwa vishindo kama radi,
Kumbe aliyemwendeya, kabambwa kwa ufisadi,
Vya watu amebugiya, rushwa na kuhepa kodi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Kombo yakamwendeya, mambo mno yakazidi,
Akabakia kuliya, nyumbani ataka rudi,
Nyumba ipi ‘taingiya’, hana tena tabaradi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo

## MASWALI

**a)** Kwa kutolea ushahidi ufaao shairini, jadili kifupi maswala **matatu** makuu ambayo mtunzi ameyashughulikia**.** **(alama 6)**

**b)** “Mtunzi huyu ni bingwa wa kutumia lugha kupitisha ujumbe.” Tetea. **(alama 4)**

**c)** Fasiri ujumbe wa mtunzi katika ubeti wa **sita.** **(alama 4)**

**d)** Nafsi nenewa katika shairi hili ni nani? Thibitisha. **(alama 2)**

**e)** Zaidi ya tarbia, ungelipangaje tena shairi hili**?** **(alama 2)**

**f)** Fafanua msamiati ufwatao kama ulivyotumika shairini: **(alama 2)**

i. Baidi

ii. 'mekata waya'

## SEHEMU C: TAMTHILIA*: BEMBEA YA MAISHA (Timothy Arege* )

**Jibu swali la 4 au 5**

4."Basi usijipandishe presha bure mama!"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

(b) Ainisha mbinu mbili za kimtindo zilizotumiwakatika dondoo hili**.** **(alama2)**

(c)Eleza sifa za msemewa. **(alama 4)**

(d) Jadili maudhui ya utamaduni kama yanavyojitokeza katika tamthilia nzima. **(alama10)**

5. Katika tamthilia hii Maisha yamesawiriwa kama Bembea. Kwa kutolea mifano mwafaka oanisha kauli hii na wahusika mbalimbali. **(alama 20)**

## SEHEMU D: HADITHI FUPI : MAPAMBAZUKO YA MACHWEO (*D.W Lutomia na Phibbia Muthama)*

**Jibu swali la 6 au 7**

6...iwapo penzi hili litatia doa,basi nirudishie mfuko huu kama ishara ya kulitupa penzi langu kama jongoo na mti wake..."

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b)Fafanua mbinu mbili ambazo zimetumika katika dondoo hili. **(alama 4)**

c)Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. **(alama 6)**

d)Eleza umuhimu wa msemewa wa hadithi hii katika kujenga ploti**.** **(alama 6)**

7. Swala la elimu limepewa kipaumbele katika hadithi ya Sabina. Jadili **(alama 20)**

## SEHEMU E: RIWAYA CHOZI LA HERI : Assumpta Matei

**Jibu swali la 8 au 9**

8.Eleza jinsi **maudhui ya ufisadi** yalivyoshughulikiwa katika riwaya ya Chozi la Heri. **(alama 20)**

*9.*"…liandikwalo ndilo liwalo? Since when has man ever changed his destiny?"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(b) Bainisha mbinu tatu za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. **(alama 6)**

(c) Kwa kuzingatia hoja **kumi**, jadili jinsi ambavyo hali ya, **" liandikwalo ndilo liwalo"**, inavyojitokeza katika Chozi la Heri. **(alama 10)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 3

# KISWAHILI

Paper 1

**Time: 1¾ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

## *Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

**a)** *Andika jina lako na nambari ya usajili kwenye nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

**b)** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

**c)** *Andika insha* ***mbili****. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima.***

**d)** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*

**e)** *Kila insha isipungue maneno* ***400****.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. | 20 | |
| 2. | 20 | |
| 3. | 20 | |
| 4. | 20 | |
| JUMLA | 40 | |

## MASWALI

**1.** Kumekuwa na visa vingi vya mauaji hapa nchini, mhariri wa gazeti la Taifa Leo amewatangazia wasomaji katika toleo la Jumatatu kutuma makala yao ili kuchangia katika kuandika tahariri itakayohusu chanzo cha mauaji hayo na suluhisho. Andika makala hayo.

**2.** Pesa za hazina ya ustawi wa maeneo bunge zapaswa kuondolewa chini ya usimamizi wa wabunge.Jadili

**3.** Mkono usioweza kuukata, ubusu

**4.** Andika insha itakayoisha kwa:

**……..**Nilishusha pumzi, nikashukuru Mola nilipojipata hoi bin taabani miongoni mwa wafu.

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 3

# KISWAHILI

Paper 2

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

*a) Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

*b) Jibu maswali yote.*

*c) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*

*d) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. UFAHAMU | 15 | |
| 2. UFUPISHO | 15 | |
| 3. SARUFI | 40 | |
| 4. ISIMU JAMII | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

## 1.UFAHAMU (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Miaka mingi ya kutaliwa na wakoloni iliwafanya wananchi wengi kupuuza umaarufu na uadilifu wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa kwa manufaa ya kuarifiana habari mbalimbali kwa ufasaha na kuelewana vyema.

Wakoloni pia waliwashawishi wananchi waone, kwamba lugha ya Kiswahili ni kwa ajili ya watu wale wasiokuwa na elimu na kwa wale ambao hawajastaarabika. Kwa wale wenye 'elimu ya wastaarabu,' wakoloni waliwashawishi kuamini kwamba lugha ya kigeni, yaani Kiingereza, ndiyo hasa lugha inayofaa kwa kujieleza na kufahamishana habari.

Kutokana na vikwazo hivi si ajabu kuona hadi hivi sasa, mwananchi halisi akijitwaza kwamba hawezi kujieleza kwa ufasaha au kumpasha mwenzie habari kwa ukamilifu mpaka atumie lugha ya Kiingereza. Hata katika maofisi mengi ya serikali, hadi hii leo, japo imeshapitishwa kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya taifa bado utawaona wananchi wengine wanapendelea kuzungumza Kiingereza wao kwa wao, ili wajulikane kwamba wana kisomo na wamestaarabika.

Vikwazo vya namna hii vimewalemea wananchi vile vile kwa upande wa magazeti. Utaona mwananchi ambaye anafahamu Kiingereza kidogo sana, akijinunulia gazeti kubwa la Kiingereza na kuanza kuzurura nalo kutwa nzima bila kuambulia mengi ndani yake. Pia utawasikia wananchi wengi wakijidai kwamba hawataki kusoma magazeti ya Kiswahili kwa sababu inakuwa vigumu kwao kuelewa mambo yaliyomo kama vile ambavyo wangelielewa katika gazeti la Kiingereza.

Mabeberu wameshagundua kwamba tunao upotovu wa aina hiyo, ndipo utaona mara nyingi wanawaletea wananchi magazeti mengi ya Kiingereza, mengine yakiwa na nia ya kuwapotosha wakijua kwamba watayasoma tu, mradi yameandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

Mara nyingi taifa fulani la kibeberu likitaka tuchukiane na taifa jingine ambalo ni adui yake kisiasa au kiuchumi, taifa hilo la kibeberu linaandika habari za uchochezi kwenye magazeti yao kwa lugha ya Kiingereza, mambo kuhusu taifa lile adui yake (ambalo si adui yetu).

Magazeti hayo huandikwa kwa lugha nadhifu ya Kiingereza na kuletewa wananchi hapa nchini. Maskini wananchi wengine waliotopea kwa kudhani Kiingereza ndicho lugha nzuri ya Kigazeti , wanayanunua mara moja na kuanza kuyasoma magazeti hayo, na pia kuwapa watoto wao wayasome. Matokeo yake ni kwamba, bila kujitambua, wanajikuta wanayafanya yale mabeberu waliyotarajia wayafanye, yaani wanaanza kuchukiana bure na taifa lile ambalo ni adui wa mabeberu hao, lakini si adui zetu. Madhumuni ya kuandika habari kwenye magazeti, ni kutaka kuwafahamisha wasomaji mambo yaliyotokea au yatakayotokea siku hata siku, kwa lugha inayofahamika na kueleweka kwa urahisi bila kumtatiza msomaji. Ikiwa basi ndiyo madhumuni, kuna haja gani kutumia lugha ya kigeni ili kuwaelezea wasomaji wako jambo wangaliweza kuelezwa kwa lugha yao wenyewe ambayo wanaielewa vyema.

Mtu aelezeapo jambo kwa maandishi akitumia lugha yake mwenyewe anaielewa vyema na ambayo pia wasomaji wake wataielewa kwa ukamilifu. Kwa ujumla jambo ambalo mwandishi huyo ataliandika kwa lugha ambayo ni ya asili yake ambayo anaielewa vyema, halitamtatiza msomaji wake ambaye pia anaielewa vyema lugha hiyo.

## MASWALI

**a)** Eleza mbinu zinazotumiwa na wakoloni kuwafanya wananchi kuidunisha lugha ya Kiswahili **(al 3)**

**b)** Thibitisha kuwepo kwa ukoloni mamboleo katika habari uliyosoma **(al 4)**

**c)** Eleza jinsi wabeberu wanaweza kuzua vurugu katika mataifa mbalimbali **(al 2)**

**4.** Taja sababu ambayo imewafanya wananchi wengi kupuuza lugha ya Kiswahili **(al 1)**

**5.** Wakoloni wana mtazamo gani kuhusu lugha ya Kiswahili? **(al 2)**

**6.** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa **(al 3)**

**a)**Uadilifu……

**b)**Akijitwaza……

**c)**Waliotopea**…….**

**2. UFUPISHO:** ( Alama 15 )

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Mtazamo hasi ni kukata tamaa, kuhusu hali, mtu au jambo fulani. Ni hisia ya kutotaka kushiriki wala kuhusishwa na jambo au hali fulani. Mtazamo huu ndio huwafanya wanafunzi wengi kuchukia au hata kudunisha baadhi ya masomo na walimu wanaoyafundisha. Licha ya wengi kuwa na mtazamo huu, kwa kweli huwa hawatambui. Asilimia kubwa ya wanaotambua hutatizika kujikwamua kutoka katika hali hii.

Inakadiriwa kwamba mtu wa wastani huwa na takribani mawazo elfu sitini ya kibinafsi kwa kila saa 24. Asilimia 95 ya fikra hizi huwa sawa na za siku iliyotangulia na asilimia 80 ya fikra hizi zilizorudiwa huwa hasi. Isitoshe, fikra hizi nyingi hutokea bila mtu mwenyewe kutambua na huwa mazoea. Hii ina maana kwamba watu wengi hawana ufahamu wa athari za fikra hizi maishani mwao. Kuna vyanzo kadha wa kadha vya mitazamo hii. Mwanzo kabisa ni imani potovu. Hiki ndicho chanzo kikuu cha mtazamo hasi. Kushikilia imani potovu kuhusu maisha pamoja na matukio fulani maishani hujenga mtazamo hasi. Unayaona maisha kwa macho ya imani zako na iwapo imani hizo ni potovu, basi hutayathamini maisha yako. Ili kukabiliana na hali hii, sharti kwanza ubadili imani yako.

Uamini kwamba mabadiliko yanaweza kutokea na uchukue hatua ya kuanzisha mabadiliko hayo maishani mwako. Unahitaji kuepuka fikra hasi zinazoambatana na maisha yako ya awali na kulitathmini kila tukio maishani kama tukio huru, lisilo na uhusiano na yaliyowahi kukutamausha.

Kujikwamua kutoka katika imani duni unahitaji kuibuka na idadi kubwa ya imani chanya kuliko hasi kuhusu hali mahsusi. Baada ya hilo, zikabili imani zako potovu moja baada ya nyingine huku ukijiuliza endapo imani hizo ni kweli na endapo zina mashiko. Tumia dakika tano hivi kila siku kushadidia fikra chanya inayokinzana na ile inayokudidimiza. Ukifanya hivi kwa takribani siku

thelathini, imani yako itaanza kuchukua mkondo unaofaa. Familia au rafiki anaweza kuwa kikwazo. Pasipo kufahamu, familia yako na rafiki unaoandamana nao huathiri pakubwa hisia zako. Wakiwa na mtazamo hasi huweza kukushawishi ukaanza kuhisi wanavyohisi na kuyaona mambo kwa mtazamo wao. Kukabiliana na hali hii wapaswa kudhibiti hisia zako.

Tawala namna unavyohisi na kukabiliana na hali mbalimbali bila kuathiriwa na wandani hawa. Epuka wandani wa aina hii kadri inavyowezekana, ikiwezekana jitenge nao ili ujifunze kuwa na uhuru wa kufanya maamuzi yako binafsi bila kuathiriwa nao. Unapaswa kupunguza ushirika hata na jamaa zako wanaokuingiza katika hali ya kutamauka. Punguza muda wa kukaa nao hasa wanapogeukia mkondo huu wa kukatiza tamaa.

Mazingira hasi ni kizingiti kingine. Pengine huoni ukuruba baina ya maisha yako na mazingira unamokulia au unamokaa. Ukweli ni kwamba, huenda umedumu katika mazingira hayo na kuyazoea hata ukafikiri huwezi kuyabadilisha. Kadri unavyohisi huna uwezo wa kuyabadilisha ndivyo unajizamisha zaidi katika mtazamo hasi. Ili kukabiliana na hali hii, unahitaji kuelewa kwamba fikra zako au za watangulizi wako ndizo zilikuingiza katika mazingira haya.

Kwa hivyo, unapaswa kubadili mkondo wa fikra zako na kuanza kujaribu mazoezi ambayo umekuwa ukiyaona kama usiyoyaweza. Hatua kwa hatua utagundua panapo jitihada na uelekezi unaofaa kwamba mazoezi hayo yamekuwa mepesi na hivyo kukuhakikishia kuyabadilisha mazingira yako.

Hali zisizoridhisha huweza pia kuchangia mtazamo wako. Unapojikuta ukilalamika jinsi ulivyokerwa na hali fulani, hii ndiyo sababu hasa ya kuwa na mtazamo hasi kuhusu hali hizo. Inaweza kukuwia vigumu kulikubali hili lakini kadri utakavyolikubali mapema ndivyo utayaboresha maisha yako mapema. Kulalamika tu kutakudumisha katika hali zisizokuridhisha. Kwa hivyo, ili uyabadilishe maisha yako sharti ukome kulalamika na kuanza kujikwamua kutoka kwenye hali hizi. Katika kufanikisha jambo lolote jema sharti viwepo vizingiti njiani. Mtendaji wa jambo lolote jema liwalo ana jukumu la kuibuka na mikakati mwafaka ya kuvikabili vizingiti hivi ili afanikishe ndoto yake. Hii ndiyo sababu unapaswa kuchukua hatua kutokea sasa ili kupanga na kutekeleza mikakati itakayoupindua mtazamo wako hasi uwe chanya. Kwa jinsi hii utayabadilisha maisha yako yawe ya kuridhisha zaidi na kuwa kielelezo kwa wengi waliotamaushwa na mitazamo hasi.

## Maswali.

**a)** Kwa kurejelea kifungu hiki, eleza njia za kukabiliana na mtazamo hasi.

Maneno 100-110 (alama 9, 1 utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala Safi**

(b) Kwa kurejelea taarifa hii, eleza vyanzo vya mtazamo hasi kwa maneno 45

**(alama 5, 1 mtiririko)**

**Matayarisho**

**Nakala Safi**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA: (Alama 40)

**(a)** Zilinganishe sauti /p/ na /b/ **(alama 2)**

**(b)** Bainisha majukumu ya viambishi tamati katika neno: **viliwavyo.** **(alama 3)**

**(c)** Tunga sentensi moja ukitumia nomino ambatano na nomino milikishi. **(alama 2)**

**(d)** Fafanua miundo yoyote miwili ya ngeli ya U-ZI **(alama 2)**

**(e)** Ainisha viwakilishi katika utungo huu. **(alama 2)**

Sote tutagawana na wale ambacho nyinyi mtapata.

**(f)** Kanusha. **(alama 2)**

Mwanasiasa aliyeshindwa alitoka na kuacha kura zikiendelea kuhesabiwa

**(g)** Tunga sentensi moja kutofautisha vitate hivi. **(alama 2)**

Pasa

Pasha

**(h)** Andika utungo huu upya bila kutumia vitenzi visaidizi. **(alama 2**

Wao huenda wakawa wanaweza kutuzwa na rais alasiri ya leo.

**(i)** Andika katika usemi wa taarifa. **(alama 3)**

"Wageni wetu mliotutembelea hapa, mko huru kujionea maendeleo ya kaunti yetu," gavana akatamka.

**(j)** Kistari kifupi (-) hutumiwa kuendeleza sauti katika vihisishi. Onyesha matumizi mengine mawili ya akifishi hii. **(alama 2)**

**(k)** Eleza maana mbili zinazoweza kujitokeza katika sentensi hii. **(alama 2)**

Menjo aliletewa ng'ombe na watoto wake.

**(l)** Andika katika udogo hali ya wingi. **(alama 2)**

Aligongwa katika kichwa kwa nyundo alipotoroka kuumwa na nyoka.

**(m)** Tumia neno 'maskini' kudhihirisha dhana hizi. **(alama 2)**

i) Kivumishi

ii) Kihisishi

**(n)** Pambanua kwa jedwali. **(alama 4)**

Waliochelewa waliadhibiwa vikali na mwalimu wao.

Tunga sentensi kudhihirisha chagizo ya namna ya nomino ifuatayo: unyama. **(alama 2)**

**(o)** Fafanua miundo yoyote miwili ya kiima. **(alama 2)**

**(p)** Andika upya sentensi ifuatayo ukianza kwa yambwa tendewa **(alama 2)**

Farida aliwapikia wageni chai kwa jiko.

**(q)** Tunga sentensi moja kubainisha kishazi huru na kishazi tegemezi. **(alama 2)**

**(r)** Eleza uamilifu wa kiambishi 'ji' katika sentensi hii. **(alama 2)**

Mtoto aliyejikata kijidole alipelekwa zahanatini kutibiwa.

**(s)** Andika methali inayoafiki maelezo yafuatayo. **(alama 1)**

Viongozi wanapogombana raia/watu wadogo ndio wanaoumia.

**(t)** Kamilisha:

Kutia kitumbua mchanga ni**……** **(alama 1)**

## 4. ISIMU JAMII (alama 10)

**(a)** Eleza maana ya lugha ya Taifa**.** **Alama 2**

**(b)** Fafanua michango minane ya lugha ya Kiswahili katika kufanikisha ruwaza ya 2030 .**ala 8**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 3

# KISWAHILI

Paper 3

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

## *Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

***a)*** *Andika jina lako, shule, nambari ya mtihani kisha utie sahihi katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*

***b)*** *Jibu maswali manne pekee*

***c)*** *Swali la kwanza ni la lazima*

***d)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Ushairi*

***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | JUMLA | |

## SEHEMU YA A: RIWAYA

***Assumpata K. Matei: Chozi la Heri***

***LAZIMA***

**1**. "Haiwezekani! Hili haliwekazi! Itakuwa kama kile kisa cha yule kiongozi wa kiimla wa kike"

**(a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

**(b)** Eleza kwa kifupi yaliyowapata wahafidhina baada ya usemi huu. **(alama.4)**

**(c)** Riwaya ya chozi la heri inaonyesha maovu yanayotamalaki katika jamii.Thibitisha. **(ala 12)**

## SEHEMU B: TAMTHILIA

***Bembea ya Maisha.***

***Jibu swali la 2 au la 3***

**2.** Fafanua mabadiliko yanayojitokeza katika tamthilia ya **Bembea ya maisha** **(alama20)**

**3.** ***La! Kila mbegu ipandwayo haina budi kuzaa na izaapo mazao yake huvunwa. Mtu hutakasa sahani akijua itamfaa tena. Kinacholelewa hakina budi kulea***

**a)** Eleza mutadha wa dondoo **(alama4)**

**b)** Chambua mtindo katika dondoo **(alama4)**

**c)** Kauli iliypigiwa mstari inaonyesha majukumu ya watoto kwa wazazi. Thibitisha kwa kuonyesha wazi alivyowajibika anayerejelewa na msemaji katika mjadala. **(alama4)**

## SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

***Mapambazuko ya Machweo***

**4.** ***Wanaume katika mataifa mengi barani afrika wametawaliwa na ubabedume***. Jadili kauli hii ukirejelea hadithi ya ***"Fadhila za Punda"*** **(al.20)**

**5.** Huku ukitolea mifano mwafaka ,eleza jinsi ambavyo haki za watoto/vijana zimekiukwa katika hadithi ya ***Mapambazuko ya Machweo*** **(alama 20)**

## SEHEMU D: SHAIRI

### WASIA

5. Huno wakati mufti, vijana nawausia
Msije juta laiti, mkamba sikuwambia
Si hayati si mamati, vijana hino dunia
Uonapo vyang`aria, tahadhari vitakula

Japo aula kushufu, na machoni vyavutia
Dunia watu dhaifu, yaugua nasikia
Vijana nawasarifu, falau mkisikia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

Jepusheni na zinaa, mlale penye sheria
Msije andama baa, makaa kujipalia
Jepusheni na zinaa, madhara kukadiria
Uonapo yyang'aria, tahadhari vitakula.

Ngawa waone wazuri, nadhifu kukuvalia
Wajimwaie uturi, na mapoda kumichia
Si mlango nyumba nzuri, ngia ndani shuhudia
Uonapo vyang'aria , tahadhari vitakula.

Wawapi leo madume, anasa walopapia?
Wamepita ja umeme, leo yao sitoria
Shime enyi wana shime, bora kumcha Jalia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula

Nambie faida gani, nambie ipi fidia
Upatayo hatimani, waja wakikufukua
Ila kufa kama nyani, kasoro yako mkia
Uonapo vyang`aria, tahadhari vitakula.

Vyatiririka tariri, vina vyanikubalia
Alo bora mshairi, pa tamu humalizia
Nahitimisha shairi, dua ninawapigia
Uonapo vyang'aria , tahadhari vitakula.

Ewe Mola mtukuka, si shaka wanisikia
Wakingie wanarika, na anasa za dunia
Amina wangu Rabuka, dua yangu naishia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

**MASWALI:**

**a)** Ni ujumbe gani wanaopewa vijana kupitia shairi?. **(alama 4)**
**b)** Bainisha tamathali mbili za usemi katika shairi hili. **(alama 2)**
**c)** Eleza bahari ya shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. **(alama 2)**
i)idadi ya vipande katika mshororo
ii) mpangilio wa vina katika beti.
**d)** Eleza mbinu zozote mbili za kishairi zilizotumika katika shairi hili. **(alama 2)**
**e)** Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari **(alama 4)**
**f)** Eleza toni ya shairi hili. **(alama 1)**
**g)** Tambua: **(alama 2)**
i) Nafsi neni
ii) Nafsi nenewa
**h)** Eleza umuhimu wa mbinu ya kimtindo iliyotumika katika ubeti wa tano. **(alama 2)**
**i)** Eleza maana ya msamiati: 'aula' **(alama 1)**

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**6. a)** Eleza maana ya miviga. **(alama.2)**
**b) Eleza** sifa tano za miviga. **(alama.5)**
**c) Miviga** ina udhaifu gani. **(alama.3)**
**d) Fafanua** umuhimu wa ngomezi katika jamii. **(alama.6)**
**e) Eleza** vizingiti viwili vinavyokumba ngomezi. **(alama.4)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 4

# KISWAHILI

Paper 1

**Time: 1¾ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

**a)** *Andika jina lako na nambari ya usajili kwenye nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

**b)** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

**c)** *Andika insha* ***mbili****. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima.***

**d)** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*

**e)** *Kila insha isipungue maneno* ***400****.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. | 20 | |
| 2. | 20 | |
| 3. | 20 | |
| 4. | 20 | |
| JUMLA | 40 | |

**MASWALI**

**1.** Umepata tangazo la nafasi ya kazi ya uhariri katika shirika la uchapishaji vitabu vya fasihi andishi kwenye gazeti la ***Taifa Leo***.

Andika barua ya kuomba nafasi hii na uiambatanishe na wasifu kazi wako kwa maelezo zaidi.

**2**. Jukumu la kuzuia msambao wa ***virusi vya korona*** ni la mtu binafsi. Jadili.

**3.** Andika insha itakyothibitisha ukweli wa methali

Mchelea mwana kulia, hulia mwenyewe.

**4.** Anza kwa.

Mwanangu, dunia imebadilika pakubwa lakini chunga mabadiliko hayo yasikuzuzue….

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 4

# KISWAHILI

Paper 2

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

***1***. *Andika **jina lako** na **namba yako** katika nafasi ulioachiwa hapo juu.*

***2.*** *Weka **sahihi yako** na **tarehe** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.*

***3.*** *Jibu maswali yote.*

***4.*** *Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa wazi katika kijitabu hiki cha maswali.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE.**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

**1. UFAHAMU: (Alama 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia**

Mateso ya wanawakiwa ni suala la kijamii linalofaa kutazamwa kwa darubini kali. Hata hivyo wanaoathirika zaidi ni watoto ambao bado wako katika umri unaohitaji kulelewa na kupewa mahitaji ya msingi kama mavazi, malazi, elimu na mengine anuwai. Hali ya kuachwa na wazazi imekuwa ikizikumba jamii tangu enzi za mababu na kila itokeapo, wanajamii huipokea kwa mitazamo tofautitofauti, hivyo kuwafanya wanawakiwa kuathirika sana.

Baadhi ya jamii zina imani za kijadi pamwe na mila zilizochakaa zinazozifanya kuamini kuwa baadhi ya vifo hutokana na laana. Wengine huchukulia kuwa mwendazake ameondolewa na ulozi. Imani kama hizi huifanya jamii kuwatia watoto walioachwa katika mkumbo ule ule, hivyo kuwaangalia kwa macho yasiyo ya kawaida. Hili husababisha dhana gande. Hali hii husababisha kuwachukulia watoto kama wanaotoka katika kizazi kilicholaaniwa. Jamii basi hukosa kuwapa watoto hawa stahiki yao. Hata wanapojitahidi kuiwania nafasi yao, waliowazunguka huwavunja mioyo. Jitihada zao huishia kuwa si chochote kwa kuwa jamii inawatazama kama waliolaaniwa.

Punde baada ya mzazi mmoja au wote wawili waendapo wasikorudi, inatarajiwa kwamba aliyeachiwa mtoto, awe mzazi wake, mwanafamilia au jirani awajibike na kumtunza mwanamkiwa. Kunao kadha wa kadha wanaowajibika – ninawavulia kofia. Hata hivyo wengi hutelekeza jukumu hili walilopewa na Muumba. Si ajabu basi kuona kuwa idadi ya watoto wanaozurura mitaani inazidi kuongezeka kila uchao. Ukichunguza utakuta kuwa wengi wa watoto hawa ni waliopotelewa na wazazi wao. Inakera zaidi kugundua kuwa baadhi ya watoto hawa wana mzazi mmoja. Kwamba mke au mume wa mtu ameaga, au iwe kwamba mzazi mmoja alimzaa mtoto na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi, aliyeachiwa ana jukumu la kumpa mwanawe mahitaji ya msingi. Machoni pa Jalali, kila anayeupuuza wajibu huu ana hukumu yake siku ya kiama!

Ni haki ya kila mtoto kupata elimu. Katika katiba ya Kenya mathalan, elimu ya msingi, yaani kuanzia shule ya chekechea had kidato cha nne ni ya lazima. Tangu hapo hata hivyo, jamii zimekuwa zikiwanyima wanawakiwa wengi elimu. Kwamba kunao wachache wanaowaelimisha baadhi ya wanawakiwa, ni kweli. Hata hivyo, wengi hukosa hata wa kuwapeleka katika shule ya chekechea, hivyo kuishia kutojua hata kuandika majina yao. Mfikirie mtu katika karne ya 21, asiyejua kusoma wala kuandika! Nani ajuaye, huenda huyo mwanamkiwa asiyepelekwa shuleni ndiye angalikuwa profesa, daktari, mwalimu, rubani au msomi mtajika na mtaalamu wa uwanja muhimu katika jamii!

Kila mtoto ana haki ya kulelewa hadi kufikia utu uzima kabla ya kupewa majukumu mazito. Katika katiba ya Kenya, utu uzima, ulio umri wa kuanza kufanya kazi huanzia miaka 18. Wanaohakikisha watoto hawa wametimiza utu uzima kabla ya kufanyishwa gange ngumu wanafaa pongezi. Hata hivyo wanawakiwa wamekuwa wakitumiwa na wengi kama punda wa huduma. Wanaaila wengine huwachukua wanawakiwa kwa machozi mengi wazazi wao waagapo nakuapa kuwahifadhi na kuwatunza wana wale wa ndugu zao, kumbe ni machozi ya simba kumlilia swara! Hata kabla ya mwili wa mzazi mhusika kuliwa na viwavi, mateso kwa mtoto yule huanza, akawa ndiye afanyaye kazi zote ngumu. Utakuta watoto wao wamekaa kama sultan bin jerehe huku mwanamkiwa yule

akiwapikia, kuwafulia nguo, kudeki, karibu hata awaoshe miili! Kazi kama zile za shokoa huwa za sulubu na aghalabu husindikizwa kwa matusi yasiyoandikika.

Baadhi ya waja walionyimwa huruma huwahadaa wanawakiwa na kuwapeleka ng'ambo wakitumia vyambo, kuwa wakifika kule watapata kazi za kifahari. Maskini wale hushia kushikwa shokoa, wakawa watumwa katika nyumba za waajiri wao, bila namna ya kujinasua. Wengine hushia kutumiwa kama watumwa wa 'kimapenzi' katika madanguro, miili yao ikawa ya kuuziwa makahaba waroho wasiojali utu. Kujinasua kule huwa sawa na kujitahidi kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu, maadamu wanawakiwa aghalabu hukosa watu wenye mioyo ya huruma ya kuwashughulikia. Wengi huitumia methali 'mwana wa ndugu kirugu mjukuu mwanangwa' kuwapuuzilia mbali wanawakiwa ambao hukimbiliwa tu wabinafsi hawa wanapofaidika wenyewe.

## MASWALI

**a)** Ipe taarifa hii anwani mwafaka. **(alama 1)**
**b)** Eleza dhana ya mwanamkiwa kwa mujibu wa kifungu. **(alama 2)**
**c)** Eleza imani za kijadi kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 2)**
**d)** Jadili masaibu yanayowakumba wanawakiwa. **(alama 4)**
**e)** Eleza haki mbili za kikatiba zilizokiukwa kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 4)**
**f)** Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na kifungu. **(alama 2)**
**i)** Inakera
**ii)** Majukumu

### 2. UFUPISHO: (Alama 15)

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Runinga kama kifaa kingine chochote cha mawasiliano kina manufaa yake. Kwanza kabisa, ni nyenzo mwafaka ya kufundishia. Vipindi vinavyopeperushwa katika runinga huwa na mafunzo kemkemu kwa mtu wa kila rika. Halikadhalika, runinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, runinga ikitumika pamoja na michezo ya video huauni katika ukuzaji na ustawishaji wa stadi ya kujifundisha au kujielimisha. Michezo ya video, hasa ya kielimu, huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemchemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa. Televisheni ni mojawapo ya vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu huwa ni liwazo kutokana na shinikizo na migogoro tunayokabiliana nayo kila siku. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu.

Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga huwa ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha

ujumbe usio na maadili, kama vile matumizi ya nguvu za mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo ya adabu, ubaya wa kimavazi na maonevu ya rangi, dini, jinsia, kabila na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya mambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanaowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwauliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa familia. Matumizi kama haya huwapa wanafamilia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii. Ukilinganisha na vyombo vingine vya burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala yake, tajriba ya televisheni huwa ya kibinafsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia, televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Halikadhalika, runinga na video aghalabu hueneza maadili yasiyofaa. Mathalani, baadhi ya vipindi vya televisheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa, n.k. Hulka hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinazofuatwa na waliostaarabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya dawa za kulevya kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa hila na udanganyifu mwingi ambao huwavutia vijana na watoto wengi. Si ajabu mtu anapouliza wanaotumia vileo hivi walivyoanza, watajibu kutokana na athari za matangazo katika runinga na vyombo vingine.

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa vipindi vingi vya vibonzo hushirikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya wawaelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

**a)** Fupisha aya tatu za kwanza za (maneno 70 – 75) **(alama 7, 2 za utiririko)**

**Matayarisho**

**Jibu**

**b)** Eleza udhaifu wa runinga na video. (maneno 50 – 51) **(alama 5, 1 ya utiririko)**

**Matayarisho**

***JIBU***

## MATUMIZI YA LUGHA: **(alama 40)**

**a)** Taja aina mbili kuu za ala za kutamkia sauti **(alama 2)**

**b)** Taja mfano mmoja mmoja wa sauti zifuatazo **(alama 2)**

Kimadende_____

Kipasuo kwamizo_____

**c)** Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi sahili **(alama 2)**

**d)** Ainisha mofimu katika neno lifuatalo **(alama 3)**

Tulimpikia_____

**e)** Ainisha vitenzi katika sentensi: Kitabu anachotaka kusoma ki mezani **(alama 3)**

**f)** Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi kiteuzi **(alama 2)**

**g)** Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? **(alama 2)**

a) Uzi_____

b) Muda_____

**h)** Tumia 'o' rejeshi ya kati katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Watu ambao walifika jana ni wale ambao walitoka mbali

Onyesha shamirisho kipozi na ala katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Mwindaji haramu alimuua ndovu kwa bunduki

**i)** Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale **(alama 3)**

Kilipikwa jana jioni

**j)** Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi **(alama 2)**

Msingesoma kwa bidii, msingepita

**k)** Tunga sentensi moja kudhihirisha dhamira/jukumu hili **(alama 2)**

Rai/ombi

**l)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Mtoto ambaye alianguka jana ana maumivu mengi

**m)** Onyesha matumizi yoyote mawili ya kiwakifishi: koma/kituo **(alama 2)**

**n)** Tumia neno 'Nairobi' kama **(alama 2)**

**Nomino**

Kielezi

**o)** Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya kuku na gugu **(alama 2)**

**p)** Onyesha matumizi ya kiambishi -ji- katika sentensi **(alama 2)**

Mwongeleaji stadi anajishaua sana.

**q)** Andika katika usemi wa taarifa **(alama 2)**

"Wageni wangu watafika saa ngapi? Mama aliuliza

**r)** Unda nomino kutokana na kitenzi **(alama 1)**

Safari

**4. ISIMUJAMII:** **(alama 10)**

Nipe chai, andazi mbili na egg moja**……**

**a)** Taja sajili inayorejelewa na maneno haya **(alama 2)**

**b)** Fafanua sifa nne zinazohusishwa na sajili hiyo **(alama 8)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 4

# KISWAHILI

Paper 3

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

***a)*** *Andika jina lako, shule, nambari ya mtihani kisha utie sahihi katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
***b)*** *Jibu maswali manne pekee*
***c)*** *Swali la kwanza ni la lazima*
***d)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Ushairi*
***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | JUMLA | |

**SEHEMU A: Riwaya**

**1. LAZIMA**

**Assumpta K. Matei: Chozi la heri**

"Hili lilimtia ……. uchungu, akajiona kama aliyedhalilishwa na mwanamke."

**(a)** Yaweke maneno haya katika muktadha wake **(alama 4)**

**(b)** Taja suala linalodokezwa katika dondoo hili **(alama 1)**

**(c)** Kwa kutumia hoja kumi na tano, eleza namna suala ulilolitaja hapo juu **1 (b)** linalijitokeza **(ala. 15)**

**SEHEMU B: TAMTHILIA**

**Bembea ya Maisha (Timothy Arege)**

**Jibu swali la pili au la tatu**

**2.** Huku ukirejelea tamthilia ya ***Bembea ya Maisha***, eleza tofauti ya hali maendeleo kati ya hospitali za mjini na hospitali za kijijini **(alama20)**

**3.** Eleza mambo yanayorudisha bara la Afrika nyuma kulingana na tamthilia ya **Bembea ya Maisha** **(alama20)**

**SEHEMU C: Hadithi Fupi**

**Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine**

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** Mwandishi katika hadithi ya Msiba wa Kujitakia alifaulu kutumia mbinu ya uwili. Thibitisha. **(al. 20)**

**5.** Mwandishi wa hadithi ya "**mapambazuko ya machweo**" uwajibikaji kwa kiasi kikubwa mno. Illihirisha ukweli na kauli hii **(alama 20)**

**SEHEMU D: Fasihi Simulizi**

**6. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

Heri ujue mapema
Nasaba yetu haina woga
Woga haumei kwetu, humea kwa kina mamako.
Tulichinja jogoo na fahali ili uwe mwanaume.

Ah! Kisu cha ngariba ni kikali ajabu.
Iwapo utatikisa kichwacho.
Uhamie kwa wasiotahiri,
Ama tukwite njeku.

Mpwangu kumbuka hili,
Wanaume wa mlango wetu
Si waoga wa kisu
Wao hukatwa mchana hadi usiku
Wala hawalalamiki.

Siku nilipokatwa
Nilisimama tisti
Nikacheka ngariba kwa tashtiti
Halikunitoka chozi.

Iwapo utapepesa kope
Wasichana wa kwetu na wa mbali
Wote watakucheka
Ubaki ukinuna.

Sembe umepokea
Na supu ya makongoro ukabugia
Sema unachotaka
Usije kunitia aibu

**Maswali;**

**(a)** Taja na uthibitishe shughuli zozote za kiuchumi za jamii ya wimbo huu **(alama 4)**
**(b)** Ni nani mwimbaji wa wimbo huu na anawaimbia nani? **(alama 2)**
**(c)** Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha **(alama 2)**
**(d)** Mwimbaji wa wimbo huu ana taasubi ya kiume. Thibitisha kauli hii. **(alama 2)**
**(e)** Eleza wajibu wa nyimbo katika jamii **(alama 6)**
**(f)** Ijapokuwa nyimbo ni nzuri, zina ubaya wake. Thibitisha kauli hii **(alama 4)**

## SEHEMU E: USHAIRI (ALAMA 20)

**Jibu swali la 7 au la 8**

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Kama dau baharini, duniya inavyoyumba,
Limeshamiri tufani, kila mmoja lakumba,
Viumbe tu hali gani!

Duniya yatishika, utahisi kama kwamba,
Vilima vyaporomoka, na kuvurugika myamba,
Viumbe tu hali gani!

Tufani hilo la kusi, languruma na *kutamba*,
Linapuliza kwa kasi, hapana kisichoyumba,
Viumbe tu hali gani!

Mujiwe ni kubwa sana, mfanowe kama nyumba,
Yazuka na kugongana, wala hatuna la *kwamba*,
Viumbe tu hali gani!

Mibuyu hata mivule, kama usufi na pamba,
Inarusha vilevile, *seuze hiyi migomba*
Viumbe tu hali gani!
Ni kipi kilotuliya, tuwazeni na kudumba,
Mandovu kiangaliya, yagongana na masimba,
Fisi wako hali gani!

Hata papa baharini, tufani limewakumba,
Walioko mikondoni, kila mmoja *asamba*,
Dagaa wa hali gani!

Mashehe wa mdaduwa, kwa ubani na uvumba,
Tufani hilo kwa kuwa, kusoze kwake kutamba,
Itokee afueni!

**(Shairi la 'Tufani' la Haji Gora Haji, katika *Tamthilia ya Maisha*, uk 62)**

**Maswali;**

**(a)** Taja na ueleze mikondo ya shairi hili **(alama 4)**

**(b)** Eleza dhamira ya shairi hili **(alama 2)**

**(c)** Taja tamathali za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. **(alama 2)**

**(d)** Eleza muundo wa shairi hili **(alama 4)**

**(e)** Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa tano. **(alama 3)**

**(f)** Onyesha matumizi ya idhini ya kishairi . **(alama 3)**

**(g)** Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mjibu wa shairi hili **(alama 2)**

(i) Mdaduwa :

(ii) Kutamba :

**8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Daima alfajiri na mapema
Hunipitia na jembe na kotama
Katika njia iendayo Kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani;
Nimuonapo huwa anatabasamu
Kama mtu aliye na hamu
Kushika mpini na kutokwa jasho
Ili kujikimu kupata malisho.

Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotumbuiza
Utadhani huwa vimemngojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimtetea

Nao umande kumbusu miguuni;

Na miti yote hujipinda migogo
Kumpapasa, kumtoa matongo;
Na  yeye kundelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua
Akichekelea ha ha ha ha ha ha …….

Na mimi kubaki kujiuliza
Kuna siri gani inayomliwaza?
Au ni kujua au kutojua?
Furaha ya mtu ni furaha gani?
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao
Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonga roho
Ayalimia matumbo ya waroho.
Kuna  jambo gani linalomridhisha?
Kama si kujua ni kutojua
Lait angalijua, laity angalijua!

**Maswali:**

**a)** Eleza hali ya mzungumziwa katika shairi hili. **(alama 2)**

**b)** Huku ukitoa mifano, onyesha aina mbili za uhuru wa kishairi uliotumiwa katika shairi hili **(ala. 4)**

**c)** Fafanua aina tatu za taswira ukirejelea ubeti wa pili **(alama 3)**

**d)** Maswali ya balagha katika shairi hili yanasisitiza maudhui yapi? **(alama 2)**

**e)** Kwa kutoa mifano, bainisha vipengele vitatu vya Kimtindo katika shairi hili **(alama 3)**

**f)** Eleza toni ya shairi hili **(alama 2)**

**g)** Bainisha nafsineni katika shairi hili **(alama 1)**

**h)** Eleza muundo wa shairi hili **(alama 3)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 5

# KISWAHILI

Paper 1

**Time: 1¾ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

## *Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

**a)** *Andika jina lako na nambari ya usajili kwenye nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

**b)** *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

**c)** *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima.***

**d)** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*

**e)** *Kila insha isipungue maneno **400**.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. | 20 | |
| 2. | 20 | |
| 3. | 20 | |
| 4. | 20 | |
| JUMLA | 40 | |

## SWALI LA KWANZA.

**1.**Andika barua kwa rafiki yako ukimweleza jinsi michezo inavyoweza kuimarishwa katika shule ya Sokota.

**2.**Mapenzi ya kiholela yamekuwa tatizo sugu katika taifa.Jadili

**3.** Tunga kisa kinachodhihirisha maana ya methali ifuatayo;ukiona vyaelea vimeundwa.

**4.**"Ukosefu wa nidhamu ni kosa kubwa kwa mwanafunzi kama wewe.Pokea barua hii na uje na mzazi baadaya wiki mbili**...**"Endelea.

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 5

# KISWAHILI

Paper 2

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA**

***a.*** *Karatasi hii ina kurasa kumi na mbili zilizopigwa chapa.*
***b.*** *Andika jina na nambari yako katika nafasi ulioachiwa hapo juu.*
***c.*** *Jibu maswali yote.*
***d.*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
***e.*** *Majibu yote yaandikwe katika lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

## A. UFAHAMU (Alama 15).

*Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.*

Binadamu heshi kuwa na falsafa zinazojiri akilini mwake. Amejichanjia kijisayari chake cha kufikirika mfano wa Mirihi katika falaki yake ya maisha. Ni sayari ndogo ambayo imejitenga nasayari nyingine kama vile kausi.

Katika Mirihi kuna viumbe mahuluti vyenye mitindo ya kustaajabisha. Tofauti na Kausi ambayo mabinti huwa na urembo wa kiasilia, wanamirihi ni "warembo" mithili ya walioanguliwa ja vifaranga. Viganja vyao na nyuso zao huwa zimekandwa kwa mafuta ya zebaki zikawa nyororo japo wengi huwa mithili ya suriama. Wasalaminiapo na wanakausi mikwaruzo yao huwachipua ngozi kwa kazi ya sulubu waifanyayo shambani. Fauka ya uchotara huo, wamefungasha kiasi huku wamejisetiri kwa vijisuruali na vijisketi ambavyo vimewabana kana kwamba vimeundwa kwa vitambaa vya mikononi na kutafuta misaada kutoka kwa majirani kuvivua na kuvivaa.

Wanakausi waliovalia nguo zinazowafika kwenye visigino, huchushwa mno na hivi vijiguo vinavyowasetiri hadi kwenye sisemi vilengesambwa, ukipenda magotini, bali kwenye mapaja. Ni kweli kwamba waso haya wana mji wao.Wanapodatia hasa kwenye hafla za maziko au arusi katika sayari ya Kausi, wanakausi hujibana pembeni kujionea malimwengu ulimwenguni.

Minong'onezo ndio itajaa hewani "ni yakini Pemba ndiko kwenye nguo na wenda uchi wapo". Katika hafla hizo, wale mabinti wazuri wa Mirihi hubeba vibogoshi ambamo mara kwa mara hutoa vidubwasha vidogo vidogo na kuendelea kujipodoa huku shughuli zinapoendelea. Pengine huenda umesahau kuwa katika mipango na makadirio ya matumizi ya hafla hiyo marejeleo yanayokaririwa huwa "..... wajua watu wa Mirihi hawapendi....."

Mabinti wazuri wa Mirihi kila mmoja huwa amejibebea mwavuli wa kujizuia mvua au jua huku amekumbatia maji ya chupa ya kutoka kwenye sayari ya Mirihi.

Wanakausi walalahoi huwa wakikata kiu yao rahisi kutoka kwenye mapipa yaliyojazwa maji au kwenye mifereji waliyobahatika kuwekewa na wizara ya maji, kwa kutumia viganja vya mikono. Mabwana wa Mirihi hawana haja na miavuli, wao huwa watu wenye zao. Huvalia kofia nene zinazoonekana kama somberero. Watembeapo huning'iniza funguo za magari ya kifahari katika mkono wa kushoto na simu za rununu katika mkono wa kulia.

Hapa na pale watakuwa wakiwasiliana kwa simu zao na pia kupiga gumzo na maghulamu wa Kausi ambao kwa kawaida watakuwa wakiwarai Wanamihiri, "Utaniacha hivyo?"

Baada ya hafla, mlo ambao huwa Wanamirihi hupakuliwa huku Mabwanamirihi wakidakia wasichelewe, mabintimirihi wakinyofoa kwa mikono au kung'ofoa kwa midomo yao myekundu na Wanakausi wakichungulia kwa mbali wakisubiri nafasi yao itimie.

Ghafla mawingu yataanza kutanda upande wa mashariki na mambo sasa yatachukua mkondo mpya. Wanamirihi mchakamchaka huengaenga, mbio kwenye magari yao. Lakini kuna wale ambao hawana magari ya kukimbilia. Kawaida yao huwaita Wanamirihi wenzao faraghani "Baba fulani umejaza?".

Wengine hubaki kusema, "Huenda basi letu likaniacha, tutaonana nikija wikendi."Hali iwapo mwanana, Wanakausi watakuwa sasa ndio wakati wa kujitambulisha na wengine kuyajaza magari ya Wanamirihi ya kifahari, kwa maembe, avocado, ndizi na makochokocho ya vitu vya shambani. Baada ya miezi kadha,Wanakausi wachache watawazuru Wanamirihi kuwapa shukurani katika kijisayari chao cha Mirihi.

Hapo sasa watafumbua jibu la kitendawili watakapokumbana na Bintimirihi amebeba kijikaratasi cha nailoni kimejazwa embe dodo moja, sukumawiki bila kusahau kisehemu cha nyama alichopimiwa cha shilingi kumi. Kwa kuwa atapata malazi kwake atamshauri, ".....pengine unionyeshe bucheri tununue nyama.... tupitie dukani tununue ....." hapo kwake Malaika atakuwa ameshuka kutoka Kausi hadi Mirihi.

Lakini wengine ni wale ambao pindi tu utakapowasalimia watakukwa na "zamu ya usiku siku hiyo." Wanaovalia somberero watamlaki mwanakausi kwa mlahaka wa kifalme ili akastaajabie vitu kama **majirafu,** mazulia, makochi, taja nitaje.

Yule wa awali atalala usiku huo usingizi mnono usio wa bugudha na kwenye kochi huku akihimiria kurauka mapema asikutwe na waliolala nyuma ya pazia. Hisia za Mwanakausi zitamrudisha katika tamthilia ya WoleSoyinka "Masaibu ya ndugu Jero kuwa "vidole vyote havikuumwa sawa." Mirihi ni sayari iliyo sheheni watu na viatu, kumbe Kausi ni shamba la paukwa pakawa la Edeni. Tafakari haya!

**Maswali.**

**a)** Andika anwani mwafaka ya taarifa hii. **(alama 2)**

**b)** Eleza tofauti kati ya wanawake wa Mirihi na wale wa Kausi. **(alama 3)**

**c)** Ni dhahiri kuwa Mirihi ni Sayari yenye watu na viatu. Nini maana ya viatu. Je, kuna viatu hapa? Thibitisha. **(alama 3)**

**d)** Kwa mujibu wa taarifa, mabinti wa mirihi ni wa tabaka lipi? Thibitisha. **(alama 3)**

**e)** Mwandishi anamaanisha nini anaposema " utaniacha hivyo?" **(alama 2)**

**f)** Eleza maana ya: **(alama 2)**

i. Jirafu._____

ii. Vibogoshi._____

## B. UFUPISHO (Alama 15)

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*

Mitihani imetumiwa siku nyingi kama kigezo cha kupima werevu wa mwanafunzi katika kutekeleza majukumu ya kiakili yenye kuhitaji stadi mbalimbali. Hii ni njia ya kuaminika na ni rahisi ambayo imetumiwa miaka mingi na watahini kukadiria uwezo wa mtu. Lakini wale wanaopinga mitihani wanasema kuwa mitihani haipimi kwa njia inayoaminika uwezo wa kiakili wa mwanafunzi, badala

yake, mitihani inakadiri tu uwezo wa mwanafunzi wa kukadiria mambo kama kasuku kwa muda mfupi uliojaa vitisho na shinikizo.

Wasioithamini mitihani pia wanadai kuwa mitihani humpa mtahiniwa wasiwasi mwingi. Hii ni kwa sababu hadhi na umuhimu wa mitihani imekuzwa sana miongoni mwa watahiniwa na jamii zima kwa jumla. Mitihani ndio kigezo pekee kinachokadiria kufaulu au kutofaulu Kwa mwanafunzi. Mustakabali wa mwanafunzi kuamuliwa na mtihani. Watahini hawajali Sana masuala mengine ambayo yanaweza kuhathiri jinsi mwanafunzi anavyoweza kuufanya mtihani. Kwa mfano, mtahiniwa anaweza, kuwa mgonjwa, au pengine hakulala vizuri siku iliyotangulia mtihani. Haya yote ni masuala yanayoweza kumfanya mtahiniwa kutofanya vizuri katika mtihani.

Elimu nzuri humfundisha mwanafunzi kutumia akili. Lakini mfumo wa elimu unaopendelea mitihani haufanyi hivyo. Mfumo wa aina hiyo husisitiza kufundisha yale yale yanayopatikana katika mwongozo uliotolewa tu. Mwanafunzi hapewi motisha ili kusoma kwa mapana na marefu ili kupanua akili yake. Badala yake mwanafunzi hufungiwa kwenye uwanja finyu ambamo haruhusiwi kutoka. Mwalimu naye kadhalika hana uhuru wa kumfundisha mwanafunzi kile anachofikiria kuwa muhimu katika maisha. Badala yake jukumu kubwa analoachiwa mwalimu huwa ni kumpa mwanafunzi mbinu za kukujibu maswali na kupita mtihani.

Ingawa wanaoitetea mitihani hudai kuwa matokeo ya mitihani ni ya kuaminika kwa sababu husahihishwa na watu wasiowajua watahiniwa, lakini ni vizuri pia kukumbuka kuwa watahini ni binadamu tu. Binadamu huchoka, huhisi njaa na zaidi ya yote anaweza kufanya makosa. Licha ya hayo yote, watahini hutakiwa kusahihisha rundo kubwa la karatasi, kwa muda mfupi. Mjadala uliopo kati ya wanaopendelea mitihani na wale wasiopendelea watukumbusha kuwa kuna haja kubwa ya kuendelea kuboresha mfumo wa mitihani ili uweze kukadiria kwa yakini uwezo wa kiakili wa mtahiniwa.

**Maswali.**

**a)** Fupisha aya ya kwanza na ya pili. (**maneno 60)(alama 9, 1 ya utiririko)**

**MATAYARISHO**

**JIBU**

**b)** Fupisha aya ya tatu na ya nne. (maneno 50)(alama 6, 1 ya utiririko)

**MATAYARISHO**

**JIBU**

**C. MATUMIZI YA LUGHA. (ALAMA 40)**

**a)** (i) Taja konsonati mbili zinazotamkiwa katika kaakaa gumu. **(alama 2)**

**(ii)** Sauti ulizotaja hapo juu ni za aina gani? **(alama2)**

**b)** (i) Shadda ni nini? **(alama 1)**

**(ii)** Weka shadda katika maneno yafuatayo. **(alama2)**

Ua _____

Kiwakilishi_____

**c)** Tunga sentensi mbili kuonyesha dhana tofauti zinazobainishwa na kiimbo. **(alama2)**

**d)** (i) Kiambishi ni nini? **(alama 1)**

(ii) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo. **(alama3)**

Kilicholiwa.

**e)** Bainisha maneno katika sentensi ifuatayo. **(alama 3)**

Kumbe mtu mfupi anarukia lile zuri.

**f)** Maneno yafuatayo yamo katika ngeli gani. **(alama 2)**

(i) Wembe_____

(ii) Minyoo_____

**g)** Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa wingi. **(alama 3)**

Ngamia alibeba hema lililotengenezwa kwa ngozi ya chui.

**h)** Tunga sentensi inayodhihirisha matumizi ya 'O' rejeshi tamati. **(alama 2)**

**i)** Onyesha hali iliyotumika katika sentensi ifuatayo. **(alama1)**

Mganga aonekana akiwa uchi.

**j)** Kanusha. **(alama 1)**

Ningekuwa kasisi ningewafanya mwende mbinguni.

**k)** Eleza matumizi mawili ya kiambishi –ji- **(alama 2)**

**l)** Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya visanduku. **(alama 4)**

Ng'ombe akamuliwaye atachinjwa kesho.

**m)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi. **(alama 3)**

Mtaalamu alituambia kuwa kusoma kwa mapana kungepalilia ubunifu wa wanafunzi hao wao.

**n)** Tunga sentensi moja moja ukitumia maneno yafuatayo katika kauli ulizopewa mabanoni. **(alama 2)**

**(i)** Fumba (tendata)

**(ii)** Kwaa (tendama)

**o)** Tunga sentensi mbili tofauti kudhihirisha maana mbili za kitawe 'somo'. **(alama2)**

**p)** Tambua shamirisho na chagizo katika sentensi hii. **(alama 2)**

Juma alimjengea nyanya nyumba kwa mawe vizuri sana.

## D. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

**a.** Eleza kwa ufupi jinsi mambo yafuatayo yanavyothibiti mitindo ya lugha.

Mazingira **(alama 4)**

Madhumuni **(alama 2)**

Malezi **(alama 4)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 5

# KISWAHILI

Paper 3

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

## *Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

***a)*** *Andika jina lako, shule, nambari ya mtihani kisha utie sahihi katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*
***b)*** *Jibu maswali manne pekee*
***c)*** *Swali la kwanza ni la lazima*
***d)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Ushairi*
***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | JUMLA | |

## SEHEMU A. RIWAYA YA CHOZI LA HERI

1. " …na ikitokea kwamba atauliza swali anakuwa mpokezi wa makonde ,vitisho na matusi ?"

**i.** Eleza mukatadha wa dondoo hili**.** **(Alama 4)**
**ii.** Taja na ueleze umuhimu wa tamathali ya usemi uliyotumika dondooni**.** **(Alama4)**
**iii.** Mabadiliko ni aushi. Jadili kwa kurejelea riwaya nzima ya Chozi la Heri. **(alama 12)**

## SEHEMU B. TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA. (Alama 20)

**2.** Eleza namna wahusika mbalimbali wanakabiliana na changamoto zinazowakumba katika tamthilia ya **Bembea ya Maisha** **(alama20)**

**3.** ***'Nilikupata wapi? Mahututi!'***

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili **alama4)**
**b)** Bainisha mbinu mbili za kimtindo zilizomo kwenye dondoo **alama2)**
**c)** Onyesha toni ya msemaji **alama2)**
**d)** Jadili changamoto alizopitia msemewa wa maneno haya **alama12)**

## SEHEMU C. MAPAMBAZUO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINEZO

**4.** Wafanyikazi katika nchi nyingi zinazoendelea wanakumbwa na changamoto nyingi sana. Thibitisha hali hii kwa kurejelea hadithi ya " ***harubu ya Maisha*** **(alama 20)**

**5.** Ukombozi wa wanawake unakumbwa na vizingiti vingi sana. Jadili ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi ya sabina. **(alama 20)**

## SEHEMU D. FASIHI SIMULIZI (ALAMA 20)

**6.** Dunia hadaa,ulimwengu shujaa.Mnachohitaji mlipofikia, ni ujasiri wa simba kuyakabili maisha.Adabu na bidii yenu leo, ni miche itakayozaa matunda, matunda matamu ya maisha mema kesho.Sitaki muziandame nyendo potovu . Mtakuwa mnajiponza wenyewe ; na hilo litakuwa sawa na kuutumbukiza mustakabali wenu kwenye shimo lenye kina kirefu na giza totoro.Jueni ujana ni moshi na ukienda haurudi.

(a)
**i.** Tambua kipera hiki na utoe ithibati**.** **(Alama 2)**
**ii.** Ni sifa zipi za kipera hiki zilizojitokeza hapom juu. Eleza kikamilifu **(alama 5)**

(b) Misimu hutumia mbinu anuwai katika uundaji wake. Taja tano na utolee mifano mwafaka.. **(Alama 5)**

(c) Eleza mbinu ambazo ungetumia kufanikisha kipera hiki**.** **(Alama 8)**

**7.**

**a)** Eleza maana ya miviga. **(Alama 2)**

**b)** Taja sifa tano za miviga**.** **(Alama 5)**

**c)** Pendekeza njia tatu za kuhifadhi kipera cha miviga. **(alam 3)**

**d)** Eleza udhaifu wa mbinu zifuatazoza ukusanyaji data ya fasihi simulizi.

**(i)** Hojaji **(alama3)**

(ii) Kushiriki **(alama 3)**

**e)** Fafanua matatizo yanayomkabili mtafiti wa fasihi simulizi nyanjani. **(alama 4)**

**SEHEMU E. USHAIRI**

Swali 8.

Hakika siku ya leo, ni siku ya majivuno
Basi pasiwe na choyo, na usonono
Tulekezane yaliyo, unawiri Muungano.

Tuzisafisheni nyoyo, pasiwe na miguguno
Yaongoke tutakayo, kusiwe na mabishano
Mbegu hii tupandayo, ilete mema mavuno.

Tufungulie upeo, Mola usiye mfano
Pa kitasa na komeo, tupite bila kinzano
Tupitishe njia hiyo, pasina masongamano

Twakuomba uumbao, mkono vyanda vitano
Tushikane hii leo, tuwe moja tangamano
Tupendane kwa pumbao, hali na maridhiano

Aliye ana machukiyo, adui wa Muungano
Naazibe masikiyo, asisikie maneno
Kisha awe kibogoyo, asiwe na moja jino.

Ya Ilahi ujalie, juu wetu Muungano
Nuru yake izagae, na nguvu za mapigano
Hasidi mpe hakie, mateso yaso mfano

Watamati komeleo, kuimba kwangu hukuno
Nataka maendeleo, yasiyo na malumbano
Daima tuwe ni ngao, palipo msagurano

**(i)** Huku ukitoa mifano thibitisha kuwa shairi hili ni sala. **(alama 4)**

(ii) Liweke shairi hili katika bahari mbili ukitumia: **(alama 2)**

Idadi ya

(i) Mishororo

(ii) Vina

(iii) Onyesha muundo wa shairi hili. **(alama 5)**

(iv) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. **(alama 3)**

(v)ukitoa mifano eleza umuhimu wa idhini zifuatazo kama zilivyotunika katika shairi. **(Alama 4)**

**a)** Inkisari

**b)** Mazda

**c)** Kuboronga sarufi

**d)** Tabdila

(vi) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. **(alama 2)**

**(i)** Usonono –

**(ii)** Msagurano –

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 6

# KISWAHILI

Paper 1

**Time: 1¾ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika insha* ***mbili****. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima*** *kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*

***b)*** *Kila insha isipungue maneno 400.*

***c)*** *Kila insha ina alama 20.*

***d)*** *Kila insha* ***lazima*** *iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

***Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee***

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| **Jumla** | **40** | |

# MASWALI

**1.** Umetangazwa kuwa mwanafunzi bora katika mtihani wa kitaifa. Mwalimu Mkuu wa shule ya upili ya Tuamke amekualika katika shule hii yake kuwahutubia wanafunzi kuhusu kilichochangia ufanisi wako. Andika hotuba yako.

**2.** Fafanua hatua ambazo jamii imechukua kuimarisha maisha ya wanawake katika jamii.

**3.** Andika kisa kinachodhihirisha maana ya methali; Mui huwa Mwema.

**4.** Andika insha itakayomalizia kwa: Nilijitazama na kujidharau kwa nini sikuwafahamisha walimu jambo hilo mapema.

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 6

# KISWAHILI

Paper 2

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

## *Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

- *Andika **Jina lako** na Nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- *Tia**sahihi yako**kisha **tarehe** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa*
- *Jibu maswali yote katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha majibu.*
- *Hakikisha kwamba kurasa zote zimepigwa chapa.*
- *Majibu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya **Kiswahili.***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

## 1. UFAHAMU: (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Tumeshuhudia baadhi ya ndugu wa familia moja wakiishi bila maelewano na wakati mwingine kukata kabisa kabisa mawasiliano. Hivi leo kuna familia ambazo haziwezi kuketi pamoja na kumaliza matatizo yao, na badala yake huchukua njia za vita ugomvi na hata pengine mauaji kama suluhisho la migogoro yao.

Kawaida maisha sio mstari mnyoofu. Kuna milima,mabonde,kona na hata mashimo. Ndiposa migogoro ni sehemu ya maisha yetu! Mara nyingi **haiepukiki**, isipokuwa kuipitia na kupata suluhisho. Ipo migogoro baina ya ndugu ambayo huleta kutoelewana,kukosesha amani nahata pengine kupoteza kabisa mahusiano. Ni wazi kuwa mahali popote wanapoishi watu au kufanya kazi pamoja, hapakosekani migogoro kwani hata vikombe vinapokuwa kabatini, havikosi kugongana.

Ukweli ni kwamba sote tunazaliwa na tabia tofauti, uwezo tofauti wa kuvumilia na hata kuamua kutenda. Katika mazingira yoyote ya kutoelewana, kiasi kikubwa cha busara, upendo, amani na imani huhitajika ili kuiondoa migogoro hiyo. Isipotafutiwa suluhisho ama utatuzi wake ukatendeka kwa jazba na chuki, migogoro ya ndugu katika familia hukua na kuzaa madhara makubwa.

Kuanzia utotoni au hadi uzimani, kunaweza kuwa na sababu nyingi ambazo huweza kupelekea kuleta tofauti baina ya ndugu. Kwa ujumla, ndugu ni watu unaowaamini, ambao hawatakupa kisogo. Walakini, hii sio wakati wote. Kwa bahati mbaya ukweli umetuonyesha kuwa kuna uhusiano wa kindugu ambao huisha vibaya. Sababu kubwa zikiwa ni mazingira ambayo ndugu wameishi ambayo wakati mwingine kuna upendeleo wa mzazi kwa mtoto au watoto fulani na kuwafanya wengine wahisi wivu, kutopendwa na kutengwa.

Zipo sababu za kiuchumi ambapo ndugu wengine katika familia wanafanikiwa zaidi kuliko wengine na kuwa na maisha bora zaidi kuliko wengine. Hali hii pia inaweza kuleta mfarakano kwa wale ambao hali zao ni tofauti na wengine, hasa iwapo hakukuwa na mazingira ya utangamano katika familia tangu awali.

Ndugu wa familia moja huzaliwa wakiwa na tabia tofauti. Kila mshiriki wa familia ana **haiba** na mtazamo wake tofauti katika masuala mbalimbali. Wengine hukasirika mara kwa mara, wengine ni wakimya sana, wapo walio wakorofi na wengine wanaopenda amani, hivyo jambo hili ni muhimu mno kulielewa mara inapotokea migogoro ili kutamua namna ya kupata suluhisho.

Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba migogoro hii wakati mwingine hupelekea kuvuruga mwelekeo wa maisha ya watoto hasa wakati wa ukuaji, kwani kulingana na tofauti zao, wapo wale wanaoamua kuondoka nyumbani wakiwa bado na umri mdogo na kuhamia mitaani.

Pamoja na migogoro kuwepo katika familia zetu ni vyema wazazi ama walezi waelewe tofauti za kifamilia zinavyoweza kuchangia mfarakano baina ya ndugu wa familia moja. Kwamba mzazi ama mlezi anapompendelea mtoto mmoja na kutokuwa karibu na mwingine, anatengeneza

mazingira ya tofauti baina ya watoto wake. Ni vyema kuweka uwiano sawa baina ya watoto na familia ili kuweza kupunguza tofauti zinazoweza kujitokeza.

## MASWALI

**(a).**Onyesha athari **tatu** za migogoro miongoni mwa ndugu katika familia. **(Alama 3)**

**(b).** Eleza mambo **matano** yanayochangia kuwepo kwa watoto wanaorandaranda mitaani kwa kurejelea kifungu. **(Alama 5)**

**(c).** Malezi yanachangia migogoro baina ya ndugu. Thibitisha kwa kurejelea kifungu. (**alama. 1)**

**(d).** Taja na ueleze mbinu nne za kimtindo zilizotumika katika kifungu. **(alama. 4)**

**(e).** Andika visawe vya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. **(alama.2)**

**(i)** haiepukiki

**(ii).** haiba

## 2. MUHTASARI

*Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.*

Migongoni mwa starehe ambazo Waswahili wamezihifadhi mpaka leo ni kutoleana hadithi na kutegeana vitendawili. Starehe hizo ambazo kwa kawaida hufanywa nje huwa njiani au uani, ama ndani chumbani au ukumbini, aghalabu hufanywa wakati wa magharibi au usiku baada ya kila mtu kumaliza kazi ya nyumbani,dukani,shambani,ofisini na kadhalika. Mambo haya yakitazamwa sana itaonekana kuwa hayakufanywa vivi hivi.

Tangu zamani wazee wa Kiswahili waliwakataza wana wao kucheza mchana. Hawakupenda vijana wajizoeshe uvivu kwa kupiga malapa. Walisadiki kuwa mwana ambaye hakukanywa dhidi ya utiriri huu hangeweza kujifaa yeye mwenyewe na wala hata watu wengine. Isitoshe nani

Asiyejua kuwa ajizi ninyumba ya njaa:Vijana walilimizwa kusaidia katika makazi mbali mbali yanayofanywa majumbani, mashambani na mahali popote palipohisiwa kuwa mtu angalifanyiwa jambo la kumpa riziki. Ndiposa ungesikia wazee wakiwaambia watoto wao, ‘ukisimulia hadithi mchana utaota mkia’. Ingawa kwa watu wazima maneno haya yangekuwa masihara,kwa watoto yaliaminika sana kwa hivyo wazazi wakapata mradi wao. Hi ndiyo maana Waswahili wanasimuliana hadithi na kutegeana vitendawili jioni au usiku.

Wazazi ambao hawataki watoto wao watembeetembee au wacheze michezo ambayo itawafanya wakimbiekimbie na kujihasiri huwatia ndani ili wawe nao kuanzia magharibi. Waswahili wana itikadi nyingi zinazohusiana wakati wa magharibi. Ni ajabu kuwasikia wakisema kuwa magharibi

huwaleta pamoja na kutoleana hadithi. Na hata kama si hivyo hii ni fursa nzuri kwa wazazi kuzungumza na watoto wao ambao kutwa nzima huwa hawakupata nafasi kuwa nao.

Starehe hizi pia huongeza elimu, na kama wahenga wasemavyo, elimu ni mwanga uangazao.. Kwa mfano watoto watategewa vitendawili, jambo hili litawafanya wafikiri. Na kufikiri huku kutawafanya wavumbue mambo mengi ambayo mengine hapo awali hawakuyajua na kuyathamini. Vile vile huwafunza werevu wa kufumba na kufumbua mafumbo ambayo elimu inayohitaji kiwango kikubwa cha busara.

Kutoleana hadithi ni miongoni mwa starehe ambazo kwazo hujifunza mambo mengi sana. Katika hadithi watoto wanaweza kujifunza mambo yanayohusu mila na desturi, katika mambo haya watu hujifunza tabia nzuri, heshima na uvumilivu. Pia katika hadithi mtu anaweza kujifunza mambo ya historia na pia ya mazingira aliyoyazoea na hata mambo ambayo hayajui.

Aidha hadithi ni chombo ambacho wazee hukitumia kuwafundisha watoto mbinu za kuzungumzia. Wazee wenye busara aghalabu huwapa nafasi watoto wao wabuni na wasimulie hadithi zao. Wakati mwingine jamaa mbili jirani huweza kukutana kufanya mashindano ya kutambiana hadithi. Mazoezi kama haya huwawezesha vijana kufikia viwango vya juu vya ufasaha na matumizi ya lugha na ujasiri na ukakamavu wa kuweza kusema mbele za hadhira kubwa katika maisha yao. Baadhi ya watambaji wakubwa waliopata kusifiwa haikosi mwanzo wao ulikuwa wa namna hii. Hadithi pia huwafundisha watu kuhusu maisha duniani. Zinaweza kuwafunza jinsi ya kuishi na ndugu, majirani, marafiki, wake au waume. Ulimwenguni humu tunamoishi na mambo mengi yanoyomtatiza binadamu kwa namna mbalimbali. Hadithi zinaweza kupendekeza mambo ya kufanya na kuonyesha njia zenye mapato mema tunapofikiwa na hadhaa kadhaa. Zinaweza pia kukanya kiburi na kuonyesha faida ya kutosema uwongo ama kuishi katika maisha yasiyo muruwa, yaliyojaa kiburi na majivuno. Hapana shaka hadithi zinaweza kuongoza na kuwafanya wawe watiifu na raia wema katika nchi zao.

**Maswali**

**(a).** Kwa nini mwandishi akaoanisha utambaji wa hadithi na wakati wa jioni? (Maneno 40)

**(alama 5, alama 1 ya mtiririko)**

**Nakala chafu**

**Nakala safi**

**(b).** Kwa maneno kati ya 70 na 90 eleza umuhimu wa kutambiana hadithi na kutegeana vitendawili,kulingana na mwandishi. **( Alama 8, 1 ya mtiririko)**

**Nakala chafu**

**Nakala safi**

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

**(a).** Andika neno lenye kikwamizo sighuna cha ufizi, irabu ya mbele wastani, nazali ya midomo na irabu ya chini kati. **(alama 2)**

**(b).** Eleza muundo wa silabi katika neno mbilikimo. **(Alama1)**

**(c).** Andika upya kwa kutumia 'o'-rejeshi tamati.

Majarida ambayo yatasomwa yameagizwa **(alama. 1)**

**(d).** Tunga sentensi zifuatazo **(alama 2)**

**i)** Arifu

**ii)** Rai

**e)** Tunga sentensi moja yenye kiwakilishi cha A-unganifu,kitenzi kishirikishi kipungufu na kijalizo **(alama.2)**

**f)** Andika sentensi zifuatayo katika hali ya udogo **(Alama 2)**

Mbuzi wake amekaata kamba akaingia shambani na kula mahindi.

**g).** Andika katika usemi wa taarifa **(Alama 2)**

"Wanasiasa hawa wenu wakipigana hivi wataharibu nchi" Rais alisema.

h). Changanua sentensi kwa jedwali. **(alama.4)**

Jirani aliyenisaidia juzi ataondoka mwakani.

**i).** Onyesha yambwa katika sentensi ifuatayo

Alawi alifumiwa mkeka mzuri na shangaziye kwa miyaa. **(alama 3)**

**j).** Eleza tofauti ya kisarufi ya maneno yaliyopigia mstari (alama.2)

**i)** Duka la mwalimu limechomeka

**ii)** Duka la mwalimu limechomeka

**k).** Tunga sentensi kuonyesha wakati ujao, hali ya mazoea **(Alama 2)**

**l(I).** Tumia neno pongezi katika sentensi kama **(Alama 2)**

**i).** Nomino

**(ii).** Kihisishi

**m).** Eleza matumizi ya 'na' katika sentensi ifuatayo:Ridhaa na Mwangeka walikuwa wameketi karibu na jumba lakifahari walipoitwa na Apondi. **(alama.3)**

**n).** Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo

**(i).** Mwana mwadilifu huwaletea wazaziwe fahari. **(alama 1).**

*( Badilisha neno lililopigiwa mstari kuwa nomino.)*

**(ii).** Nyota nyingi ziliipamba anga usiku huo. **(alama 1)**

*(Tumia nomino ya jamii badala ya maneno yaliyopigiwa mstari)*

**(iii).** Makokha ni mkakamavua Onyango ni mkakamavu pia. **(alama 1)**

*(Unganisha iwe sentensi moja yenye kihusishi cha kulinganisha.)*

**(iv).** 'Kibali,nionyehse ulipoandika zoezi hilo.'Mwalimu alisema. (**alama.1)**

*(Tumia kiwakilishi nafasi badala ya nomino ya pekee.)*

**o).** Kwa kutunga sentensi, onyesha ngeli mbili za neno '**upwa**' **(alama.2).**

**p).** Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii. **(alama.2)**

Selume alimsimulia Ridhaa kisa chake.

**q).** Tunga sentensi moja kubainisha maana mbili za neno. **(alama.2)**

Kina

**r).** Rubani ni kwa ndege**,…….**ni kwa meli na**……....**ni kwa matwana. **(alama 2)**

## ISIMU JAMII (Alama 10)

Wewe ni mtaalamu wa maswala ya usalama. Umepewa fursa kuhutubia warsha inayojumuisha maafisa wa usalama kutoka katika vikosi mbalimbali kuhusu jukumu lao katika kudumisha usalama,amani na maridhiano nchini.

**(a).** Taja sajili ambayo utatumia kisha ueleze sababu ya jibu lako. **(alama 2)**

**(b).** Andika huku ukifafanua vipengele vinane vya kimtindo utakavyotumia kufanikisha mazungumzo yako. **(alama 8)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 6

# KISWAHILI

Paper 3

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO:**

*a) Jibu maswali manne pekee*
*b) Swali la kwanza ni la **lazima***
*c) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.*
*d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
*e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

## SEHEMU YA A: USHAIRI

### Swali la Lazima

**1.** ***Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata:***

**Shimo: Ali Salim Zakwany**

**1.** Mwambieni kibushuti, asiruke shimo lile
Kimo chake kama goti, kwenda ng'ambu sifikile
Mtu haoli bahati, akasahau umbile
Kila muwania mbele, na nyuma 'sisahawile

**2.** Afanyayo ni hatari, sijitie mpulele
Mambo yote ajasiri, shari asithibutile
Mjalia watu kheri, shairi ni yake vivile
Kila muwania mbele, na nyuma 'sisahawile

**3.** Asambe ndiyo busara, kutenda kitendo kile
Itamuwia hasara, na madhara kama yale
Mola mwingi wa subira, ajapo chomwa vidole
Kila muwania mbele, na nyuma 'sisahawile

**4.** Licha na yeye nyadungo, chuya katika mchele
Hata warefu ja pondo, hawatusi shimo lile
Walojaribu kitendo, shimoni watumbukile
Kila muwania mbele, na nyuma sisahawile

**5.** Nimefika kituoni, nasema mumuwasile
Mfua maji ngamani, ili kwamba sizamile
Chombo huungia mwambani, na nahodha ni yuyule
Kila muwania mbele, na nyuma 'sisahawile

### MASWALI

**a)** Lipe shairi hili kichwa mwafaka. **(alama 1)**
**b)** Fafanua toni ya shairi hili. **(alama 4)**
**c)** Taja na utoe mifano ya tamathali za usemi mbili zinazopatikana katika shairi. **(alama 4)**
**d)** Eleza umbo la shairi hili. **(alama 4)**
**e)** Kwa kutoa mifano minne, eleza aina moja ya idhini ya kishairi iliyotumika zaidi katika shairi. **(alama 3)**
**f)** Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari. **(alama 4)**

## SEHEMU YA B: RIWAYA – CHOZI LA HERI (ASSUMPTA MATEI)

**2.** "Jua linalochomoza halina ule wekundu wa jua la matlai ambao huleta haiba ya uzawa wa siku yenye matumaini. Naona wingu kubwa angani likitembea kwa kedi na madaha na kulifunika jua..... Mawingu yaliyoshiba yakataka kutapika yanagooka, yanakaribiana, kupigana busu na kusababisha mwanguko wa matone mazito ya mvua..."

**(i)** Eleza aina za taswira zinazojitokeza katika dondoo hili **(alama 8)**
**(ii)** Eleza mbinu nyingine ya kimtindo inayojitokeza katika dondoo hili. **(alama 2)**
**(iii)** Eleza sifa na umuhimu wa msimulizi wa dondoo hili. **(alama 10)**

**3.** Lakini itakuwaje 'historical injustice' nawe Ridhaa hapo ulipo sicho kitovu?
**(i)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
**(ii)** Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. **(alama 2)**
**(iii)** Eleza sifa nne za mzungumzaji wa maneno haya. **(alama 8)**
**(iv)** Eleza mambo matatu yaliyowakumba walioishi penye kitovu kisicho chao. **(alama 6)**

## SEHEMU YA C: TAMTHILIA - BEMBEA YA MAISHA (Timothy Arege)

4. Ukirejelea Anwani ya Tamthilia ya Bembea ya Maisha, onyesha namna wahusika wanavyobembea maishani mwao. **(alama 20)**

**5.** Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kuwa mchezo kumbe ilikuwa kweli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silezi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. Siku hazigandi wala jana hairudi. Sasa jana imebaki kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika."

**a)** Yaweke maneno haya katika muktadha wake **(alama 4)**
**b)** Eleza kwa mfano mbinu nne za kimtindo zilizotumika **(alama 4)**
**c)** Barusha toni katika dondoo hili. **(alama 2)**
**d)** Ni maudhui gani yanayojitokeza katika dondoo hili? **(alama 4)**
**e)** Onyesha sifa za mzungumzaji zinazodhihirisha kuwa silezi zao hawakuzila kwa furaha. **(alama 6)**

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI - MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI ZINGINE.**

**6.** (a) Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo lifuatalo. **(alama 6)**

"Jimbo la matopeni lilikuwa limegeuzwa ngome ya watu fulani binafsi. Watu wenye ushawishi mkubwa serikalini! Watu wasiojali maisha ya wapiga kura kama Machoka na Zuhura. Wapiga kura walioamka siku hiyo asubuhi ya majogoo, wakastahimili baridi kali ya bukrata. Wakavumilia jua kali la mchana. Zuhura alikumbuka namna yeye na wenzake walivyotunga foleni ndefu kwenye vituo vya kupigia kura. Yote haya wakiwa na matumaini ya maisha bora ya baadaye, si bora maisha! Kumbe wajinga ndio waliwao! Mzigo mzito wa maisha haukuwatisha wala kuwakosesha usingizi viongozi wao. Ama kweli, mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi. "

**(b)** Onyesha namna wanamatopeni wanavyokumbwa na madhila kwa kurejelea hadithi ya "Msiba wa kujitakia" **(alama 14)**

**7.** "Katika hali ile ya uchungu, kilio na mtanziko wa mawazo, akaiona simu yake imeanguka chini ya kitanda….. Haidhuru hata kama atamuunga mkono mwanawe."

**(i)** Eleza muktadha wa maneno haya. **(alama 4)**

**(ii)** Fafanua mbinu ya kimtindo inayojitokeza katika dondoo hili. **(alama 2)**

**(iii)** Eleza sifa nne za anayerejelewa katika dondoo hili. **(alama 4)**

**(iv)** Eleza jinsi "taasubi ya kiume" inavyoshughulikiwa na mwandishi wa "fadhila za punda". **(alama 10)**

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**8.** Ewe Mainga wa Ndumi
Siwe uloambia akina mama
Siku tulopiga foleni
Chakula cha msaada kupata
Turudishe vifaranga kwenye miji
Wageuke vijusi tena
Njaa isiwaangamize?

Siwe ulopita
Matusi ukitema
Chumvi na sukari kuturushia ja samadi?
Uhitaji wetu ukatutuma
Kuokota vihela uloturushia
Ukatununua, kura ukapata?

Sasa miaka mitano imetimia
Waja tulaghai tena
Mainga wa Ndumi huna lolote safari hii
Ubunge umekudondoka ukitazama
Wanyonge tumeamua
Kwingine kujaribu.

## MASWALI

**a)** Eleza aina ya kipera hiki. **(alama 2)**
**b)** Huku ukitoa mifano, tambua mbinu za lugha nne zilizotumiwa katika utungo huu. **(alama 8)**
**c)** Tambua nafsineni katika utungo huu. **(alama 2)**
**d)** Fafanua toni ya utengo huu. **(alama 2)**
**e)** Fafanua umuhimu wa kipera hiki. **(alama 6)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 7

# KISWAHILI

Paper 1

**Time: 1¾ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

## *Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

(a) *Andika Insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima.*

*(b) Kisha chagua Insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*

*(c) Kila Insha isipungue maneno 400.*

*(d) Kila Insha ina alama 20.*

*(e) Kila Insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

*(f) Karatasi hii ina kurasa 2 zilizopigwa chapa.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**1. LAZIMA**

Mwandikie barua mhariri wa Gazeti la Baraka ukimweleza sababu za watoto wengi katika kaunti yako kuacha shule na kujiingiza katika ajira za mapema.

**2.** Vipakatalishi vimeleta manufaa mengi nchini .

Fafanua.

**3.** Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali:

Mcheka kilema hafi bila kumpata.

**4.** Andika kisa kitakachoanzia kwa maneno yafuatayo:

Kushoto kulikuwa na jitu la miraba minne ambalo lilitema cheche za matusi ungedhania ni karakana **…**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 7

# KISWAHILI

Paper 2

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

## *Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

1. *Andika jina lako, shule na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
2. *Andika tarehe ya mtihani na utie sahihi yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
3. *Jibu maswali yote.*
4. *Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa baada ya kila swali katika kijitabu hiki cha maswali.*
5. *Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 UFAHAMU | 15 | |
| 2 UFUPISHO | 15 | |
| 3 MATUMIZI YA LUGHA | 40 | |
| 4 ISIMU JAMII | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

**SEHEMU YA A: UFAHAMU** **(alama 15)**

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali***

"Swala la idadi kubwa ya watoto wadogo wanaoendelea kumiminika mijini na kuonekana wakiranaranda mijini ovyo,halijapewa umuhimu wowote wa haja na serikali za nchi nyingi,licha ya mijadala katika warsha anuwai,zilizofanyika kujadili swala hili nyeti.

Kwa kutokuwa na sheria ama sera iliyo wazi kuhusu haki na usalama wa watoto,sarikali zetu hazina budi kukubali kubeba uzito wote wa lawama. Hii ni kwa sababu, serikali zetu zimelipuuza na kuvalia miwani swala hili kwa kuchukulia kuwa litapotea lenyewe katika hewa yabisi. Yafaa ifahamike kuwa usalama wetu katika siku zijazo utategemea jinsi tutakavyolikabili ana kwa ana tatizo hili wakati huu. Wakati wa kutenda ni sasa. Aidha, watoto hawa wanaokulia mitaani bila malezi,maelekezo wala mwongozo mwafaka wa kimaisha, wanakua bila mapenzi hivyo hawajui maana ya kupenda. Wanachokijua ni chuki na haja ya kulipiza kisasi didhi ya jamii iliyowachonga jinsi walivyo. Hawajali lolote hata kifo. Wako tayari kujikabidhi kwa haini yeyote mwenye nia mbaya,bila kujali matokeo, muradi tu, wapate riziki.

Tunapendekeza kwa serikali, washika dau kama vile mashirika ya kujitolea, viongozi wa dini, shule, vyuo na wananchi kwa jumla wachange bia katika kutafuta mikakati ya kulitatua tatizo hili kabla halijageuka kuwa janga la kijamii ambalo tutashindwa kulimudu. Mpango wa vijana hawa kujiunga na huduma ya taifa ni jambo linalofaa kutiliwa maanani.

Tunapendekeza makao Zaidi ya watoto wanaozurura mijini yajengwe ambapo watapata mafunzo ya kiufundi yatakayowawezesha kujitegemea maishani. Badala ya kulitegea mgongo swala hili, serikali zinawajibika kuwasajili hawa watoto ili waweze kuunganishwa na familia na koo zao. Utafiti uliofanywa na wataalamu wa Elimu jamii umebainisha kuwa ni asilimia kumi tu ya watoto hawa wa mitaani wasiokuwa na mahali wawezapo kupaita nyumbani. Asilimia tisini iliyobaki, angalau wana mahali wanapoweza kupaita nyumbani ilhali wanaendelea kuwa mitaani. Wazazi tumesahau wajibu wetu. Wengi wetu tumelikimbia jukumu la ulezi tulilopewa na muumba. Hawa waliojipaka masizi mwilin mzima, wanaozurura ovyo mitaani, si matokeo ya maumbile;hawakuja duniani kwa sadfa, hawakuulizwa wala kushauriwa. Makosa ni yetu wazazi. Tuliwaleta hapa duniani, kisha tukawakimbia.Hatutasamehewa duniani na akhera.

Mwenye njaa hana miiko. Ili kijiruzuku, hawa watoto daima wanachumia jaani.Kwa kudura ya jalia, huenda siku moja watalia kivulini. Asiyekuwa na wake ana mungu.Aghalabu, watoto wanaozurura mitaani hupewa pesa na wafadhili. Wakati mwingine wanaiba. Maisha haya ya kuomba au kuiba wanaona yanaridhisha Zaidi kuliko kumenyeka na kazi ya kibarua kutwa kucha. Kwa bahati mbaya, watoto hawa wamatumia pesa wanazopata kutoka kwa wafadhili kujichimbia kaburi. Aidha pesa wanazopatiwa watoto hawa wanazitumia kununulia gundi badala ya chakula. Wafadhili wanashauriwa wawape chakula hawa watoto badala ya pesa taslimu. Kusema kweli, unapompa mtoto wa mitaani pesa,utakuwa unainua biashara ya mwenye kiwanda cha gundi,jambo ambalo litakuwa sawa na kuweka sahihi mkataba wa kifo cha mtoto mwenyewe.

Wataalamu wa afya wanaonya kuwa gundi ikivutwa kwa muda mrefu inaweza kusababisha upofu au kifo.Wataalamu hawa wanazidi kutuarifu kuwa matumizi ya muda mrefu ya gundi huathiri ubongo,figo na maini. Mtumiaji pia anaweza kupoteza uwezo wa kutembea na hata kupooza kabisa.

Sababu wanazotoa hawa watoto ni kwamba, uvutaji gundi,huwaondolea njaa,baridi ya usiku na kuwatuliza mawazo. Ni jambo la kusikitisha kwamba tunaendelea kushuhudia bila kujali hawa watoto ambao ni kiungo cha jamii yetu,wakijiangamiza. Wananchi kwa ujumla hawaha budi kuhamasishwa dhidhi ya athari ya matumizi ya gundi.Wafanya biashara wanaowauzia watoto hawa gundi yafaa wakome,la sivyo wachukuliwe hatua.Kutolitatua tatizo hili la watoto wa mitaani hivi sasa,kutapeleka kuwako kwa kizazi cha mitaani ambacho kitazaliwa mitaani,kulelewa mitaani,kuoa mitaani na kufia mitaani.Kadiri mataifa yanavyoendelea kujitia hamnazo kuhusiana na swala hili,ndivyo tunavyokubalia jinai itawale,sasa na wakati ujao.

Hawa watoto watakapokua,watageuka kuwa wapigaji watu kabari,majambazi,wezi wa kutumia nguvu ama watatumiwa na mahaini kutimiza uhaini wao.Hawa watoto wenye njaa,watalazimika hatimaye,kuwatoa wenywe shibe tonge mdomoni.Matokeo ya hali hii ni kwamba katika siku zijazo,hawa ndio watu watakaotunyima starehe ya kulala unono.Watatuchafya mitaani,majumbani,vijijini na kutuvizia mabarabarani.Tuna sababu nzuri ya kutiwa hofu na tatizo hili,kwani jinsi kizazi kinavyozidi kupanuka,inaonekana tumelitega bomu ambalo litakuja kutulipukia usoni mwetu.”

**Maswali**

**(a)** Taja jambo moja linalochangia kuweko kwa watoto wanaorandaranda mitaani. **(alama 1)**

**(b)** Maisha ya mitaani huathirije watoto? **( alama 3)**

(c) Tatizo la watoto wanaorandaranda mitaani laweza kutatuliwaje? **(alama 3)**

(d) Eleza maana ya: **(alama 2)**

**i.** Hawa watoto wanachumia jaani

**ii.** Jinsi kizazi cha mitaani kinavyozidi kupanuka,inaonekana tumelitega bomu ambalo litakuja kutulipukia usoni mwetu. **(alama 2)**

**iii.** Mwenye njaa hana miiko. **(alama 2)**

**(e)** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye taaria: **(alama 2)**

i. Aidha: ii.Gundi:

## 2.**UFUPISHO:(ALAMA 15)**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo***

Lugha ndio msingi wa maandishi yote. Bila lugha hakuna maandishi. Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha husitawisha ufahamu wetu wa mambo tusomayo. Mazoezi katika kuandika husitawisha ufahamu katika kusoma kwa sababu katika kuandika ni lazima kuyatumia maneno vizuri na kufahamu ugumu wa usemi. Twajifunza matumizi ya lugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine wakizungumza. Lugha tusomayo ni anina ya lugha ya masungumzo.

Kuna ujuzi mwingi katika kuzungumza kama vila michezo ya kuigiza, hotuba, majadiliano na mazungumzo katika darasa. Haya yote husaidia katika uhodari wa matumizi ya lugha. Ujuzi wa kila siku utasaidia katika maendeleo ya kusoma na usitawi wa msamiati. Ikiwa mwanafunzi amemwona ndovu hasa, atakuwa amejua maana ya neno ndovu vizuri zaidi kuliko mwanafunzi ambaye hajawahi kumwona ndovu bali ameelezwa tu vile ilivyo. Vilevile ujuzi wa kujionea sinema au michoro husaidia sana katika yaliyoandikwa. Ikiwa mwanafunzi ana huzuni au ana furaha, akiwa mgonjwa au amechoka au amefiwa, haya yote ni ujuzi. Wakati juao mwanafunzi asomapo juu ya mtu ambae amepatikana na mambo kama huyo hana budi kufahamu zaidi.

Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabuni. Hata hivyo, lugha zote hazina usitawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi. Fauka ya hayo , karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu kwenye lugha nyingine.

Inambidi mwanafunzi asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma tu juu ya taaluma fulani anayojifunza . Inafaa asome juu ya michezo, mambo ya mashairi na juu ya mahali mbalimbali ili kupata ujuzi wa mambo mengi.

**a)** Fupisha aya za kwanza mbili kwa kutumia maneno 65 (alama 10, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

b) Kwa kuzingatia habari zote muhimu na bila kupoteza maana asilia, fupisha aya ya mwisho (Maneno 30) (alama 5 utiririko)

Matayarisho

**Jibu**

## MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**(a)** Toa mifano miwili miwili **ya** **(al.2)**

i. Sauti ghuna ambazo ni vipasuo ……..……..

ii. Sauti sighuna ambazo ni vikwamizo ……..……

**(b)** Onyesha mofimu katika neno Aliyemcha **(al.2)**

**(c)** Andika sentensi yenye muundo ufuatao **(al.2)**

KN(W+V) + KT (t +RH)

**(d)** Tumia neno shirika kama nomino na kama kielezi katika kutunga sentensi moja **(al.2)**

**(e)** Kwa kutunga sentensi vumisha nomino nguruwe kuwa kivumishi cha idadi bainifu. **(al.1)**

**(f)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya **kutendewa** **(al.1)**

Mtoto wa waziri amekufa

**(g)** Yakinisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu wingi **(al.2)**

Msomi hakutuzwa siku hiyo

**(h)** Tunga sentensi moja inayobainisha maana mbili tofauti za neno chuma **(al.2)**

**(i)** Tambua kiima na aina za yambwa katika sentensi ifuatayo**.** **(al.4)**

Mwalimu mkuu hupigiwa nguo pasi na Maria

**(j)** Kwa kutumia mifano mwafaka fafanua miundo yoyote miwili ya kirai nomino **(al.2)**

**(k)** Andika sentensi ifuatayo kwa **wingi** **(al.2)**

Mgeni huyo na mwingine walikula wali kwa uma

**(l)** Andika neno lenye silabi funge yenye muundo wa konsonanti moja **(al.1)**

**(m)** Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika udogo **wingi** **(al.2)**

Ng'ombe wangu ana ndama mdogo

(n) Tunga sentensi zenye mipangilio ifuatayo**;** **(al.4)**

**i.** Kishazi tegemezi na kishazi huru

**ii.** Kishazi tegemezi na kishazi tegemezi

(o) Eleza matumizi ya 'ki' katika sentensi ifuatayo**:** **(al.3)**

Nyamunga na kitoto wamekuwa wakila, wakiimba kikasuku

**(p)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mchoro wa matawi**.** **(al.4)**

Mtoto wa mjomba alikuja kwetu nyumbani jana

**(q)** Andika kwa msemo wa taarifa**.** **(al.2)**

'Yafaa tumwendee mama mkubwa ili atushauri juu ya jambo hili,' Amina alipendekeza.

(r) Andika kinyume cha: **(al.1)**

Chakula hiki kitamu nitakimeza

**(s)** Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatavyo**.** **(al.2)**

**(i)** Kiwakilishi nafsi huru

**(ii)** Kiwakilishi nafsi kiambata

## 4. ISIMUJAMII (alama10)

**(a)Tofautisha** kati ya kuhamisha msimbo na kuchanganya msimbo. **(alama 2)**

**(b)Taja** mambo mawili yanayochangia katika uhamishaji msimbo. **(alama 2)**

**(c )**Taja kaida mbili zinazotawala maamkizi katika jamii huku ukitoa mifano mwafaka.**(alama2)**

**(d)** Fananisha sifa zozote nne za sajili ya maabadini na mahakamani. **(alama 4)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 7

# KISWAHILI

Paper 3

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

## *Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

*(a) Jibu maswali manne pekee.*
*(b) Swali la kwanza ni la lazima.*
*(c) Maswali mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu zilizosalia yaani.*
*(d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
*(e) Kila swali lina alama ishirini (20)*
*(f) Majibu yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

## SEHEMU YA A: TAMTHILIA

**Timothy Arege; Bembea ya Maisha**

***1. Lazima***

Eleza ufaafu wa anwani **Bembea ya Maisha** katika tamthilia ya **Bembea ya Maisha (ala 20)**

## SEHEMU YA B

**RIWAYA: CHOZI LA HERI**

*(Assumpta K. Matei)*

Jibu swali la Pili au la Tatu

**2.** "Watu husema kuwa binadamu hawawi sawa ila kifoni…"

a) Eleza muktadha wa maneno haya. **(alalama 4)**

b) Tambua mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. **(alama 2)**

c) Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji wa maneno haya. **(alama 6)**

d) Thibitisha kuwa hakuna usawa baina ya wanadamu. **(alama 8)**

**Au**

**3.** Jadili nafasi ya sehemu zifuatazo katika riwaya ya Chozi la Hari:

(a) Hotuba **(alama 10)**

(b) Uozo katika jamii **(alama 10)**

## SEHEMU C

### HADITHI FUPI

**Mapambazuko ya Machweo**

**4.** "...iwapo penzi hili litatia doa, basi nirudishie mfuko huu kama ishara ya kulitupa penzi langu kama jongoo na mti wake...

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

**b)** Fafanua mbinu mbili ambazo zimetumika katika dondoo hili. **(ala 4)**

**c)** Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. **(alama 6)**

**d)** EIeza umuhimu wa msemewa wa hadithi hii katika kujenga ploti. **(al 6)**

**5.** Kwa kurejelea hadithi ya **Ahadi ni Deni**, fafanua namna Uwajibikaji umejitokeza. **(alama 20)**

**SEHEMU YA D USHAIRI**

*Jibu swali 6 au 7*

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Daima alfajiri na mapema
Hunipitia na jembe na kotama
Katika njia iendayo kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani;
Nimuonapo huwa anatabasamu
Kama mtu aliye na kubwa hamu
Kushika mpini na kutokwa jasho
Ili kujikimu kupata malisho.
Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotumbuiza
Utadhani huwa vimemngojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia;
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimletea
Nao umande kumbusu miguu;
Ni miti yote hujipinda migongo
Kumpapasa, kumtoa matongo;
Na yeye kuendelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua
Akichekelea ha ha ha ha ha ha ha …
Na mimi kubaki kujiuliza
Kuna siri gani inayomliwaza?
Au ni kujua au kutojua?
Furaha ya mtu ni furaha gani
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao
Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonga roho
Ayalimia matumbo ya waroho;
Kuna jambo gani linamridhisha?
Kama si kujua ni kutokujua
Laiti angalijua, laiti angalijua!

(a)Eleza matatizo manne yanayompata mzungumziwa. **(Alama 4)**
(b)Eleza mtindo wa lugha uliotumiwa na mshairi na utoe mifano. **(Alama 8)**
(c)Taja nafsineni katika shairi hili. **(Alama 1)**

(d)Eleza toni ya shairi hili. **(Alama 1 )**
(e)Taja mbinu mbili za uhuru wa kishairi uliotumika na utoe mifano. **( Alama 2)**
(f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. **(Alama 4)**

**(7)*Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Leo kitaka nifike, natamani, ila wauma mwili
Kwa kazi nihusike, samahani, unahiliki mwili
Napenda nihesabike, makundini, ila huwezi mwili
Vitisho pamwe kelele, ninavicha, kwa nafsi na mwili
Ila ugonjwa utimile, umechacha, na kuudhili mwili
Msikose simile, magalacha, si gurudumu mwili.
Vingekuwepop viraka, kuutia, ngeushuruti mwili
Kifundi kivipachika, kuingia, hata kuridhi mwili
Upya ukaungilika, kuvutia, roho na wake mwili.
Lakini kamwe haiwi, kuvipata, vipande vyake mwili
Sihofu kupata mawi, sitajua, kupigania mwili
Hata kufutwa sikawi, nitakita, kidete nao mwili.
Kazi ninaithamini, ni hakika, akilini na mwili
Ila kamwe siamini, kusagika, damu, jasho na mwili
Uwele hususani, kioneka, nguvu hitishi mwili.

(a)Liweke shairi hili katika bahari tatu. **(Alama 3)**
(b)Eleza dhamira ya mshairi. **(Alama 2)**
(c) Eleza muundo wa shairi hili. **(Alama 4)**
(d) Toa mifano ya uhuru wa kishairi uliotumika. **( Alama 4)**
(e)Eleza kwa kifupi maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. **(Alama 3)**
(f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. **(Alama 4)**

## SEHEMU D
## FASIHI SIMULIZI

A(i) Miviga ni nini? **(Alama 2)**
(ii) Eleza sifa nane za miviga. **(Alama 8)**
B (i) Ulumbi ni nini? **(Alama 2)**
(ii)Eleza sifa nane za ulumbi **(Alama 8)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 8

# KISWAHILI

Paper 1

**Time: 1¾ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

**a)** Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

**b)** Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

**c)** *Andika insha mbili. Swali la **kwanza** ni la lazima.*
**d)** *Kisha chagua insha nyingine moja kutoka kwa hizo tatu zilizobakia.*
**e)** *Kila insha isipungue maneno 400.*

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| | Jumla 40 | |

## MASWALI

**1.** Wewe kama msimamizi wa mifumo ya elimu umealikwa na mwandishi wa habari ili kuhojiwa kuhusu changamoto zinazokumba mfumo mpya wa elimu ya umilisi. Andika mahojiano hayo.

**2.** Serikali za majimbo zitawafaa wananchi wote. Fafanua.

**3.** Mchagua nazi hupata koroma. Thibitisha ukweli wa methali hii.

**4.** Anza insha kwa maneno haya; Nilizinduka jimbi la kwanza na kujiandaa kwenda katika hafla**…….**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 8

# KISWAHILI

Paper 2

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***b)*** *Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***c)*** *Jibu maswali yote*

***d)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*

***e)*** *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE:**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

## 1. UFAHAMU

*Soma makala yafuatayo kisha utekeleze maagizo yafuatayo*

Utotoni niliamini kwamba kusoma ndiko ufunguo wa kila kitu ulimwenguni kwa jinsi kunavyoonekana kuwatoa watu katika uzuzu, ukata na ugonjwa: na kuweka kwenye maisha bora ya mwangaza wa kujua kusoma na kuandika, utajiri wa kuweza kuvaa hata suti ya vipande vitatu, na kuwa na afya ya kuonekana kwa kitambi. Hizo ni zamani zile ambapo shule ya vidudu haikuwa sharti la mtoto kukubaliwa katika darasa la kwanza. Mtoto angelisha au kusaidia kwa kazi za nyumbani mpaka kufika umri labda wa miaka kumi kisha, kufumba na kufumbua, afisa wa serikali angeonekana akishauriana na mzazi wa mtoto. Matokeo yangekuwa mtoto huyo kuanza safari ndefu ya kila siku, apate asipate chakula.

Mimi kwa upande wangu sikujali maisha pata-nenda shule, kosa – bado – nenda – shule. Sikujali kero za baridi kali wala karaha za vua la asubuhi. Kuanzia utotoni *niliwahusudu* wenzangu waliokuwa wakirauka kiasi cha kufikiriwa kuwa walilala kwa shati na kaptula zao, au kwa blauzi na skati na kaptula zao. Nilipendezwa na yunifomu zao nikatamani na hata kuapa kwamba siku moja nitavaa kama wao na kutembea kwa maringo kama wao. Zaidi nilitamani kufika walikokuwa wakienda na kufanya walivyokuwa wakifanya huko.

Penye nia hapakosi njia. Nia yangu ilidhihirika pale nilipojiunga na darasa la kwanza. Darasa la kwanza lilinisoma kisogo baada ya siku mbili tu. Nalo la pili likanipungia mkono baada ya juma moja. Miaka mitano baadaye nilikutana na kiunzi cha kwanza kwenye mtihani wa kitaifa wa chumba cha saba uliokuwa kifungua mlango wa kuingilia kidato cha kwanza.

Baada ya miaka minne nilikutana na mlango funge mwingine ambapo nilibisha na ukanifungukia kwa *kutia fora* katika mtihani wa kiwango cha elimu ya upili. Katika miaka miwili iliyofuatia nilijiunga na shule maarufu ya kitaifa siku hizo.

Masomo hayakuendelea kuwa mteremko kwangu kwani uchechefu wa karo na masurufu ulimaanisha kuwa siku nyingi nilikuwa nje ya kuta za darasa letu. Hata ivyo *nilijifunga masombo.*Hatimaye nilifunguliwa milango ya kuingia ndaki.

Baada ya kuhitimu kwa shahada ya kimsingi ya uzamili, kisha uzamifu au udaktari falsafa hatimaye, nilifanywa meneja kufikia leo. Hata nikiwa ukubwani bado ninazidi kusoma na kutafiti ili nisiote ukurutu wa akili.

Cheo na madaraka haya ya umeneja yamaanisha kila siku nivae suti kamili na shati nyeupe pe, ambayo shingoni imeambatanishwa na kipande maalumu cha kitambaa kinacholewalewa kifuani. Nijiangaliapo kiooni hujifananisha na mtu ambaye amejitia kitanzi shingoni.

Nina kitambi ambacho labda ni *taashira* ya utajiri. Hata hivyo ingawa mimi si tajiri mwenye sauti kubwa kiuchumi, ninaweza kujivunia elimu yangu iliyoniwezesha kujimudu kidogo maishani. Sasa nina shamba langu mwenyewe, nyumba yangu mwenyewe ambayo imejaa mali yangu mwenyewe. Nina redio yangu mwenyewe, rununu yangu mwenyewe na wanyama wangu mwenyewe.

Lakini mwenzangu ambaye zilimwishia ukingoni katika shule za nasari, hana elimu, pesa wala mahali pa kuzikiwa wakati mpira utakapomwia mwingi.

## MASWALI

**a)** Eleza imani ya mwandishi kuhusu elimu. **(alama 3)**

**b)** Taja dhiki zilizomkabili mwandishi alipokuwa **shuleni** **(alama 2)**

**c)** Onyesha uhusiano uliopo kati ya elimu, kazi na ukwasi kwa mujibu wa habari hii. **(alama 3)**

**d)** Ukirejelea makala haya, fafanua msemo, 'elimu ni bahari haina kikomo' **(alama 3)**

**e)** Hatima ya wale ambao hawakupata elimu ni ipi? **(alama 2)**

**f.** Badala ya maneno yafuatayo mwandishi angetumia msamiati gani? **(alama 3)**

**i.** Niliwahusudu……

**ii.** Ndaki……..…

**iii.** Taashira……..

## 2. UFUPISHO

Dhuluma kwa wanawake sio matokeo ya siasa baada ya uhuru, bali ni matokeo ya hali iliyokuwepo tangu enzi za mababu zetu; kabla ya ukoloni. Kubaguliwa na kudhulumiwa kwa wanawake kisiasa kunaoana na kunyonywa kwake kijamii kunakoshuhudiwa siku nenda miaka rudi.

Elimu ya jadi ilimwandaa mwanamke kuwa chombo kitiifu cha mwanamume. Mwanamke aliandaliwa katika unyago na katika mfumo mzima wa malezi kuwa chombo cha kutumikia mwanamume-kumstarehesha, kumfariji, kumlisha na kumzalia watoto. Mwanamke tangu jadi hakuruhusiwa kushiriki katika shughuli za kisiasa na utawala wala hakuna mtu aliyeamini kwamba mwanmke angeweza kushikilia wadhifa wowote wa uongozi.

Demokrasia ya jadi naihusudu sana; ambapo wazee walikaa chini ya mbuyu na kuamua mambo ya jumuiya. Mahakama ya kijiji ilikuwa aghalabu ni ya wazee na na wanaume peke yao. Hakukuwa na mwanamke aliyeshirikishwa, hata kama alikuwa ajuza. Sifa waliyokuwa nayo wanawake ni ile ya usihiri na uganga. Mwanamke yeyote ailiyezeeka alidhaniwa kuwa bingwa wa uchawi, ulozi na ushirikina. Kwa hivyo, wanawake ndio waliokuwa washirikina wakubwa, maana fursa ya kupata elimu pana zaidi hawakuwa nayo. Si ajabu kuwa mwanamke alipojitokeza na kusema jambo la busara, alipuuzwa na pengine kutukanwa hadharani.

Kwa bahati nzuri, kumezuka mwamko uliotuingiza katika enzi mpya. Vita vya wanawake vya kujihami na kujiendeleza katika ulimwengu unaotawaliwa na wanaume vimetapakaa kote katika

kila sehemu ya dunia. Wanawake wengi wamekiuka misingi na miziz ya utamanduni na kung'oa asasi za kijamii na itikadi ambazo daima zimeendelea kumyanyasa na kumuumbua utu mwanamke tangu jadi. Watetezi wa haki za wanawake zamani walilaumu suala la serikali za mataifa mwaka hadi mwaka. Huku masuala ya wanawake ya kijamii, utu na utamaduni yakishangiliwa kupitishwa, watetezi wameeleza wasiwasi wao ikiwa kupitishwa kwa maazimio kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka kwa wanawake kimataifa au katika nchi moja. Fauka ya hayo, baadhi ya wachunguzi wanaonelea kuwa maazimio mengi hayadokezi hatua za kufikiwa haki za wanawake.

Maazimio mengine yanazungumzia juu ya kuondolewa kwa ubaguzi dhidi ya wanawake, kushiriki kwao katika uendelezaji wa amani ya kimataifa na ushirikiano wa kimataifa, majukumu yao katika jamii, mfuko wa Umoja wa Mataifa wa wanawake (Unifem) na kuimarisha hadhi ya wanawake katika sekretariati ya Umoja wa Mataifa miongoni mwa shughuli nyingine katika mkabala huu.

Wanawake wameonyesha vipaji vyao katika nyanja mbalimbali za maisha; siasa, uchumi, utawala na kadhalika. Wanawake wamejikakamua na kudhihirisha kuwa wao pia wana jukumu muhimu la kutekeleza ili kuyaongoza maisha yao naya watu wengi. Wadumishaji wa dhuluma za kijinsia hawana budi kusalimu amri na kuukubali ukweli huu, wapende wasipende. Mtazamo juu ya haki sawa unatokana na kukubaliwa na kuondolewa kwa aina zote za ubaya dhidi ya wanwake wanojitolea mhanga kutetea hadhi yao pamoja naya wanyonge wengine. Wao huonekana kama waasi, wapinga mila na watovu wa utii.

## MASWALI

**a)** Bila kubadilisha maana asilia, fupisha aya tatu za kwanza. (Maneno 45-55) **(Alama 6)**

**Matayarisho**

Jibu.

**b)** Kwa kurejelea aya tatu za mwisho, pambanua hoja muhimu zinazoguziwa na mwandishi. (Maneno 60-65) **(Alama 9)**

Matayarisho

**Jibu**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

**a)** Tofautisha Irabu /u/ na /o/ **(Alama 2)**

**b)** Tunga sentensi ili kubaini matumizi ya neno vibaya katika sentensi kama;
kielezi na kivumishi **(Alama 2)**

kielezi

Kivumishi

**c)** Yakinisha sentensi ifuatayo.

Nisipomwona sitamlipa pesa zake. **(Alama 1)**

**d)** Tumia kivumishi cha 'a' unganifu katika sentensi ukitumia nomino katika ngeli ya A-WA. **(Alama 2)**

**e)** Tunga sentensi ili kutofautisha vitenzi vifuatavyo.

**i)** ni **(Alama 1)**

**ii)** yamekuwa **(Alama 1)**

**f)** Tunga sentensi ili kubaini; **(Alama 2)**

kivumishi cha idadi jumla

kivumishi cha idadi kamili

**g)** Toa maana mbili ya sentensi hii

Nionyeshe vile nitakavyobeba. **(Alama 2)**

**h)** Kanusha sentensi ifuatayo kwa njia mbili .

Wachezaji walikuwa wanafanya mazoezi. **(Alama 2)**

**a**……

**b**……

**i)** Andika katika usemi wa taarifa.

"Tutakwenda kanisani kesho kutwa." Kame alisema. **(Alama 2)**

**j)** Changanua sentensi hii kwa kutumia kielezo jedwali. **(Alama 4)**

"Mshale huu mrefu umevunjika mara mbili

**k)** Tunga sentensi mbili tofauti ili kudhihirisha matumizi ya 'mshazari' **(Alama 2)**

**l)** Unganisha sentensi hii kwa kutumia kirejeshi 'O' Kucha zake ni ndefu. Kucha zimekatwa. **(Al 1)**

**m)** Eleza matumizi ya 'Ki' katika sentensi

Ukirusha kipira kitapotea **(Alama 3)**

**n)** Tunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizoonyeshwa. **(Alama 2)**

**i)** La (kutendeshana).

**ii)** Pa (kutendesha).

**o)** Andika neno lenye kiyeyusho. **(Alama 2)**

p) Andika kwa wingi

Mtoto yuyu huyu ndiye aliyeiba nguo yangu. **(Alama 1)**

**q)** Unda sentensi yenye vijenzi vifuatavyo vya kisarufi.

Kiwakilishi + kivumishi + kitenzi + kielezi **(Alama 1)**

**r)** Akifisha sentensi ifuatayo ;

Bw. Juma alimwambia bibi yake nitakutuza ukiendelea kutenda mazuri. **(Alama 2)**

**s.** Tunga sentensi mbili ili kuonyesha tofauti kati ya maneno yafuatayo; **(alama 2)**

**i.** kua

**ii.** kuwa

**t.** Tunga sentensi moja yenye virai viuatavyo. **(alama 2)**

RN (nomino, kivumishi kielezi), RT (kitenzi, nomino)

**u.** Andika katika udogo. Kitabu cha mtu huyo kimeletwa na mwanafunzi wake. **(alama 1)**

## 4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

**a)** Ndada, mbona umerara sana na kecho akuna kazi.

**i)** Mzungumzaji ana tatizo gani? **(Alama 2)**

**ii)** Tatizo hili limesababishwa na nini? **(Alama 1)**

**b)** Watu wanapozungumza huenda wakafanya makosa ya sarufi na ya kimatamshi hapa na pale, na hata hutumia msamiati vibaya.

Eleza sababu saba za kufanywa makosa haya **(Alama 7)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 8

# KISWAHILI

Paper 3

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

***a)*** *Jibu maswali manne* ***pekee****.*
***b)*** *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima***
***c)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; Riwaya Hadithi fupi,Tamthilia na Ushairi.*
***d)*** *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja****.*
***e)*** *Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | Jumla | |

## SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI

**1. LAZIMA (ALAMA 20)**

**a.** Jadili sifa zozote nne za mtambaji bora**.** **(alama 4)**

**b.** Fafanua hasara zozote nne za miviga. **(alama 4)**

**c.** Jadili hatua tano zinazofuatwa wakati wa utafiti. **(alama 5)**

**d.** Tofautisha istilahi zifuatazo za Fasihi Simulizi**.** **(alama 3)**

**i.** Matambiko

**ii.** pembezi

**iii.** Misimu

**e.** Eleza sifa nne za maapizo**.** **(alama 4)**

## SEHEMU B: RIWAYA

**ASSUMPTA MATEI: *CHOZI LA HERI***

*Jibu swali la 2 au la 3*

**2.** Mwandishi amejadili kwa kina maudhui ya mapuuza. Thibitisha . **(alama 20)**

**Au**

**3.** Maisha yangu yalijaa shubiri tangu utotoni.

i. Eleza muktadha wa maneno haya. **(alama 4)**

ii. Fafanua mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo hili**.** **(alama 4)**

iii. Jadili jinsi mwandishi amesawiri suala la ukatili. **(alama 12)**

## SEHEMU C: HADITHI FUPI

**Mapambazuko ya Machweo *na Hadithi Nyingine***

*Jibu swali la 4 au la 5*

**4.** Fafanua jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika hadithi ya Nipe nafasi **alama 20**

**5.** "Thank you. U mteja wa pekee, unajua kuthamini huduma nzuri unapopewa."

**i)** Fafanua muktadha wa dondoo hili. **(al.4)**

**ii)** Taja na ueleze mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili. **(al.4)**

**iii)** Kwa kurejelea hadithi ya "Kila Mchezea Wembe," Fafanua changamoto zinazowakumba watumiaji wa vileo kupita kiasi. **(al. 12)**

## SEHEMU D: TAMTHILIA

**BEMBEA YA MAISHA;** *Jibu swali la 6 au la 7*

**6.** Eleza nafasi ya mbinu rejeshi katika tamthilia ya **Bembea ya Maisha** kukuza vipengele vifuatavyo:

**a)** Maudhui **(alama8)**

**b)** Ploti **(alama8)**

**c)** Wahusika **(alama4)**

***7. "Mgaala muuwe na haki umpe"***

**a)** Eleza muktadha wa dondoo **(alama4)**

**b)** Tambua kipengele cha kimtindo katika dondoo hili **(alamal)**

**c)** Eleza umuhimu wa mbinu ya kimtindo uliyotaja **(alama2)**

**d)** Dhibitisha ukweli wa msemaji kwa mujibu wa dondoo hili **(alama3)**

**e)** Onyesha namna mbinu hiyo ya kimtindo ilivyotumika katika tamthilia ya Bembea ya Maisha **(alama10)**

## SEHEMU E: USHAIRI (Alama 20)

**8. SOMA SHAIRI KISHA UJIBU MASWALI.**

1. Sidhani ni kichekesho, kesho kuwepo sidhani
Vilivyoko ni vitisho, viwewe na visirani
Mimi kupe kwenye josho, la sumu iso imani
Kesho yangu imeshaliwa.

2. Kesho yangu imeshaliwa, isibaki hata kitwa
Kwamba hai nitakuwa, kesho na kesho kutwa
Hilo haliwezi kuwa, na wakati limepitwa
Na i wapi kesho yangu?

3. Sikwambii mtondoo, au ni mtondogoo
Ajapowika jogoo, kesho sipo ng'oo
Hata simu za "haloo", hazinipati "haloo"
Nitaituhumu kesho.

4. Kesho nitaituhumu, kwa sababu ya hasama
Hasama ya mahasimu, waliolishana njama
Kutaka kunihujumu, wanizulie nakama
Itokapi yangu kesho?

5. Wa kwanza huyu Ukimwi, daima aniotea
Kwa dawa huyu hazimwi, haachi kuturingia
Amekuwa kama zimwi, mtu lisilomjua
Ati nipangie kesho?!

6. Nipange yangu matanga, au kujenga nyumba?
Nipange kung'oa nanga, au shairi kuimba?
Nipangeni cha kupanga, biashara za mtumba?
Kesho si ukoo wangu.

7. Ukimwi nduguze wako, Ebola na Malaria
Kichomi na sekeneko, mno wajifaragua
Maadamu wangaliko, vipi kesho kuwazia?
Kesho si ndu yangu mwandani.

8. Mimi napangia leo, maana kesho sijui
Usafiri nifanyao, kwenye vyombo anuwai
Una mikasa kibao, majanga ya kila nui
Salama yangu i wapi?

9. I wapi salama yangu, huku wapo wa kijicho
Ngaa nipatapo changu, waingiwa mpekecho
Kunipikia majungu, nikikosa changu hicho
Waso nitakia kesho!

10. Kesho wasonitakia, watele kama siafu
Majambazi nasinzia, tapeli na wazinifu
Roho yangu wapania, kunipeleka kwa ufu
Nipewe jina "Hayati"

## MASWALI

**a.** Ujumbe wa shairi hili unakatisha tamaa. Thibitisha. **(4)**
**b.** Hili ni shairi la aina gani? **(1)**
**c.** Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari**.** **(4).**
**d..** Eleza mbinu nne za lugha zilizotumiwa. **(4)**
**e.** Andika bahari kwa kuzingatia vigezo; **(2).**
Mizani
Vina
**f.** Onyesho jinsi mshairi alivyotumia idhini yake ya kishairi. **(2).**
**g.** Taj**a;** **(3)**
Toni
Nafsi - neni
Nafsi- nenewa.

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 9

# KISWAHILI

Paper 1

**Time: 1¾ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO:**

***(a)*** *Andika insha* ***mbili****. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima****.*

***(b)*** *Kisha chagua insha moja nyingine kutoka kwa hizo tatu zilizobakia.*

***(c)*** *Kila insha isipungue maneno 400.*

***(d)*** *Kila insha ina alama 20.*

**Kwa matumizi ya matahini pekee**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| JUMLA | 40 | |

## MASWALI

**1.** Umechaguliwa kuwa katibu wa **Chama cha Kiswahili** shuleni. Andaa kumbukumbu za mkutano uliofanyika hivi majuzi ili kupanga mikakati ya kukiendeleza Kiswahili ndani na nje ya shule yenu.

**2.** Vijana wa sasa wanakumbwa na changamoto nyingi za maisha. Thibitisha kauli hii huku ukieleza namna wanavyoweza kuzishughulikia.

**3.** Ngozi ivute ili maji.

**4.** Andika insha itakayomalizikia kwa kifungu hiki:-

**……..** ndivyo wahenga kuwa aliye juu mngojee chini. Hii ni zamu yao sasa. Wamewadhulumu wanawake kwa miaka na miaka. Wacha wapate kichapo cha kisasi.

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 9

# KISWAHILI

Paper 2

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***b)*** *Tia sahihi kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***c)*** *Jibu maswali* ***yote***
***d)*** *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
***e)*** *Majibu yote* ***lazima*** *yaandikwe kwa Lugha ya* ***Kiswahili***
***f)*** *Usitoe ukurusa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki*

**KWA MATUMIZI YA PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **Jumla** | **80** | |

## 1. UFAHAMU (ALAMA 15)

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata***

Wahenga walisema kutoa ni moyo usambe ni utajiri. Iwapo wangefufuka leo hii wangeongezea kuwa ujasiri ni moyo usiseme ni umri. Kauli hii kama ile ya kwanza imesheheni ujumbe muhimu. Katika jamii nyingi, mtoto haruhusiwi kukaa au kuzungumza mbele ya watu wazima. Akiwa wa kike ndiyo basi. Ni ajabu basi kwa mtoto wa kike kutoka jamii yenye imani kali za jadi zinazomdunisha mwanamke kuweza kupata tuzo yenye staha ya juu zaidi.

Malala Yousafzai alishinda Tuzo ya Nobel mwaka 2014 akiwa na umri wa miaka 17. Aliyeshinda naye tuzo hii adhimu ni Kailash Satyarthi. Kigoli huyu alituzwa tunu hii kwa kupigania haki za wasichana kupata Elimu nchini Pakistan. Harakati hizi hakuzianza juzi. Mwaka 2012 alipigwa risasi na mijibaba ya ugaidi ya kundi Fulani linaloegemea mrengo wa siasa kali kwa 'hatia' za kuwatetea mabanati. Inasemekana alishambuliwa alipokuwa akisafiri kwenye basi la shule. Kilichochochea mashambulizi ni tuhuma kuwa alikuwa ameanzisha jukwaa kwenye mtandao wa Shirika la Utangazaji la BBC alilokuwa akichangia maandishi alipokuwa na umri wa miaka 11. Maandishi yake yalikuwa na ujumbe wa kupinga juhudi za makundi Fulani kuwanyima wanawake Elimu.

Haikuwezekana hata baada ya kupona kurudi Pakistani. Alihamia Uingereza alipofadhiliwa na wahisani. Licha ya kuwa aliishi ugenini na bila aila yake mwana huyu hakupoteza makali ya ari yake ya kuendelea kutetea maslahi ya kielimu ya wenzake wa kike.

Yeye ndiye mwenye umri wa chini zaidi katika historia kupata tuzo hili. Baadhi ya wale walioshinda Nobel katika umri mkubwa ni Desmond Tutu, Nelson Mandela na Wangari Maathai. Kila mmoja wao alitambuliwa kwa sababu mahususi zinazohusu jitihada za kuboresha maisha ya wanajamii.

Njia nyingine kuu aliyoitumai Malala ni hotuba. Mwaka 2013 alihutubia Kongamano la Vijana la Umoja wa Mataifa katika hafla iliyoandaliwa kwa heshima yake. Aliwashangaza wengi kwa ufasaha na uweza wake wa kutongoa hoja. Kila mtu aliguswa na dhati ya kauli zake. Katibu Mkuu hakuwa na jingine ila kulipa kongamano hilo jina Malala. Mtoto huyu wa kimaskini alipewa taathima ambayo watu wachache sana wamepata kutunukiwa. Hii ni heshima inayotengewa marais na wafalme. Na wanapoipata huruhusiwa kuhutubia kwa dakika tano tu.

Mwaka 2014, viongozi wenye sifa za ubabe wa kuwabinya wapinzani wao lakini wameshindwa kuwaokoa wanyonge walipokuwa wakilaza damu, yeye alisafiri hadi Naijeria kudai kuachiliwa kwa wasichana 200 waliotekwa nyara na kundi haramu.

Katika hotuba iliyojaa hisia ambazo huhusishwa tu na akina mama wenye uzazi mkubwa aliyoitoa Naijeria , aliwaasa watoto wenzake wasimruhusu mtu yeyote awaambie kuwa wao ni wanyonge au hawana uwezo. Aliwanasihi kuwa wao sio wadhaifu kuliko wavulana na wasijione wanyonge kuliko watoto wa kitajiri wala wale wanaotoka nchi zenye uwezo mkubwa . Alihitimiza kuwa wao ndio watakaoijenga jamii na kuwa wana uwezo wa kuyaendesha mambo.

Mshindi wa tuzo hii yenye thamani ya dola za kimarekani milioni moja ameitabaruku kwa watoto wenzake ulimwenguni. Bila shaka mwanzilishi wa tuzo ya Nobel ameguswa na tendo la mtoto huyu huko kuzimuni. Kama kumbukizi tunu hii hutolewa wakati wa kuadhimisha kifo cha Mwanaviwanda wa

Kiswidi aliyeasisi tuzo hii kufuatana na wosia wake mwaka 1895. Kama Alfred Noble mwenyewe, kwake Malala, ngwenje au darahimu si muhimu . Lililo muhimu ni ukombozi wa watoto na

hasa wa kike kielimu. Malala bado anavaa mtandio wake huku akidhihirisha adabu na unyenyekevu wa kupigiwa mfano.

## MASWALI

**1.** Eleza mtazamo wa jamii ya Malala kuhusu watoto wa kike. **(alam.2)**

**2.** Unafikiri Malala alistahili kutuzwa Tuzo ya Nobel? Toa sababu tatu. **(alama.3)**

**3.** Ni njia zipi alizozitumia Malala kutetea haki ya watoto wa kike kupata Elimu? **(alama 3)**

**4.** Malala anawapa ushauri upi watoto wenzake? **(alama. 1)**

**5.** Kwa nini inasemekana kuwa Tuzo ya Nobel ina staha ya juu zaidi? **(alama.2)**

**6.** Andika kichwa kifaacho kwa kifungu hiki. **(alama.2)**

**7.** Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa: **(alama. 3)**

**a)** Tunu

**b)** Wahisani

**c)** Ubabe

**2. UFUPISHO**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Ukame ni tukio hatari la kimaumbile. Athari zake hutofautiana kutoka eneo moja hadi lingine. Kwa sababu hiyo, si rahisi kuielewa dhana ya ukame; kwa hakika si rasihi kuifafanua dhana hii. Katika eneo la Bali, kwa mfano, isiponyesha kwa muda wa siku sita wenyeji huchukulia hali hiyo kuwa ukame japo kiasi hicho cha mvua ni kikubwa mno ikilinganishwa na Libya ambayo hupata kiasi kidogo cha chini ya milimita 180 ya mvua kwa mwaka.

Katika hali ya kawaida ukame hutokana na kipindi kirefu cha uhaba wa mvua hasa katika mzima au zaidi. Uhaba huu wa mvua huweza kusababisha uhaba wa maji kwa shughuli, kundi au sekta Fulani. Shughuli za binadamu huweza kufanya hali ya ukame mbaya zaidi.Shughuli hizo ni pamoja na kilimo, unyunyiziaji maji na ukataji wa miti.

Ni vigumu kubaini wakati mahususi ambao ukame huanza kwa kipindi hicho cha ukosefu wa mvua huwa cha mfululizo, na eneo huendelea kupata mvua iliyopungua kwa miezi au hata miaka. Mimea hukauka na wanyama hufa kutokana na ukosefu wa maji. Ukame basi huwa hatari kwa maisha ya

binadamu na viumbe wengine kwa kuwa huweza kusababisha njaa na kuyafanya maeneo kuwa majangwa.

Mbali na ukosefu wa mvua, ukame pia husababishwa na kiangazi. Kiangazi huongeza kiwango cha joto. Joto hilo hufanya maji yaliyohifadhiwa kuwa mvuke haraka, hivyo kiwango chake kupungua. Hali ya *el ninyo* pia husababisha ukame katika baadhi ya maeneo ambayo huwa hayana mvua. Upepo huivutia mvua mahali panaponyesha na kuliacha kame eneo ambalo halina mvua ya aina hii. Hata katika maeneo yenye mvua ya *el ninyo* , kiangazi kikali huifuata na hivyo kusababisha ukame. Hali hii huitwa *la nina*. Mambo yanayotokana na mabadiliko ya hali ya anga ulimwenguni pia yanaweza kuchangia ya ukame. Ongezeko la joto duniani linafanya hali ya ukame kuwa mbaya zaidi.

Ukame una mdhara chungu nzima kwa binadamu. Madhara hayo huweza kuwa ya kiuchumi, kimazingira, kimazingira au hata kijamii. Ukame husababisha kupungua kwa mimea na mavuno. Huweza pia kutokea dhoruba za mchanga. Dhoruba hizi hutokea palipo na jangwa. Ukosefu wa maji ya kunyunyizia mimea husababisha njaa na magonjwa kama vile utapiamlo yanayotokana na ukosefu wa lishe bora. Makazi ya wanyama wanchi kavu na wale wa majini pia huathiriwa vibaya. Hali kadhalika, ukame husababisha uhamaji. Hii inamaanisha kuwa jamii huweza kutoka katika makazi asilia na wakati mwingine huweza hata kuwa wakimbizi.

Ukame husababisha ukosefu mkubwa wa maji. Ukosefu huu huwa na athari hasi kwa maendeleo ya viwanda kwa kuwa vingi huhitaji kiasi kikubwa cha maji. Juu ya hayo, maji huhitajika katika kuzalisha umeme. Umeme una matumizi mengi katika viwanda, nyumbani, afisini na hata hospitalini. Ukosefu wa umeme basi huwa ni tatizo kuu.

Aidha, ukame husababisha madhara mengi, binadamu wanaweza kujikinga kutokana na uhaba wa rasilimali za asili kama vile chakula na maji. Pia mioto mikubwa huweza kuenea haraka wakati wa ukame na hivyo kusababisha vifo vya binadamu na wanyama na uharibifu wa rasilimali nyingine. Ingawa ukame husababisha madhara mengi, binadamu wanaweza kujikinga kutokana nao kwa kupunguza makali ya ukame. Jambo la kwanza wanaloweza kufanya binadamu ni kuhifadhi maji. Maji ya mvua yanafaa kuhifadhiwa katika mabwawa na mapipa. Haya yanaweza kutumiwa wakati wa ukame hasa katika kukuza mimea. Mkakati mwingine ni kutumia mbinu za kupunguza chumvi na kemikali nyingine zilizomo kwenye maji ya bahari ili yaweze kutumika katika unyunyiziaji wa mimea. Hili litapunguza tatizo la ukosefu wa chakula. Pia ni muhimu kufanya utafiti kuhusu hali ya anga ili kupanga na kuweka mikakati ifaayo kukabiliana na hali hiyo.

Ni muhimu kuwa na mipangilio mizuri ya matumizi ya ardhi. Mathalani upanzi wa mimea itakayozuia mmomonyoko wa udogo, kubadili aina ya mimea inayokuzwa sehemu fulani pamoja na upanzi wa mimea isiohitaji mvua nyingi katika kame ni hatua mwafaka. Aidha, ni vizuri kupunguza matumizi ya maji hasa katika mazingira ya nyumbani kwa mfano tunapofua na kuosha. Njia nyingine ya kukabiliana na tatizo hili ni kusafisha maji yaliyotumiwa ili kuyatumia tena.

**(a)** Kwa maneno **50**, eleza visababishi vya ukame kwa mujibu wa taarifa

**(alama. 4; 1 ya mtiririko)**

**Matayarisho**

**Nakala safi**

**b)** Fupisha ujumbe wa aya ya **tano** hadi **saba** kwa maneno 70. (alama. 6; 1 mtiririko )

**Matayarisho**

**Nakala Safi**

**a)** Eleza masuala ambayo mwandishi ameibua katika aya mbili za mwisho kwa maneno **60**.

**(alama 5; 1 ya mtiririko)**

**Matayarisho**

**Nakala safi**

## 3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA ALAMA 40

**a)** Andika maneno yenye miundo ifuatayo . **(alama.2**

**i)** Kipasuo ghuna cha midomoni, irabu ya chini, kati, kipasuo sighuna cha ufizi, irabu ya juu mbele.

**ii)** Nazali ya ufizi, kipasuo ghuna cha kaakaa laini, irabu ya juu, nyuma, irabu ya nyuma wastani.

**b)** Bainisha silabi zinazowekwa shadda katika maneno yafuatayo **(Alama. 1)**

**i)** Waliotusifia

**ii)** Sherehekea

**c)** Andika sentensi ifuata katika wingi. **(Alama.2)**

Wayo wa mguu wangu wa kulia umeungua

**d)** Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. **(alama. 1)**

Njia hii yetu inapitiwa na mtu mnene

**e)** Tunga sentensi moja yenye kivumishi cha pekee kinachoonyesha idadi jumla. **(alama.1**

**f)** Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo

**i)** Maafisa hao walipewa uhamisho. Maafisa wengine hawakupewa uhamisho

(unganisha kuunda sentensi ambatano) **(alama.2)**

**ii)** Hadithi hiyo ilitungwa vizuri ikawavutia wengi

( badilisha vitenzi vilivyopigiwa mstari kuwa nomino) **(alama.2)**

**iii)** Tunda halitaoshwa vyema. Tunda halitalika .

(unganisha kuwa sentensi moja kwa kutumia ‘po’) **(alama.2)**

**iv)** Kengewa alitoa ahadi .Wengi waliiamini ahadi hiyo. (unganisha kuwa sentensi moja inayoanza kwa . Ahadi….) **(alama .2)**

**g)** Tunga sentensi ya masharti inayoonyesha kwamba kitendo kilifanikiwa kutokana na kufanikiwa kwa kingine. **(alama. 2)**

**h)** Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kielezi. **(alama.2)**

**i)** Ainisha maneno ya liyopigwa mstari katika sentensi ifuatayo. **(alama. 3)**

Mwenyewe hakuwa amekupa ruhusa kuitumia

**j)** Akifisha sentensi ifuatayo.

Kiwango cha umasikini katika kaunti ya homabay kinasikitisha sana itabidi sote wakatizi wa hapa tujizatiti ili tutimize malengo ya millennia seneta mteule alituhimiza

**k)** Andika maneno yenye mofimu zifuatazo. **(alama. 2)**

**i)** Umoja (ngeli ya u-i), mzizi, kiisho

**ii)** Kikanushi, kiambishi ngeli (ki-vi, Umoja)

Mzizi, kauli tendeka, kiisho

**l)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. **(alama. 2)**

KN (N+RH) + KT (T+RE)

**m)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kukanusha . **(alama. 2)**

Ngoma hizo zilihifadhiwa ili ziuzwe mjini.

**n)** Andika sentensi ifuatao katika wakati uliopita hali ya mazoea. **(alama.2)**

Ekapolon atawashauri wanafunzi kuhusu umuhimu wa kufanya bidi

**o)** Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendesha kwa kuzingatia maneno yaliyopigiwa mstari **(Alama. 2)**

Alimfanya mtoto anywe uji ukamfanya ashibe.

**p)** Tunga sentensi ukitumia mzizi, ingineo kumaanisha “mbali na”. **(Alama. 1)**

**q)** Hewala ni kwa kukubaliana na jambo, **……** .ni kwa kutoka kitu kinusurike, na**…….….**ni kwa aliyefanya vyema katika jambo. **(alama.1)**

**r)** Zito ni kwa jepesi, **……..**ni kwa choyo na, **……**ni kwa kali. **(alama.2)**

**s)** Andika visawe vya kauli zi zilizopigiwa mstari.

Atyang alikumbwa na matatizo mengi lakini hakukata tama.

## 4. ISIMU JAMII. **(Alama.10)**

Eleza sababu tano zinazowafunga watu kufanya makosa ya kisarufi katika mazungumzo.

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 9

# KISWAHILI

Paper 3

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako, namabari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
***b)*** *Jibu maswali manne pekee.*
***c)*** *Swali la kwanza ni la Lazima.*
***d)*** *Maswali haya mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki.*
***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

**KWA MATUMIZI YA MTIHANI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

## SEHEMU YA A

## FASIHI SIMULIZI

**1. Lazima**

Tumia kifungu kifuatacho kujibu maswali yanayofuata

**a)** Nyumbani mwetu mna papai lilioiva lakini siwezi kulichuma – ndugu wa kiume asimuoe nduguye wa kike.

**I)** Bainisha kipera kinachorejelewa **(Al 1).**

**II)** Andika shughuli moja ya Kijamii na moja ya Kiuchumi ambazo huendelezwa katika jamii ya utingo huu. **(Al 2)**

**III)** Eleza dhima nne za kipera kinachorejelewa katika jamii yako. **(Al 4)**

**IV)** Wewe ni mwasilishaji wa kipera hiki jukwani. Eleza mambo matano ambayo utazingatia katika uwasilishaji wako. **(Al 5)**

**b)** Fafanua majukumu yoyote manne ya nyimbo katika jamii. **(Al 8)**

## SEHEMU B

## TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA

**2)** Kwa kurejelea mifano mbalimbali thibitisha namna ndoa katika tamthilia ya **Bembea ya maisha** zimemulika uhalisia wa jamii za kiafrika. **(alama20)**

***3) "Lakini nilivyosema, Mungu hamwachi mja wake.."***

**a)** Eleza mutadha wa dondoo hili **(alama4)**

**b)** Tambua sifa tatu za msemewa **(alama3)**

**c)** Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kukuza vipengele vifuatavyo:

Ploti **(alama2)**

Maudhui **(alama4)**

**d)** Kwa kurejelea tamthilia nzima eleza ukweli wa kauli "Mungu hamwaachi mja wake." **(alama7)**

## SEHEMU C

## RIWAYA

**4.** Eleza ufaafu wa anwani ya chozi la heri **(Al 20)**

**5a.** “uuuui! Uuuui! Jamani tusaidieni! Uuuui! Uuuui! Mzee kedi usituue, sisi tu majirani! Maskini wangu!”

a)Elezea muktadha w dondoo hili**.** **(Al 4)**

b) Fafanua tamathali ya usemi huu **(Al 2)**

c) taja mambo yaliyofanyikia Ridhaa awali ya kuashiria mikasa. **(Al 4)**

b) Kwa kurejelea riwaya ya chozi la heri jadili dhiki za wakimbizi**.** **(Al 10)**

## HADITHI FUPI - MAPAMBAZUKO YA MACHWEO

**6)** Fafanua changamoto wanazokumbana nazo waajiriwa katika hadithi **Harubu ya Maisha** **(alama 20)**

**7)** NDOA ni taasisi iliyokuzwa katika hadithi **fadhila za punda.** Fafanua **alama 20**

## SEHEMU YA E

## USHAIRI

**8.Soma shairi kisha ujibu maswali**

Ndugu ona mbwa yule, ambaye ananyekenya;
Yaone mabuu yale, ambayo yamchezeya;
Kuwa leo yuafile, mwili yanautaniya;
Jana awile jasiri!

Juzi shujaa awile, pasiwe kumfikiya;
Kwenye makani yale, alipojisururiya;
Leo kuwa yuafile, mainzi yamchekeya;
Jana awile Jasiri!

Mijino mikubwa ile, ambayo ‘mejitokeya;
Yali kiwaliza wale, karibu walosogeya;
Tena akibweka yule, waoga walijinyiga;
Jana awile jasiri!

Kamwe kuishi milele, kupe ukajinyonyeya;
Walo chini yako wale, muhali unawaziya;
Ameshindwa yule pale,sembuse wewe sikiya;
Jana awile jasiri!

Kama walo hai wale, yafaa kuzindukiya;
Ni dunia maji mle, muhimu kujiwaziya;
Wazipunguze kelele, na kwingi kujishauya;
Jana awile jasiri!

**a)** Fafanua ujumbe wa shairi hili **(Al 2)**
**b)** Eleza muundo wa shairi hili **(Al 5)**
**c)** Eleza toni ya shairi hili **(Al 2)**
**d)** Ainisha shairi hili kwa kuzingatia **(Al 3)**
**i)** Ruwaza ya mistari
**ii)** Ruwaza ya vipande
**iii)** Ruwaza ya mizani
**e)** Eleza mbinu nne ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi **(Al 4)**

**f)** Bainisha sifa mbili za anayezungumziwa katika shairi hili **(Al 2)**
**g)** Eleza tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika shairi hili **(Al 2)**

**Au**

**9.Soma shairi kisha ujibu maswali**

**Nizike Ningali Hai!:** Hassam Muchai
Kipusa Binti Hamadi, siku n'takuwa kimba
Nizikwe Kifudifudi, na yoyo kuyumbayumba
Takuwa bure biladi, matozi ungayasomba
Nizike ningali hai, n'kifa hutonizika

Tena ningaumwa ungo, na mapumu kuugua
Lioze ini na nyongo, na pua zisipumua
Takuwa sina kinyongo, mradi nimeshatua
Nizike ningali hai, n'kifa hutonizika

Nizike sasa mwenzangu, nizike ningali hai
Singojee kufa kwangu, uanze kurairai
Kulilia kifo change, ni bure hakukufai
Nizike ningali hai, n'kifa hutonizika

Nikifa hutonizika, kimwana sanda nunua
Manukato ya kupaka, na nguo za kuanua
Nivishe sione shaka, Washindwe kupambanua
Nizike ningali hai, n'kifa hutonizika

Tena nikande misuli, nikande pande kwa pande
Siate kiwiliwili, shingo, miguu ikande
Umalizapo kiwiliwili, mwenzangu niende shonde
Nizike ningali hai, n'kifa hutonizika

***a)*** Dhamira ya matunzi wa shairi hili ni gani? **(Al 2)**
***b)*** Bainisha nafsineni katika shairi hili **(Al 2)**
***c)*** Eleza toni ya shairi hili **(Al 2)**
***d)*** Changanua muundo wa shairi hili **(Al 5)**
***e)*** Fafanua maana ya kibwagizo cha shairi hili **(Al 2)**
***f)*** Eleza mbinu nne ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi **(Al 4)**
***g)*** Bainisha bahari ya shairi hili **(Al 3)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 10

# KISWAHILI

Paper 1

**Time: 1¾ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

**a)** Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

**b)** Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

**c)** *Andika insha mbili. Swali la **kwanza** ni la lazima.*

**d)** *Kisha chagua insha nyingine moja kutoka kwa hizo tatu zilizobakia.*

**e)** *Kila insha isipungue maneno 400.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| | Jumla 40 | |

## INSHA

**1. Lazima.**

Umepata kazi ya utangazaji katika kampuni moja nchini. Umealikwa kwa mahojiano. Andika mahojiano kati yako na mkurugenzi wa kampuni hiyo **(al.20)**

**2.** Andika kisa kitakachodhihitisha maana ya methali sikio la kufa halisikii dawa **(al.20)**

**3.** Jadili mikakati inayotumiwa na serikali kupambana na tishio la usalama nchini **(al.20)**

**4.** Andika kisa kitakachomalizia kwa maneno haya

**…….**nilitamani ardhi ipasuke inimeze mzima mzima. **(al.20)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 10

# KISWAHILI

Paper 2

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

***1.*** *Jibu maswali yote katika nafasi uliyopewa.*

***2.*** *Andika majibu yako kwa lugha ya Kiswahili.*

| | SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|---|
| 1. | Ufahamu | 15 | |
| 2. | Ufupisho | 15 | |
| 3. | Matumizi ya lugha | 40 | |
| 4. | Isimujamii | 10 | |
| | Jumla | 80 | |

## SEHEMU YA KWANZA (ALAMA 15)

### UFAHAMU

MAJILIO ya wakoloni barani Afrika ambao walidumisha utawala wao katika'bara jeusi' kwa takriban kipindi cha miaka sabini kulisababisha mivutano ya kiisimu mpaka leo (Ngugi,1993,uk 42)

Wakoloni walizipa kipaimbele lugha za kigeni na kuzikandamiza zile za kiasili zisiweze kuelezea uhalisi wa maisha katika viwango vya teknolojia. Kwa hakika, itazichukua lugha hizi muda mrefu kwenda sambamba na maendeleo ya fikra na teknolojia kwa kutoandaliwa vyema kutekeleza wajibu huu.

Lugha ni kipengele muhimu sana cha utamaduni. Hivyo basi serikali zinawajibika kuzilinda, sio tu kwa sababu lugha zimejaa maarifa mengi ya tangu jadi, bali pia kwa sababu lugha ni chombo cha maendeleo ya binadamu.

Maarifa yote na ufanisi wa binadamuu huelezwa kupitia kwa lugha. Mwelekeo ulioonekana kishika sana katika mataifa megi barani afrika, ikiwemo Kenya, ni kuhusudu lugha na tamanduni za kigeni. Lugha za kigeni zimehusishwa na maendeleo na ustaarabu.

Hatua iliyochukuliwa na serikali ya Tanzania ya kufunza masomo yote kwa lugha ya Kiswahili kuanzia darasa la kwanza hadi chuo kikuu ilizua kejeli na kicheko kwa baadhi wa wakenya; hususan katika stesheni za fm. Kisa na maana: jambo hili haliwezekani!

Je, ni lazima tutegemee lugha za kigeni kupiga hatua kimaendeleo? La hasha! Kuna ushahidi wa mataifa kama vile Uchina, Ufini,Sweden, Indonesia,Japan,Malaysia, India,Uyahudi n.k. yalioendeleza lugha zao kimakusudi ili ziweze kukidhi haja kufundishia masomo yote hadi viwango vya juu sana vya elimu.

Katika sherehe za kuadhimisha siku ya kimataifa ya 'lugha mama' miongoni mwa mataifa wanachama wa umoja wa mataifa (united Nations International Mother Language Day) mnamo februari, 2000, mkurugenzi wa shirika la umoja wa mataifa kuhusu Elimu,sayansi na utamanduni(UNESCO), jenerali koichiro Matsuura alisema: 'mojawapo ya vigezo vitumiwayo na wataalmu kukadiria iwapo lugha Fulani inatishiwa kuangamia au kufa ni iwapo watoto wanajifunza lugha hiyo…

Iwapo takribani asilimia 30 ya watoto, hawajifunzi lugha yao'ya mama', basi lugha hiyo inatishiwa kuangamia… lugha hiyo bila shaka huenda ikafa pamoja na kizazi kinachoizungumza.'

Kwa mujibu wa UNESCO, lugha nyingi ambazo zimetishiwa kufa au kutoweka zinapatikana katika mabara ya merakani na Australia. Shirika hililinaongeza kuwa, nchini Kenya, lugha kama vile suba,El Molo, Lorkoti, Yaaku sogoo,kore,Segeju,Omotik, na KInare' zimekufa' au kutoweka huku Bong'om na Terik/Tiriki zimo kwenye hatari ya kutoweka.

Lugha pia huangamia wakati ambapo lugha hizo zinashindwa kuzihudumia jamii zao ipasavyo kama chombo mahsusi cha mtagusano wa kijamii. Baadhi ya lugha huku na kusambaa huku zingine zikididimia na hatimaye'kumezwa' na lugha zilizoshaimiri au hata kutoweka kabisa. Kwa mfano, jamii ya Seng'wer 'imemezwa' na makabila kama vile Wapokot, Wamarakwet, Wakeiyo,

Watugen, Wanandi na Waluhya, ilhali Wakipsigis,Watugen na Wamaasai'wammeza'jamii ya Ogiek.

Hata hivyo,mkaoni nyanza ya kusini nchini Kenya, wakakti wa uchaguzi mdogo wa useneta katika gatuzi ya Homabay, tulisikia kupitia kwa profesa….(aliyewania kiti), kwamba jamii ya Abasuba ipo-wala'haijamezwa' na jamii ya waluo.

Msimamo wa wizara ya elimu nchini Kenya kuhusu ufundishaji wa 'lugha ya mama' unaonekana kuyumba. Mara tunaambiwa lugha ya mama itafundishwa katika madarasa ya chini katika shule za mashambani; mara tunaambiwa itafundishwa katika madarsa ya chini katika maeneo Fulani; ilimradi wizara haijitokeza waziwazi na sera wala mwongozo mwafaka.

Njogu (2003) anahoji;'mkondo uliopo nchini Kenya hivi sasa ni ule wa jamii nyingi kuwahimiza watoto wao kuzungumza lugha za kigeni kama vile kiingeraza, kifaransa, na hata kijerumani na kupuuza lugha ya kwanza. Hii inatokanan na imani kuwa lugha za kigeni ndizo zitakazofungua njia za kigeni ndizo zitakazofungua njia za maendeleo hapo baadaye.

Mkondo huu usipozuiliwa, huenda ukasababisha vifo vya lugha za kiasili' Njogu anaendelea: 'uwezo wa kuongea lugha nyingine pamoja na yenye asili ya kikoloni huweza kujenga jisia za kujiamini miongoni mwa watu wasiokuwa na uwezo mwingi wa kiuchumi-nako kujiamini ni hatua ya awali ya kuleta maendeleo ya jamii'MAKIWA! Familia, jamaa na marafiki wa Grace Ogot aliyeandika baadhi ya kazi zake kwa lugha ya mama.

## Maswali

**1.** Ni nini kisababishi cha mivutano ya kiisimu katika bara la afrika **(al. 2)**

**2.** Serikali zinafaa kuwajibika katika kuzilinda lugha . eleza **(al. 2)**

**3.** Ni hatua gani ambayo ilichukuliwa nan chi ya Tanzania ambayo ilizua kejeli na kicheko kwa baadhi ya wakenya **(al. 1)**

**4.** Lugha ya mama inasemekana kuwa katika tishio la kuangamia kwa kutumia vigezo gani? **(al. 2)**

**5.** Kwa nini jamii nyingi huwahimiza watoto wao kuzungumza lugha za kigeni kigeni **(al. 2)**

**6.** Kuna mabara ambayo yametajwa kuwa na lugha nyingi ambazo zinatishiwa na kufa au kutoweka. Yataje mabara hayo. **(al. 2)**

**7.** "Msimamo wa wizara ya elimu kuhusu ufundishaji wa lugha ya mama unaonekana kuyumba " Eleza **(al. 2)**

**8.** Eleza maana ya msamiati ufuatayo kwa mujibu wa taarifa au ufahamu

**a)** Takriban

**b)** Mtagusano

## UFUPISHO

TUMEKWISHA kueleza katika makala ya hapo awli kuwa lugha ni maalum kwa binadamu tu na kwamba hakuna kiumbe yeyote ambaye si mwanadamu mwenye uwezo wa kujua, kujifunza na kutumia lugha zaidi ya binadamu.

Bila shaka, mawasiliano ya binadamu yanaweza kujumuishwa kama mawasiliano ya wanyama yaliyoendelezwa. Utafiti wa mawasiliano ya wanyama, uitwao'zuosemiotiki'(zoosemiotics) tofauti na 'athroposemiotiki'( utafiti wa mawasiliano ya binadamu), umechangia pakubwa katika ukuzaji wa uwezo wa mnyama wa kutambua. Jambo hili ni dhahiri kwani binadamu wanaweza kuwasiliana na wanyama kwa kutumia njia za kipekee lakini si'lugha'.

Makala haya yanalenga kuthmini na kuzamia sifa au tabia za lugha ya mwanadamu. Kimsingi sifa ai Tania hizi ndizo zinazoitofautisha lugha ya mwanadamu na aina nyinginezo za mawasiliano zitumiwazo na ndege au wanyama.

Unasibu wa lugha ya binadamu unaangaliwa katika ukweli kwamba binadamu hazaliwi na lugha, anakutana nayo kwa unasibu tu. Hakuna uhusiano wa moja kwa moja au wa aili kati ya kitajwa(kitu au umbo linalomaanishwa au maana).

Uhusiano wake ni wa unasibu na unatokana na makubaliano ya watu wajua – lugha yao. Hata makubaliano haya ya kwamba kitu kiitwe au dhana Fulani iitwe na kuelezwa kwa namna Fulani ni ya kinasibu tu. Hapa tunamaanisha kwamba mkutano au kikao ambaco binadamu amewahi kukaa akasema mathalani neno "chuki" limaanishe hali ya kutompenda mtu au neno "upendo" limaanishe hali ya kuonesha huba kwa mtu. Kila jamuiya-lugha ina namna yake ya kuufasili na kuelekezea ulimwengu kwa lugha yake ambayo inatofautiana na jamuiya-lugha nyingine.

Lugha ya mwanandamu inao uwezo wa kuambukiza utamanduni kutoka katika kizazi kimoja kwenda kizazi kingine au kutoka katika jamuiya-lugha moja kwenda katika nyingine. Leleweke kuwa, uwezo huu wa kuambukiza maarifa ya lugha hufanyika kwa njia ya kusoma au kujifunza na si kurithi. Kwa mfano, mtu anaweza kurithi. Kwa mfano, mtu anaweza kurithi maumbile kutoka kwa wazazi wake, mathaalan aina ya nywele, macho, pua, kucha au masikio lakini mtu hawezi kurithi lugha.

Lugha inamfikia kwa kuambukiza katika jamuiya-lugha anayokulia na kulelewa. Yatupasa tukumbuke kuwa, ingawa mwanadamu anazaliwa na ule uwezo(kitengo cha lugha) wa kujifunza lugha"language Acquisition Device"kama anavyoeleza mwanaisimu Naom Chomsky, lakini hazaliwi na lugha. Hii ndiyo sababu mwanandamu anaweza kujifunza lugha yeyeote ile na kwa wakati wowote maadamu yupo katika mazingira na hali ya kawaida na saidizi.

Lugha ya mwanandamu imepangwa katika viwango viwili ambavyo vinashirikiana na kukamilishana. Kiwango cha kwanza I kile kiwango cha utamkaji wa sauti au utoaji wa sauti kwa kutumia ala mbalimbali za matamshi. Sauti hizi zikisimama peke yake hazina maana yoyote, ni kama milio tu kama kupiga chafya, au kelele zinazotokana na kubururwa kwa meza kwenye sakafu au kelele za injini ya pikipiki.

Sauti hizi zinapounganishwa (kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za lugha husika) tunapata kiwango kingine cha pili cha maana. Sifa ya uwili inadhihirisha sifa ya uwekevu katika lugha ya

mwanadamu kwani kwa kutumia sauti hizi chache mzungumza lugha anaweza kutunga na kutamka sentensi nyingi au tungo nyingi na zenye maana tofauti tofauti bila kikomo

Suala jingine la msingi ni kwamba, tunaposema kuwa lugha imegawika katika viwango viwili, kiwango cha sauti na kiwango cha maana haimaanishi kwamba binadamu anatumia viwango hivi kuipekepeke. Hata siku moja mwanadamu hasemi kwamba sasa naanza kutamka sauti za neno Fulani, halafu ndiyo niweke maana yake. La hasha!

Binadamu hutamka kwa mara moja sauti pamoja na maana zikiwa zimebebana ndani kwa ndani(hutamka sauti pamwe na maana). Yaani, wakati anatamka sauti na kuziunganisha ndiyo wakati anaambatanisha na maana ndani yake. Hii ndiyo sifa au uwili katika lugha ya mwanadamu.

Uzalikaji katika lugha ya binadamu unajidhihirisha katika uwezo wa mwanandamu kubuni na kuunganisha maneno na miundo mbalimbali ya tungo bila kikomo. Mjuzi wa lugha anastahili kutunga na kuzielewa tungo mbalimbali ikiwa ni pamoja na zile ambazo hajawahi kuzisikia wala kuzitunga yeye mwenyewe.

Aidha, anapaswa kuelewa tungo zilizotungwa na watu wengine na kufahamu maana ya kisemantiki na ile kipragmatiki zinazodhihirika kadri anaposimbua jumbe zilizomo. Anapaswa kuzielewa tungo sahihi na zile zisizo sahihi. Hivyo uwezo huu unatofautiana na aina nyingine ya mawasiliano inayotumiwa nan a wanyama wengine, kwa mfano,"nyenje ni mnyama mwenye milio au ishara nne za kuchagua ili awasiliane, tumbili ana miito sita tu. Hivyo wanyama wote hawa wana idadi isiyobadilika ya milio na sauti au ishara na hawana uwezo wa kubuni namna nyingine ya kuwasiliana au kubuni milio mingine ya kuwezesha na kudumisha mawasiliano yao.

## Maswali

**a)** kwa maneno kati ya 50- 60 fupisha aya tau za kuanza (**al. 8. 1 mtiririko)**

**matayarisho**

**Jibu**

**b)** kwa kutumia maneno 60-70 bainisha ujumbe ambao mwandishi anaibua katika ya tatu za mwisho (al. 7, 1 mtirirko)

**matayarisho**

**Jibu**

## SEHEMU YA TATU: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**1.** Bainisha sifa za sauti ifuatayo /o/ **(al. 2)**

**2.** Kambishi ni nini? **(al. 1)**

**3.** Onyesha matumizi ya kiambishi "ku" katika sentensi ifuatayo

Nitakupa fedha za mchango ili uende ukaniwakilishe **(al. 2)**

**4.** Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizowekwa katika mabano

**i)** pa(kutendeka)

**ii)** ha(kutendewa) **(al. 2)**

**5.** Tunga sentensi moja katika wakati ujao hali timilifu **(al. 1)**

**6.** Onyesha aina za virai katika sentensi ifuatayo.

Mteja wangu atawasili kesho saa tatu **(al. 2)**

**7.** Tumia kivumishi kionyeshi kisisitizi cha mbali kidogo pamoja na nomino katika ngeli ya li-ya kutunga sentensi **(al. 2)**

**8.** Tunga sentensi moja yenye kishazi huru na kishazi tegemezi ukitumia'o' rejeshi tamati **(al. 2)**

**9.** Changanua sente4nsi ifuatayo kwa jedwali/visanduku

Mkulima alilima kwa bidii lakini hakupata mazao mengi **(al. 4)**

**10.** Onyesha aina za shamirisho katika sentensi uliyopewa

Babu alisomewa barua na mjukumu wake

**11.** Tunga sentensi mbili ili kuonyesha matumizi ya kiambishi 'po' cha

(i) Wakati

(ii) Mahali

**12.** Changanua kitenzi kufuatacho **(al. 4)**

Alimlisha.

**13.** Kwa kutunga sentensi eleza matumiz mawili tofauti ya **kiakifishi** **(al. 2)**

Parandesi

**14.** Eleza maana ya sentensi ya masharti (**al. 1)**

Tunga sentensi ya **masharti (al. 2)**

**15.** Andika visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari

Daktari alipokuwa akimtibu alishikwa na kisulisuli **(al. 2)**

**16.** Bainisha kihisishi na kihusishi katika sentensi

Naam! Ameingia kabla ya mwalimu kufika **(al. 2)**

**17.** Andika sentensi ifuatayo kwa msemo wa taarifa

"nitaweza kuondoka kwangu kesho asubuhi."mwalimu akasema **(al. 3)**

**18.** Bainisha kiima na chagizo katika sentensi

Mwenyewe alimpenda kwa dhati **(al. 2)**

## SEHEMU YA NNE: ISIMU JAMII (ALAMA 10)

**1.** Taja dhana au nadharia zinazohusiana na chimbuko la lugha ya Kiswahili **(al. 3)**

**2.** Eleza maana ya istalahi zifutatazo kama zinavyotumika katika isimujamii

**i)** misimu

**ii)** lafudhi

**iii)** pijini **(al. 3)**

**3.** Taja sifa nne za sajili ya maabadini **(al. 4)**

# KCSE 2023 REPLICA PREDICTIONS

*Kenya Certificate of Secondary Education*

## PREDICTION TRIAL 10

# KISWAHILI

Paper 3

**Time: 2½ Hours**

---

**NAME**……

**SCHOOL**…… **SIGN**……

**INDEX NO**…… **ADM NO**……

*Kenya Certificate of Secondary Education.*

**MAAGIZO**

***a)*** *Jibu maswali manne* ***pekee****.*

***b)*** *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima***

***c)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; Riwaya Hadithi fupi,Tamthilia na Ushairi.*

***d)*** *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja****.*

***e)*** *Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | Jumla | |

## SEHEMU A:

***"Mapambazuko ya Machweo na hadithi nyingine"*** **Swali la lazima**

**1.** Swala la Elimu limepewa kipaumbele katika hadithi ya sabina. Jadili **alama 20**

## *SEHEMU B:*
## *Chozi la heri*

***Chagua swali la 2 au 3***

**2.** "…….. wanahofia kusema wasije wakavikata viganja vinavyowalisha……..

(a)Eleza muktadha wa dondoo hili (ala. 4)

(b) Taja maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili na ueleze (ala. 2)

(c)Kwa kutoa hoja kumi, eleza namna maudhui uliyotaja hapo juu (2b) yanavyojitokeza katika riwaya (ala. 10)

(d) Eleza sifa nne za msemaji (ala. 4)

**3.** (a) Migogoro ni maudhui muhimu katika riwaya hii. Fafanua (ala. 10)

(b) Uozo umetamalaki katika jamii ya *Chozi la Heri*. Tetea kauli hii kwa kutolea hija kumi zilizoelezwa (ala. 10)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**Bembea ya Maisha Jibu swali la 4 au 5**

**4.** ***Wewe unajua vote valivosemwa. hadharani na faraghani. Si makanisani, si magweni. leo nikiviona vitoto hivi vilivyochekwa na kusimangwa jana, vikijiendeshea mambo yao ninaridhika"***

**a)** Bainisha matokeo ya maneno yaliyopigiwa mstari **alama6)**

**b)** Eleza sifa za mwanawe msemewa **alama4)**

**c)** Kwa hoja kumi, jadili namna suala la malezi lilivyoangaziwa katika tamthilia. **alama10)**

**5.** ***Naam, bembea! Hata ikiwa ya kamba au chuma hatimaye hulika. Wanasema papo kwa papo kamba hukata jiwe. Bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa mchezo. Huungwa na mchezo kuanza tena.***

**a)** Jadili dhana 'bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa mchezo. ' Ukirejelea tamthilia **(alama10)**

**b)** Jadili namna wahusika tofauti wanavyounga bembea **(alama10)**

## SEHEMU D: USHAIRI

***Jibu swali la 6 au la 7***

**6. Shairi**

La adhabu hili wingu, lataka kutunyeea
Himahima kwalo vungu, pasi nako kuchelea, Kujikinga hili wingu, sije katunyeshea.

Wengineo hawajali, wasinayo wasiwasi, Tahadhari hawabali, wajiunge nasi
Aidha watafakali, mengine yalo hasi.

Vua hili halibagui, jinsia wala umri, Na kama hawajui, tuwajuze vizuri, Kwani siso adui, kuwao msumari.

Tangazo haliwapiku, wahimizwa kujikinge, Wingu hili la usiku, ukicheza likuringe, Latutia usumaku, daima likunyonge.

Vumilia kwalo vungu, nje kuna dhoruba,
Yavuma kwa machungu, bila lolote huba, Tunza chako kijungu, fungia kwalo juba.

Japo nafika tamati, nawaacha tafakari,
Madhara linalo wananti, wingu hili sukari,
Daima mwape kujiseti, mjitunze kujijari

**Maswali**

**1.** Eleza ujumbe wa mwandishi katika ubeti wa nne **(ala. 2)**
**2.** Onyesha ufundi wa kimuundo wa mwandishi katika utunzi wa shairi hili **(ala. 4)**
**3.** Eleza namna jazanda imetumika katika utungo huu. **(ala. 2)**
**4.** Kwa kuzingatia idadi ya mishororo katika beti tambua aina ya ushairi huu **(ala. 1)**
**5.** Tamthini ustadi wa mshairi katika matumizi yaidhini ya kishairi **(ala. 3)**
**6.** Litie shairi hili katika bahari tatu tofauti **(ala. 3)**
**7.** Andika ubeti wa **nne** kwa lugha ya tutumbi **(ala. 4)**
8. Eleza sifa moja ya nafsi neni katika shairi hili **(ala. 1)**

**7. Ushairi**

**Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yanayofuata**

**1.** Maendeleo ya umma Sio vitu maghalani
Kama tele vimesaki
Lakini havishikiki Ama havikamatiki
Ni kama jinga la moto

Bei juu

**2.** Maendeleo ya umma
Sio vitu gulioni
Kuviona madukani
Kuvishika mikononi
Na huku wavitamani Kama tama ya fisi
Kuvipata ng'o

**3.** Maendeleo ya umma
Sio vitu shubakani
Dhiki ni kwa mafakiri
Nafuu kwa matajiri
Ni wao tu washitiri

Huo ni ustiimari
lo! Warudia

**4.** Maendeleo ya umma Ni vitu kumilikiwa
Na wanyonge kupatiwa
Kwa bei kuzingatiwa
Bila ya kudhulumiwa
Na hata kuhadaiwa
Hiyo ni haki

**5.** Maendeleo ya umma  Dola kudhibiti vitu
Vijapo nchini mwetu
Na kuwauzia watu
Toka nguo na sapatu
Pasibakishiwe na kitu
Huo usawa

**6.** Maendeleo ya umma
Watu kuwa na kauli Katika zao shughuli
Vikaoni kujadili
Na mwisho kuyakubali
Maamuzi halali

Udikteta la

**7.** Maendeleo ya umma
Watu kuwa waungwana
Vijakazi na watwana
Nchini kuwa hakuna
Wote kuheshimiana
Wazee hata vijana

**Maswali**

**(a)** Toa anwani mwafaka ya shairi hili **(ala. 1)**

**(b)** Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu zako **(ala. 2)**

**(c)** Eleza dhamira ya mwandishi kuandika shairi hili **(ala. 3)**

**(d)** Toa mifano miwili ya urudiaji katika shairi hili, Je urudiaji huu una kazi/majukumu gani? **(ala. 4)**

**(e)** Onyesha matumizi mawili ya tamathali za usemi katika shairi hili **(ala. 4)**

**(f)** Eleza toni ya mshairi. Toa sababu **(ala. 2)**

**(g)** Nafsineni ni nani? **(ala. 1)**

**(h)** Toa mfano mmoja wa twasira katika hili. Je, twasira hiyo inajengwa na nani? **(ala. 3)**

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8. (a)** Fafanua sifa za matambiko katika jamii **(ala. 4)**

**(b)** Eleza tofauti kati ya maigizo ya kawaida na maonyesho ya sanaa **(ala. 10)**

**(c)** Taja shughuli zozote mbili zinazoonyesha matumizi ya Ulumbi katika jamii ya kisasa **(ala. 2)**

**(d)** Tofautisha dhana zifuatazo

**(i)** Miviga na maapizo **(ala. 2)**

**(ii)** Ngoma na ngomezi **(ala. 2)**

# *To Obtain Copies of Respective Marking Schemes / Answers*

## CALL/TEXT/WHATSAPP

## *0746-222-000*

## *0742-999-000*

*mwalimuconsultancy@gmail.com*

***This is a Copyright Property of Mwalimu Consultancy Ltd.***

# *Powered By Mr Isaboke*

*Ukihitaji majibu, Piga 0746 222 000 / 0742 999 000*